**20 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 20 Mei, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Waziri nenda upande wa pili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tutaanza na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Jesca kwa niaba ya Mheshimiwa Sekiboko.

Na. 376

### Kurekebisha Madaraja ya Watumishi wa Umma

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, lini watumishi wa umma watarekebishiwa madaraja hasa walimu waliopandishwa na kunyang'anywa mwaka 2016 - 2018 kupisha uhakiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 Serikali ilisitisha mambo mbalimbali ya kiutumishi ikiwemo upandishaji vyeo ili kupisha zoezi la uhakiki wa taarifa za kiutumishi na vyeti vya elimu kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua changamoto zilizojitokeza kutokana na sitisho hilo mwaka 2021/2022 Serikali ilianza kutekeleza zoezi la kuwarejesha watumishi wa umma wa kada mbalimbali kwenye nafasi na vyeo vyao stahiki kwa njia mbalimbali ikiwemo msawazo wa vyeo na mserereko wa madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 hadi sasa jumla ya watumishi 375,904 wamepandishwa vyeo wakiwemo watumishi 85,471 walioathirika na zoezi la uhakiki. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 81,503 wakiwemo walimu walioathirika na zoezi la uhakiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uhakiki umefanyika tangu mwaka 2018 lakini wapo walimu mpaka leo wanadai malipo yao kulingana na madaraja ambayo wamepandishwa bila *impact* kwenye mishahara yao, ni ipi kauli ya Serikali juu ya walimu wenye madai haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo watumishi katika kada mbalimbali ambao wamekuwa wakidai *arrears* kwa miaka mingi zaidi ya miaka mitano, je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha madeni haya ya watumishi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Husna Sekiboko

anayeuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kulipa madai mbalimbali ya mishahara, lakini pia madai mbalimbali ya madeni ambayo yaliachwa kutokana na zoezi linaloendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Bunge lako lilitoa maelekezo kwa Serikali na Serikali ilifanya utaratibu wake wa kuwajulisha waajiri wote walete taarifa za watumishi wote ambao wana madai kwenye Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha tumetenga nafasi 52,551 kwa ajili ya kwenda kulipa madeni yote ambayo watumishi wanadai ambayo tayari yamehakikiwa. Kwa wale ambao hawajaleta madai ya watumishi wetu katika maeneo mbalimbali, msisitizo wangu katika asubuhi ya leo, ni kuendelea kuwakumbusha tena waajiri wote leteni madeni tunayodaiwa kwa sababu hii ni haki ya watumishi wa umma kulipwa na Serikali yao inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Bunge lako lilitupitishia bajeti na kwa kweli tunakushukuru wewe Naibu Spika kwa niaba ya Bunge na nataka niwahakikishie watu wote ambao madeni yao hayajalipwa, nataka nirudie tena, waajiri leteni taarifa zao na Serikali ipo tayari kwa ajili ya kuyalipa madeni yote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Nishati Mheshimiwa Kapufi.

Na. 377

**Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo Mkuu Tabora – Mpanda**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa njia ya umeme ya msongo mkuu Tabora – Mpanda utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilometa 383 kutoka Tabora hadi Mpanda, Katavi lengo likiwa ni kuunganisha Mkoa wa Katavi katika Gridi ya Taifa. Gharama za mradi huu ni shilingi bilioni 116. Aidha, utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Septemba, 2022 na umefikia 58%, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru swali langu la msingi linauliza ni lini mradi huu utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza narudia, ni lini mradi huu utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nini mpango wa Serikali katika kunusuru Mji wa Mpanda dhidi ya katikakatika ya umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia mradi huu wa kufikisha umeme wa Gridi ya Taifa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na lini mradi huu utakamilika? Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Wana-Mpanda na watu wa Katavi wote kwa ujumla. Suala la kupeleka Gridi ya Taifa Mpanda na Katavi ni suala la kipaumbele chini ya Awamu ya Sita kuhakikisha mikoa yote ambayo haijaunganishwa na Gridi ya Taifa inaunganishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba kwa niaba ya watu wa Katavi watuvumilie kidogo, mradi unaenda vizuri na kwa

maelekezo ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati tunasimamia kwa weledi mkubwa sana na nina imani miezi michache ijayo tutakuwa tumekamilisha hii njia ya kusafirishia umeme, uzuri kituo cha kupooza umeme kimeshafikia 98%. Kwa hiyo, ni njia tu hii ya kusafirishia umeme itakamilika hivi karibuni na watu wa Katavi watapata umeme wa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, tunaelewa umuhimu wa umeme wa uhakika Mpanda na Katavi kwa sababu wananchi wa Katavi ni wafanyakazi wazuri sana. Sasa kwa hatua za haraka, kwa maelekezo ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati leo mafundi wetu watafungua mtambo wa megawati moja Biharamulo ili kuweza kuupeleka Mpanda pale ili kuweza kuongeza uzalishaji kwa sababu mahitaji ni megawati saba, lakini tunazalisha karibia megawati 6.15 tutaongeza megawati moja ili tuweze kupunguza mgao Katavi pamoja na Mpanda, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, Serikali inatambua kwamba njia hiyo ya umeme haiwezi kukamilika bila kuwalipa wananchi wa Sikonge fidia ya shilingi bilioni 2.2 ambayo bado Wizara ya Fedha haijaipa Wizara ya Nishati hizo hela.

Sasa ni lini Wizara ya Fedha itatoa fedha hizo ili Wizara ya Nishati walipe fidia hiyo ili kukamilisha huo mradi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fidia la wananchi hawa wa Sikonge tayari tunalifanyia kazi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tupo kwenye hatua za mwisho kwa ajili ya kufanya malipo haya na uzuri Wizara ya Fedha wameshaji-*commit* kwamba wanatoa fedha kwa ajili ya kulipa fidia wananchi hawa. Tunaomba wananchi wa Sikonge, Tabora na yale maeneo ambayo wanadai fidia katika mradi huu wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Mpanda waendelee

kutuvumilia, tutalipa fidia hiyo kwa sababu tayari tulishaji-*commit* kwamba tutalipa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Kapinga.

Na. 378

**Ujenzi wa Barabara ya Kigonsera – Matiri**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Kigonsera hadi Matiri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kigonsera – Matiri yenye urefu wa kilometa 25 ni sehemu ya barabara ya mkoa ya Kigonsera – Kilindi – Mbaha yenye urefu wa kilometa 55 inayounganisha barabara kuu ya Songea – Mbinga na mwambao wa Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kuifungua barabara hii inayoanzia Kigonsera hadi Mbaha ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Hadi sasa jumla ya kilometa 35 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe, kilometa 12 zimefunguliwa na jitihada za kufungua sehemu iliyobaki ya kilometa nane zinaendelea. Mara baada ya kazi hii kukamilika, barabara hii itafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nishukuru kwa majibu ya Serikali lakini swali langu mimi nimeuliza ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha

lami? Na hii ni ahadi ya Rais, ni lini siyo hayo maelezo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa.

Kwa hiyo, bado naendelea kuuliza ni lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Barabara za Jimbo la Mbinga Vijijini kutokana na mvua zilizonyesha zimeharibika sana na zimeleta usumbufu mwingi sana kipindi hiki cha mvua. Barabara ya kutoka Kingori hadi Paradiso, Barabara ya kutoka Njia Panda Rugali - Mkumbi pia Barabara ya Nyoni - Tingi barabara hizi ni mbovu sana. Je, Serikali ina mkakati gani kupitia hizi fedha za dharura kuzijenga barabara hizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga, Naibu Waziri amesema hivi mara baada ya kazi hii kukamilika barabara hii itafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya ujenzi wa kiwango cha lami. Mheshimiwa Naibu Waziri endelea kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge swali la pili kama Mheshimiwa Naibu Spika ulivyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara za Jimbo la Mbinga kwa maana ya Wilaya ya Mbinga zimeharibika na hii ni pamoja na barabara zote nchi nzima kutokana na mvua ambazo zimenyesha sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote, Serikali imeshafanya tathmini ya uharibifu wa miundombinu na hasa barabara nchi nzima na tayari sasa hivi tupo tunatafuta fedha na nina uhakika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa kipaumbele kikubwa kuhakikisha kwamba baada ya kurejesha mawasiliano tutahakikisha kwamba tunarudisha barabara zote kwenye hali yake ya kawaida.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwamba mpango upo mkubwa ambao Serikali inafanya kuhakikisha kwamba inarejesha mawasiliano, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daktari Mhagama.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Serikali imeona kwa uhakika kabisa uwezo wa *TARURA* wa kuhudumia barabara ya Wino - Ifinga yenye urefu wa kilometa 48 ni mdogo. Ni lini sasa Serikali itakubali maombi ya Halmashauri ya Madaba kupitia mkoa kuijenga Barabara ya Wino - Ifinga kwa kupitia Mfuko wa *TANROADS?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara ambazo zinakuwa na sifa na zinakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tayari barabara yake imeshakuja ofisini kwetu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba timu ya wataalamu itakwenda kuhakiki hiyo barabara na kama itakidhi vigezo, Wizara ya Ujenzi kupitia Waziri wa Ujenzi hatasita kuipandisha barabara hiyo ili iweze kuhudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, ajiandae Raymond.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya kutoka Kolandoto - Munze – Mwangongo upembuzi yakinifu umeshafanyika; je, ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ni kati ya barabara kuu ambayo ni *track road* na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba asubiri katika bajeti hii inayokuja, ni barabara ambazo tumezifikiria kama bajeti itapitishwa basi itakuwa ni kati ya barabara ambazo zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond, ajiandae Mtemvu.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuwa Barabara ya Rau - Kinyamvuo na Rau - Shimbwe kupitia Mamboleo ni ahadi ya wakuu wa Serikali kuanzia Rais wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa mpaka leo na sasa hivi baada ya mafuriko wananchi hao hawatoki ndani. Ni lini barabara hizo zitajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na kupitia Bunge hili nimwagize Meneja wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa sababu kama wananchi bado mpaka dakika hii mvua zimepungua hawawezi kutoka ndani, nimwagize Meneja wa Mkoa wa Kilimanjaro aweze kutembelea hizo barabara na aweze kuleta mahitaji haraka Wizarani ili tuweze kurejesha mawasiliano kwa wananchi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa ahadi hizo Mheshimiwa Mbunge naomba nikajiridhishe tuone tumefikia hatua gani kwa maana ya kufanya maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami kama viongozi wetu wa Kitaifa walivyotoa ahadi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mkwamo wa kuendelea kuijenga barabara ya Makondeko – Kwembe – Kisokwa hadi Mloganzila na Serikali imejenga kilometa nne tu kutoka Kibamba hadi Mloganzila; je, Serikali mko tayari kuanza kujenga kipande cha Makondeko hadi Kwembe kwa kilometa nne tu angalau ili wananchi waweze kuishi salama kwenye barabara ile?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ni kati ya barabara ambazo tunasema katika

Mkoa wa Dar es Salaam ni barabara ambazo zinapunguza msongamano na bado tutaendelea kuijenga. Sina uhakika kama ni kilometa nne, lakini zipo kwenye mpango wa kuhakikisha kwamba zile barabara zote tunazikamilisha ikiwa hatua madhubuti ya Serikali kupunguza misongamano ya magari katika Jiji la Dar es Salaam, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aziza.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kuinusuru Barabara ya Itigi – Tabora ambayo imejengwa kwa muda mfupi na imeshaanza kuharibika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokifahamu ni kwamba Barabara ya Itigi – Tabora imejengwa yote kwa kiwango cha lami na kama kuna uharibifu ambao siyo wa kawaida na najua ni barabara ambayo siyo ya muda mrefu, namwomba Mheshimiwa Mbunge aweze kutusaidia ama niwaagize Mameneja wa Mkoa wa Singida na Tabora waweze kupita katika barabara hiyo ili waweze kujiridhizisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri baadaye muone Mbunge akueleze ni sehemu gani? Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Barabara ya Kiberashi – Chemba – Kwa Mtoro mpaka Singida tumeshasaini mkataba, lakini mpaka leo ni kimya; nini kauli ya Serikali kuhusiana na barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali kwa barabara hizi zote pamoja na hiyo ya Handeni – Kiberashi – Chemba – Kwa Mtoro ni barabara ambazo zipo kwenye mpango na Serikali kweli tusaini mkataba, tuko kwenye hatua za mwisho za manunuzi. Baada ya wakandarasi hao kuzipitia hizo barabara ili tuweze kuzijenge kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri kauli ya Rais ni jibu la kufanyia kazi, malalamiko mengi kwa Wabunge ni ahadi za Rais kujenga barabara wakati wa kampeni; je, hauoni sasa ni wakati wa kukusanya barabara zote ambazo Rais aliomba ili ziweze kufanyiwa kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa huo ni ushauri uchukue.

Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila.

Na. 379

**Ujenzi wa Madaraja ya Bujonde na Ilondo Mwaya – Kyela**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Madaraja ya Bujonde na Ilondo Mwaya - Kyela utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ujenzi wa Daraja la Bujonde linalounganisha Kata ya Kajunjumele na Bujonde. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imefikia 85% na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2024. Baada ya kazi ya usanifu kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Daraja la Ilondo - Mwaya, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu

na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kulijenga daraja hili, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, wakati Serikali inaendelea na upembuzi yakinifu, je, ni mkakati gani unafanywa kwa barabara ambazo zinaunganisha madaraja hayo mawili, kati ya Kajunjumele – Mwaya – Lusungo na Matema?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Daraja la Bujonde pia lina kipande cha barabara cha Ibanda – *Itungi Port*, je, baada ya kumwondoa mkandarasi nini mkakati wa Serikali kwa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyojenga madaraja ambayo mara nyingi ndiyo kikwazo kikubwa cha kuunganisha eneo na eneo Serikali itazijenga hizo barabara ambazo zinaunganisha haya madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu baada ya kumwondoa mkandarasi, kwanza nimwagize Meneja wa Mkoa wa Mbeya kwamba kama kuna changamoto zozote ambazo zinaendelea sasa hivi ahakikishe kwamba anaweka utaratibu wa kuzikarabati hizo barabara wakati Serikali inakamilisha taratibu za kuweza kufanya tathmini na kuona namna ya kusimamisha au kusitisha mkataba na mkandarasi ambaye alikuwa amepewa barabara hii kwa kufuata taratibu zote za mkataba, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kigua.

Na. 380

**Ujenzi wa Barabara ya Kiberashi hadi Songe – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Kiberashi hadi Songe Kilindi kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kiberashi – Songe (Kilindi) – Kwaluguru yenye urefu wa kilometa 127 imeingizwa kwenye Mpango wa Bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa ajili ya kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kazi hii ikikamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kipande cha makao makuu ya wilaya kwenye Kata ya Songe na Bokwa ujenzi unaendelea na sehemu zimekamilika, lakini hakuna taa na maeneo hayo yanakuwa yanapata ajali; je, Serikali ni lini itaweka taa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kipande cha Handeni – Kiberashi katika zile kilometa 20 baadhi ya wananchi wamepisha ujenzi wa kiwango cha lami lakini hawajalipwa fidia hadi leo; je, nini mpango wa Serikali wa kuwalipa fidia wananchi hawa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa Serikali kwa sasa ni kuhakikisha kwamba makao makuu ya wilaya tunaweka taa na ndiyo kipaumbele na sasa hivi tunafanya manunuzi ya taa kwa ujumla wake. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge tuone kama makao makuu ya wilaya yake ipo kwenye mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulipaji wa fidia kwa wananchi hawa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba limekuwa ni suala ambalo Mheshimiwa Mbunge tunajua umekuwa unalifuatilia na sisi kama Wizara tumeshawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili waweze kukamilisha taratibu za malipo ili wananchi hao ambao wamepisha ujenzi wa mradi huo waweze kulipwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Tabasamu, kwa niaba Mheshimiwa Mkundi.

Na. 381

**Ujenzi wa Feri ya *MV* Buyagu**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza:-

Je, lini mradi wa ujenzi wa Feri ya *MV* Buyagu utakamilika ikizingatiwa kuwa mkataba wa ujenzi umekwisha muda wake Aprili, 2024?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajenga kivuko kipya kitakachokuwa kiunganishi muhimu kati ya Wilaya ya Sengerema na Wilaya ya Misungwi kupitia eneo la Buyagu lililoko Sengerema na eneo la Mbalika lililopo Misungwi. Mkataba wa ujenzi wa kivuko hiki ulisainiwa mwezi Aprili, 2023 kati ya Serikali kupitia *TEMESA* na mkandarasi *Songoro Marine Transport Mwanza*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za ujenzi wa kivuko hiki zimepangwa kukamilika mwezi Agosti, 2024 baada ya muda wa awali kuongezwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina masali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kwa kuwa ujenzi wa kivuko hiki ulikuwa unaenda sambamba na ujenzi wa gati, Gati la Mbarika na Gati la Buyagu, wananchi wa Wilaya ya Sengerema wanataka kujua ni lini sasa gati hizi zitakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Kivuko cha Kisorya kwenda Ukerewe kimekuwa ni hatari sana kwa maisha ya wananchi wa Ukerewe na kwa kuwa kivuko hicho pamoja na Kivuko cha Bukondo Bwiro, Kivuko cha Kome na hiki Kivuko cha Buyagu vyote vilitakiwa kukamilika pamoja; nini kauli ya Serikali ili tusisubiri yakatokea mambo ya kutisha ndiyo tukakurupuka kwenda kufanya shughuli zinazotakiwa pale? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Gati za Mbarika na Buyagu ziko kwenye mpango wa kujengwa na tutahakikisha wakati tunakamilisha kivuko na gati hizo ziwe zimekamilika ili kivuko hiki kiweze kufanya kati ya pande hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kivuko cha Kisorya ambacho kina-*operate* kati ya Kisorya na Rugenzi ikiwa ni pamoja na vivuko vingine, maana tuna vivuko vipya zaidi ya vitano ambavyo vinajengwa na tuna uhakika kwamba pengine kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu vivuko vyote vitakuwa vimeshakamilika kwa sababu vingi viko zaidi ya 75% vikiwa vinajengwa pale *Songoro Marine* pale Mwanza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Antipas, kwa niaba Mheshimiwa Inno.

Na. 382

**Fidia kwa Wananchi wa Kijiji cha Ngombo – Malinyi**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS K.n.y. MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kulipa fidia wananchi wa Kijiji cha Ngombo waliopisha Hifadhi ya Pori Tengefu la Kilombero?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Ngombo kipo katikati ya eneo la ardhi oevu ndani ya Pori Tengefu Kilombero. Uwepo wa kijiji hiki pamoja na vijiji vingine ndani ya pori hilo ulifanya ukubwa wa eneo la pori kupungua kwa 61.5% kutoka kilometa za mraba 6,500 hadi kilometa za mraba 2,500. Hali hiyo ilipelekea Serikali kupitia Kamati ya Mawaziri Nane kuelekeza Kijiji cha Ngombo kufutwa na wananchi wake kuhamishiwa maeneo mengine sambamba na eneo la Pori Tengefu Kilombero kupandishwa hadhi kuwa Pori la Akiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hatua hiyo, Serikali imeshakamilisha zoezi la uthamini kwa wananchi wa Kijiji cha Ngombo kwa vitongoji vyote vitatu vinavyounda Kijiji hicho ambavyo ni Idenge, Ikwachu na Ifuru. Aidha, jumla ya shilingi 7,351,097,480.46 zimeainishwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi hao. Wizara inasubiri fedha kutoka Hazina ili iweze kulipa fidia kwa wananchi ili waweze kuondoka katika eneo la hifadhi na eneo hilo kuendelea kusimamiwa kama Pori la Akiba Kilombero kwa mujibu wa Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Sura ya 283.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Inno.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, pamoja na majibu

mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa wa Kijiji cha Ngombo wamekaa muda mrefu wakisubiri hiyo fidia ili waweze kuondoka kiasi ambacho wameshindwa kulima lakini pia wameshindwa shughuli nyingine zozote za kijamii ili kuweza kukidhi mahitaji yao na familia zao; je, nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati kipindi hiki tunasubiri kupata fidia, je wananchi waendelee kuandaa mashamba yao ili kusudi waweze kujipatia chakula na kipato kwa ajili ya familia zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninawashukuru wananchi hawa kwa jinsi ambavyo wamekuwa na subira kuruhusu mchakato huu wa fidia ambao ni muhimu sana kufanyika uweze kukamilika. Nawaomba waendelee kuwa na subira, tunaamini ndani ya kipindi kifupi fidia hii itapatikana, kwa hiyo, wataendelea na maisha yao kama kawaida.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, hivi sasa utaratibu wa fidia nchini kwa wanaoathiriwa na wanyama haueleweki vizuri. Serikali ina mpango gani wa kuweka wazi utaratibu huu wa fidia kwa wananchi wanaoathiriwa na wanyama katika mali zao na maisha yao?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, fidia kwa wananchi wanaopata madhara ya wanyama inafanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni ambayo iko wazi na tumekuwa tukiisema mara kadhaa katika Bunge hili na kwa bahati nzuri kanuni hizi zimesambazwa kwa Maafisa Hifadhi wote

wa halmashauri zetu ambao tunaamini na wao wanafanya kazi ya kutoa semina kwenye vijiji vyetu, lakini kama haieleweki natoa rai kwa Maafisa Wanyamapori katika halmashauri zetu waendelee kufanya kazi nzuri hii ya kutoa elimu kwa wananchi ili jambo hili lieleweke.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Genzabuke.

Na. 383

**Mgogoro wa Mpaka kati ya Vijiji na *TFS***

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafika katika Kata ya Kagerankanda kutatua mgogoro wa mpaka baina ya vijiji na *TFS*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Kagerankanda inaundwa na vijiji viwili vya Mvinza na Kagerankanda. Kata hiyo inapakana na Hifadhi ya Msitu wa Makere Kusini uliohifadhiwa kwa *TSN* ya tarehe 10 Agosti, 1953. Kwa sasa hifadhi hii ina ukubwa wa hekta 65,178 kutoka hekta 75,190 zilizokuwepo awali. Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya jamii hasa ardhi kwa ajili ya kilimo, makazi na malisho ya mifugo, hifadhi hii ilikumbwa na uvamizi kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Hivyo Serikali iliridhia maombi ya wananchi ya kumega sehemu ya eneo lake kwa ajili ya kutumiwa na jamii hizo. Taratibu hizi zilikamilika kwa kupitia *TSN* 718/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, umegaji wa hifadhi hii ulifanyika kwa kuzingatia maelekezo ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka 2017. Kufuatia maelekezo yake, Hifadhi ya Makere Kusini iliondolewa jumla ya hekta 10,012 na kugaiwa kwa wananchi wa maeneo hayo pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na katika eneo lililomegwa, Kijiji

cha Kagerankanda kilipata jumla ya hekta 2,496, Kijiji cha Mvinza hekta 2,174 na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kupewa jumla ya hekta 5,342.16.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, wananchi wa Vijiji vya Mvugwe, Makere, Kitagata, Nyachenda, Nyamidaho, Mugombe na Nyakitonto na kata nyingine ambazo sikuzitaja zimezunguka Hifadhi ya Makere Kusini na kwa sasa wananchi hao wanazuiliwa kuvuna mazao yao; je, Serikali iko tayari kuiagiza *TFS* na watu wa Kitalu cha Kagerankanda kilichopo Kabulanzwili ili wananchi waweze kuvuna mazao yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kati ya ekari 10,000 zilizotolewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Magufuli ni vijiji viwili tu vilivyoweza kupata ambapo ekari 2,496 ziligaiwa Kijiji cha Kagerankanda na Kijiji cha Mvinza kilipata hekta 2,174, lakini ekari hizo 5,000 zilizobaki zimechukuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Vijiji vyote hivyo nilivyovitaja kwa maana ya Mvugwe, Makere, Kitagata, Nyachenda, Mugombe, Nyakitonto, Nyamyusi na Kulugongo vyote vinategemea hifadhi hiyo ya Makere.

Je, Serikali iko tayari kukaa na Wizara ya TAMISEMI ili hizo hekta 5,000 zilizochukuliwa na Halmashauri ya *Kasulu DC* zirudishwe kwa wananchi wa vijiji hivyo niulivyovitaja?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Genzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili la wananchi kulima kwenye hifadhi limekuwa likiendelea kwa muda mrefu, lakini

vilevile tulipata maombi ya Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma na Kagera tulipokaa nao kwamba yale maeneo ambayo wananchi wamelima kwenye hifadhi waruhusiwe kuvuna mazao yao, lakini wasiruhusiwe kulima tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekwishatoa maelekezo kwa wahifadhi wetu wa maeneo haya kwamba wananchi waliolima kwenye hifadhi waruhusiwe kuvuna mazao yao, lakini wasiruhusiwe kuendelea kupanda kwenye hifadhi hizi. Ninawakumbusha wahifadhi wetu agizo hili bado linasimama na sasa Serikali au Wizara tutafuatilia wahifadhi wetu wote ambao hawajatekeleza agizo hili na hatutasita kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, wakati tulipopata maelekezo ya kumega ardhi kwa vijiji hivi, vilevile tulipewa maelekezo ya kutenga eneo kwa ajili ya halmashauri kwa shughuli za uwekezaji, lakini vilevile kuwa akiba endapo yatatokea mahitaji ya ziada, wananchi waweze kupewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu eneo hili sasa hizi hekta 5,000, zinamilikiwa kisheria na halmashauri, tutaendelea kuwasiliana na wenzetu wa halmashauri kuona namna bora ya ardhi hii kutumika kwa mujibu wa sheria kwa sababu halmashauri hii wananchi hawa ni wananchi wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Paresso.

Na. 384

**Kukamilisha Mradi wa Maji Kijiji cha Chemchem - Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji katika Kijiji cha Chemchem – Karatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.
**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Chemchem unaohusisha ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 135,000 kwenye mnara wa meta sita, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 16.5, ujenzi wa vituo 14 vya kuchotea maji, ujenzi wa ofisi ya *CBWSO*, ujenzi wa nyumba ya kuendeshea mitambo *(pump house),* kufunga mfumo wa umeme jua *(solar system)* pamoja na ujenzi wa mbauti ya kunyweshea mifugo *(cattle trough)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 85% na umeanza kutoa huduma ya maji safi na salama kwenye baadhi ya maeneo ikiwemo; Shule ya Msingi Chemchem, Shule ya Sekondari Chemchem na Zahanati ya Chemchem. Utekelezaji wa mradi huo unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2024 na kunufaisha wananchi wapatao 6,010 wa Kijiji cha Chemchem, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sensa iliyopita, wanufaika wameongezeka katika kijiji hicho na wananchi wamekuwa wanatarajia mradi huu ukamilike kwa wakati kwa sababu umekuwa ni mradi wa muda mrefu sana

Je, ni lini kwa uhakika, kwa sababu kilichopo *site* na unachokisema kina tofauti kidogo, ni lini kwa uhakika wananchi hawa watarajie kupata mradi huu wa maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuna wananchi wa vijiji vya jirani ikiwemo Rhotia Juu pamoja na Kilimatembo Juu, ni lini na wananchi hawa wataweza kupata maji kwa sababu vijiji hivyo havina maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli natambua na Serikali inatambua uwepo wa changamoto hii katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge analiongelea na ni kiu ya Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya maji. Ni kweli mradi huu umechukua muda mrefu, ni kweli kabisa kwa sababu ya hatua mbalimbali ambazo zilikuwa zinachukuliwa na Serikali ikiwemo utafutaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kwa mujibu wa majibu yangu ya msingi, mradi huu unaenda kukamilika Juni, 2024. Kwa hiyo, hiyo ndiyo kauli ya Serikali kuhusiana na mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika eneo la Kilimatembo pamoja na Rhotia, kuna mradi ambao unaendelea pale, lakini Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kukarabati na kupanua miundombinu ili tufikishe huduma ya maji katika maeneo yanayozunguka katika mradi ule na Kijiji cha Kilimatembo pamoja na Rhotia wataweza kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa Kata za Kimyaki, Siwandeti, Kiranyi, ambayo ni maeneo yenye wananchi wengi zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba watu wanapata *accessibility*

ya maji safi na salama na tuna mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba vijiji ambavyo vimebaki havina maji, lakini kulingana na programu ya kila Mbunge kupata vijiji vitano ambavyo vitapata huduma ya maji. Tutaangalia sasa kwamba ni vijiji vingapi ambavyo vitakuwa vimebaki havina huduma ya maji ili Serikali iweke mkakati maalum kwa ajili ya kuhakikisha tunafikisha huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambako miradi ya maji bado haijakamilika, tuna maelekezo mahsusi kutoka kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha kwamba miradi yote ambayo imekwama basi tunaikwamua ili wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nataka kujua ni lini Serikali itapeleka fedha katika Mradi wa Maji Itumba - Isongole ulioko Wilaya ya Ileje ili wananchi waweze kunufaika na maji hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Stella kwa kupitisha bajeti yetu ya maji kwa kishindo kabisa, alikuwa anapitisha huduma ya maji kwa wananchi wa Ileje. Kwa kupitisha bajeti hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapoingia sasa kwenye utekelezaji, tutapeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mradi huo unaenda kukamilika na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi; je, ni lini Mradi wa Maji wa Kata ya Ruaha Mbuyuni katika Wilaya ya Kilolo utakarabatiwa? Kwa

sababu Mto wa Lukosi ulipochepuka uliondoa mabomba yote kwa hiyo, wananchi wa Ruaha Mbuyuni wanapata shida sana kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia changamoto ambayo imejitokeza katika mto ule. Ni kweli kabisa Serikali inatambua kuna mabomba ambayo yalipitiwa kulingana na mto jinsi ulivyokuwa umechepuka, lakini pia wakati tunajaribu kuweka jitihada za kurejesha huduma, bado mabomba yalipata changamoto. Serikali imeshatenga fedha na tayari tunanunua mabomba kwa ajili ya kwenda kurekebisha eneo lile ili kurudisha huduma haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetenga kiasi cha shilingi bilioni 5.56 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu yote ya maji ndani ya Jimbo la Kilolo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Bilakwate.

Na. 385

**Kibali cha Ujenzi wa Mradi wa Maji – Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza: -

Je, lini kibali cha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Kyerwa, Nyaruzumbura, Nyakatuntu, Kamuli kitatolewa ili ujenzi uanze?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji utakaonufaisha vijiji 57 wilayani Kyerwa ikiwemo Kyerwa Mjini, Nyaruzumbura, Nyakatuntu hadi Kamuli kwa kutumia chanzo cha Mto Kagera. Aidha, katika mpango wa muda mfupi, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji itakayonufaisha vijiji 27 vya Nkwenda, Rwabwere, Karongo, Nyamiaga, Nyakatera, Kagu, Masheshe, Nyamweza, Kaikoti, Iteera, Muleba, Chanya, Kimuli, Rwanyango, Chakalisa, Kikukuru, Omukitembe, Karambi, Rwele, Rubilizi, Mukunyu, Kitwechenkura, Rukuraijo, Makazi, Kibimba, Nyakatete na Mabira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali katika mwaka wa fedha 2024/25 itachimba visima katika Vijiji vya Omuchwenkano, Businde, Nyaruzumbura, Bugara, Rukiri, Nyakatuntu, Kyerere, Kamuli, Ibamba na Rukuraijo ili kuongeza vyanzo vya maji. Kukamilika kwa miradi hiyo kutaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji wilayani Kyerwa kufikia wastani wa 80.3% mwezi Juni, 2025. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kabla sijauliza maswali ya nyongeza, ninaomba nitoe pole kwa Wana-Kyerwa na Wizara ya Maji kwa kumpoteza Meneja wetu wa Wilaya, ndugu yangu Tungaraza, tunawapa pole sana Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza; pamoja na Serikali kuweka mpango wa kuchimba visima vya maji, kuna visima ambavyo vimechimbwa zaidi ya miezi sita na mpaka sasa hivi visima hivi bado havijajengewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini visima hivi vitajengewa kwenye Kata ya Kibale, Kijiji cha Kigologolo, lakini pia kwenye Kata ya Businde, Kijiji cha Omuchwenkano?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kuna mradi wa maji katika Kata ya Songambele, Kijiji cha Songambele, ni zaidi ya mwaka sasa tumepitisha kwenye bajeti mradi huu haujaanza. Ni lini mradi mradi huu utaanza ili kuwapatia wananchi wa Songambele maji safi na salama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kwa niaba ya *RUWASA* na Wizara ya Maji na sekta ya maji kwa ujumla tunapokea pole hizo kwa kuondokewa na *DM* wetu kutoka kule Kyerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu Kigologolo pamoja na Omuchwenkano, katika jibu langu la msingi nimeitaja Omuchwenkano, lakini vilevile katika Kigologolo, Serikali itaanza kwanza ukarabati kwa sababu ni kweli kabisa kisima kipo kimechimbwa, lakini bado ile miundombinu ya kusambazia maji haijakamilika na Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inafanya ukarabati wa miundombinu ili wananchi waweze kufikishiwa huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, katika mradi wa Songambele, kwanza nimpongeze sana kwa ufuatiliaji mzuri sana Mheshimiwa Innocent Bilakwate kwa ajili ya mradi huu na kwa ushirikiano ambao anaendeea kutupatia na sisi Serikali hatutamuangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huu fedha ambazo zilitengwa kwa bahati mbaya au nzuri hatukuweza kuzipata kwa wakati. Nimhakikishie katika mwaka wa fedha 2024/2025 mkandarasi anaenda kupatikana na mradi huu utaanza mara moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona, mwaka 2023/2024 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya mradi wa maji wa Kata za Itandula na Mbalamaziwa, Jimbo la Mufindi Kusini, lakini mpaka sasa fedha hizo hazijaenda. Ni lini Serikali itapeleka fedha hizo kukarabati mradi huo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua changamoto ya kucheleweshwa kufikishwa fedha katika mradi huo lakini nikuhakikishie kwamba kabla ya mwaka wa fedha haujaisha fedha hizo zitakuwa zimepelekwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Londo, kwa niaba Mheshimiwa Babu Tale.

Na. 386

**Msingi wa Wafanyabiashara Kutoza Bei tofauti au Fedha za Kigeni kwa Wateja Raia wa Kigeni**

**MHE. HAMISI S. TALETALE K.n.y. MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza: -

Je, ni nini msingi kwa wafanyabiashara kutoza bei tofauti au fedha za kigeni kwa wateja ambao ni raia wa kigeni na nini athari zake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Serikali imeandaa sheria na kanuni ili kumlinda mlaji na kuhakikisha kuwa bei za bidhaa na huduma zinapangwa kwa msingi wa nguvu ya soko. Kwa mantiki hii, biashara zimekuwa zikiendeshwa chini ya utaratibu wa soko

huria ambapo bei za bidhaa na huduma hupangwa kuendana na uwiano wa uhitaji na upatikanaji wa bidhaa husika. Hata hivyo, wafanyabiashara wanaweza kutoza bei tofauti kwa bidhaa na huduma baina ya wazawa na raia wa kigeni au kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine Serikali inatambua na imeendelea kukumbusha kuwa shilingi ndio fedha halali kwa ajili ya malipo mbalimbali hapa nchini. Kutokana na hilo, raia wa kigeni hawatakiwi kulazimishwa kulipa kwa fedha za kigeni hususan pale wanapokuwa na shilingi za Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, wageni wanaruhusiwa kutumia fedha za kigeni ili kurahisisha ufanyaji wa biashara pale wanapokosa shilingi za Kitanzania na viwango vya ubadilishaji fedha havikitakiwi kutofautiana na vile vinavyotozwa katika masoko ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna athari za kimsingi za uchumi kwa wafanyabiashara kutoza bei tofauti baina ya wateja raia wa kigeni na wazawa kwani bei hizo huamuliwa katika soko huru na hivyo inatarajiwa kupanda na kushuka kulingana na nguvu za mahitaji na ugavi sokoni, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Babu Tale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu ya Serikali, naamini tatizo litakuwa linakwenda kuisha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Babu Tale, umeridhika? Zungumza kwa sauti mzee wa vyombo.

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Iddi Kassim.

Na. 387

**Kutoa Msamaha wa Kodi kwa Wakandarasi Msalala**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kurahisisha mfumo mzuri wa kutoa msamaha wa kodi kwa wakandarasi wanaojenga barabara Halmashauri ya Msalala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, msamaha wa kodi kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya kimkakati ya Serikali unatolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 6 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani yaani *VAT* kama ilivyofanyiwa maboresho na Sheria ya Fedha ya mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho ya sheria hiyo yalilenga kurahisisha na kuongeza ufanisi katika utoaji wa msamaha wa kodi ambapo awali mamlaka ya kutoa msamaha yalikuwa chini ya Waziri wa Fedha. Aidha, kwa marekebisho hayo, mamlaka ya kutoa msamaha yakakasimishwa kwa Kamishna Mkuu wa *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maboresho ya sheria, Serikali kupitia *TRA*, ilianzisha kitengo maalumu kwa ajili ya kushughulikia misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kuanzishwa kwa kitengo hicho kumesababisha kuwa na muda mfupi zaidi wa kushughulikia maombi ya msamaha wa kodi hiyo ukilinganisha na wakati wa awali kabla ya maboresho hayo. Vilevile katika jitihada za kuongeza ufanisi na kutoa msamaha wa kodi ndani ya muda mfupi, Serikali ilianzisha mfumo wa kieletroniki wa kuwasilisha maombi hayo *TRA (Tax Exemption Management System)*, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mamlaka ya utoaji msamaha wa kodi yamewekwa kwa Kamishna Mkuu wa *TRA*, sasa Serikali haioni haja ya kugatua madaraka na kuwapatia mamlaka mameneja wa mikoa ili waweze kutoa misamaha hiyo ya kodi ili kurahisisha kazi za ujenzi wa barabara ufanyike kwa haraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kumekuwa na malimbikizo ya madai ya *VAT* kwa wakandarasi, sasa Serikali haioni haja ya kuweka mchakato rahisi wa kuweza kuwalipa haraka wakandarasi hao ili waweze kutumia fedha zao ili kuijiendeleza kwenye miradi yao ya ujenzi wa barabara? Ahsante *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, ushauri wake Mbunge umepokelewa na unaenda kufanyiwa kazi hasa katika kipindi hiki cha ukusanyaji wa maoni, Serikali itaangalia na wataalamu wetu watatushauri, kama ipo tija ya kupeleka mikoani, basi Serikali itafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, madeni ya makimbikizo ya madai ya *VAT Refund*, yaliyo mengi tayari yameshahakikiwa na yamelipwa na yale ambayo yamewasilishwa siku za karibuni, yanahakikiwa na yakikamilika tu Serikali italipa *refund* hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Amandus.

Na. 388

**Kufufua Viwanda Nachingwea**

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafufua viwanda vya Mafuta Ilulu na kubangua korosho – Nachingwea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Serikali ilifanya zoezi la tathmini na ufuatiliaji kwa viwanda vyote vilivyobinafsishwa nchi nzima ikiwa ni pamoja na viwanda vya Mafuta Ilulu na kubangua korosho - Nachingwea. Tathimini hiyo imeisaidia Serikali kuweka mikakati ya kufufua viwanda hivyo, ikiwemo kuvirejesha Serikalini na kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Korosho cha Nachingwea kimepata mwekezaji ambaye ni kampuni ya *ANH & RAKA Ltd*. ambaye amesaini Mkataba wa Pango kwa maana ya *Lease Agreement* na mamlaka ya *EPZ* tarehe 11 Desemba, 2023 kwa ajili ya kuchakata mazao ya kilimo ikiwemo korosho, ufuta na karanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kiwanda cha Mafuta Ilulu kimepata mwekezaji kampuni ya *MCL Agro Co. Ltd*. ambaye amesaini Mkataba wa Pango yaani *Lease Agreement* na Mamlaka ya *EPZ* tarehe 28/3/2023 kwa ajili ya kuchakata mazao ya kilimo ya korosho, ufuta na karanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, wawekezaji hao wapo katika hatua mbalimbali za maandalizi ya kuanza uendelezaji. Aidha, kwa mujibu wa mikataba wawekezaji hao wanapaswa kuwa wameanza uzalishaji ndani ya miezi 24 kutoka tarehe ya kusaini mkataba, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amandus.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kwa kuwa viwanda hivi tayari vilipata wawekezaji ambao walishindwa kuendeleza kama mkataba ulivyodai, je, ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali kwa wawekezaji hawa ambao walishindwa kufanya kazi iliyokusudiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, zao la korosho ni zao la kibiashara na linatuingizia kama Taifa fedha nyingi za kigeni, kwa kufufua viwanda hivi vya kubangua korosho tutakuwa tunaongeza thamani ya zao lenyewe, lakini pia tutakuwa tunainua uchumi wa wakulima na kuongeza pato la Taifa. Ni mkakati gani wa Serikali kuhakikisha korosho haziuzwi zikiwa ghafi badala yake kufufua viwanda vingi vya kubangua korosho ili tuweze kuinua ubora wa zao hilo na kuongeza thamani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Chinguile kwa ufuatiliaji kuhusu uongezaji thamani wa mazao mbalimbali ikiwemo korosho katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hatua ambazo Serikali imechukua kwa swali lake la kwanza, ni kupitia kama nilivyosema na kufanya tathmini ya viwanda vyote ambavyo vilibinafsishwa na havifanyi kazi. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuvirejesha na ndiyo maana viwanda zaidi ya 20 vimesharejeshwa na vingine tunaendelea utaratibu kukamilisha urejeshwaji, zaidi ya viwanda 33 na hiyo ndiyo hatua ya kwanza kwamba wale ambao wameshindwa kuviendeleza viwanda hivi, vyote vitanyang'anywa ili tuweze kutafuta wawekezaji wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, katika hilo tunataka wale ambao sasa huenda walifanya hujuma kwenye viwanda vile

ambavyo walipewa vilikuwa labda na mitambo na vifaa mbalimbali vya mashine za viwanda hivyo ambavyo *either* wameng'oa au wamefanya hujuma yeyote, basi nao kulingana na mikataba ile nao watachukuliwa hatua mbalimbali za kisheria kulingana na mikataba ambayo tuliingia nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili, ni kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuhakikisha bidhaa, mazao ya kilimo yanaongezwa thamani ikiwemo korosho ambayo inaingizia Serikali fedha nyingi za kigeni. Lengo sasa ni kuhakikisha korosho inaanza kuuzwa ikiwa imebanguliwa badala ya kuwa ghafi na ndiyo maana tumeanza moja, kurejesha hivi viwanda na kuvifufua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Wizara kupitia taasisi zetu, tunaandaa mashine, teknolojia rahisi ya viwanda vidogo vidogo ambavyo vitawasaidia wakulima wadogo wadogo na wajasiriamali waweze kubangua katika ngazi ya chini ili tuhakikishe tunauza korosho ambayo imebanguliwa badala ya kuendelea kuuza korosho ghafi, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanyika, jiandae Mheshimiwa Suma.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, pale Njombe tuna kiwanda cha kuchakata maziwa ambacho kimefungwa kwa miaka saba na nimeuliza mara nyingi hapa ndani. Serikali inachukua hatua gani kuratibu ili kiwanda hiki kifunguliwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mwanyika, Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Viwanda na Biashara ya Bunge lako Tukufu kwa kufuatilia kuhusiana na maendeleo ya viwanda katika Mkoa wa Njombe mahususi kiwanda hiki cha maziwa ambacho kwa kweli amekuwa akifuatilia na tumeshafanya hatua mbalimbali, moja, ni kujadiliana na wenzetu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumekaa vikao na benki kwa maana ya wadau mahususi, Benki ya Kilimo - *TIDB* na tumeshakubaliana kwa hatua za awali kwamba kiwanda hiki tunawatafutia wawekezaji na mwekezaji ambaye atakuwa tayari ataweza kupewa mkopo ili kuhakikisha anakifufua lakini pia kuhakikisha na viwanda vingine vya namna hii vinafufuliwa katika Mkoa wa Njombe na maeneo mengine hapa nchini, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa na mimi swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Chai cha Chivanje kilichoko Wilayani Rungwe kimefungwa na mwekezaji. Wakulima wa Chai wa Wilaya ya Rungwe wanasumbuka sana mahali pa kupeleka hiyo chai.

Sasa je, ni lini Serikali itafungua kiwanda hicho ili wananchi na wakulima wa Wilaya ya Rungwe waendelee kupeleka chai kwenye kiwanda hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na namshukuru sana Mheshimiwa Suma Fyandomo ambaye kwa kweli pamoja na mambo mengine, amekuwa akifuatilia sana kuhusiana na viwanda vya chai ambavyo vimekuwa na changamoto si tu katika Mkoa wa Mbeya kule Rungwe, lakini na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza kufanya kazi ya kufuatilia viwanda vyote vya kuchakata chai hapa nchini ikiwemo kiwanda hiki ambacho amekisema Mheshimiwa Mbunge ili kuhakikisha, kwanza, wawekezaji hawa ambao kama wameshindwa, tuwatafute wawekezaji wengine, lakini pia kuhakikisha wakulima hawa ambao wamelima chai ambayo kwa kweli isipovunwa na kupelekwa kiwandani, inaharibika na ni hasara kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshaanza kufanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, tunataka kuona wawekezaji hawa ambao walikubali kuchukua viwanda hivi wanafanya kazi na kuviendeleza viwanda hivi kulingana na mikataba ambayo Serikali imeingia nao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pole nyingi kwa wananchi wa Hai kwa kuondokewa na Katibu wa Kata ya KIA.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kufufua Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools*, walituahidi eneo la Njiapanda Machame wataanzisha *centre* kwa ajili ya kusaidia kiwanda hiki na wananchi wanaotumia njia ya Machame, je, mchakato huu umefikia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na pia nampongeza Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kwa ufuatiliaji wa kuendeleza eneo hili ambalo lilikuwa ni eneo la *Kilimanjaro Machine Tools* kwa maana ya kuhakikisha wananchi wa pale wanafaidika na uwekezaji wa kiwanda hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faida ya Bunge lako, lakini pia kwa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na wananchi wa Hai kwamba tayari tuna mkandarasi ameshapewa kazi ya kufanya tathmini na kuanza michoro kwa ajili ya eneo hili la Njiapanda ambalo tumelenga ambayo ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba tuwe na mitaa ya biashara na mitaa ya viwanda ambapo hapa sasa kunakuwa na eneo hili kwa ajili ya biashara mbalimbali ikiwemo kama vituo vya mafuta na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kazi inafanyika na

mkandarasi yuko tayari kuandaa michoro ya eneo hili kwa ajili ya eneo la kibiashara katika Halmashauri hii ya Hai.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ulinzi. Mheshimiwa Cherehani kwa niaba Mheshimiwa Ngassa.

Na. 389

**Nafasi za Ajira na Mafunzo kwa Vijana**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA K.n.y. MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuongeza nafasi za ajira na mafunzo jeshini kwa vijana wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cherehani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania huandikisha askari wapya kwa mujibu wa sheria, kanuni na maelekezo yanayotolewa mara kwa mara. Utaratibu wa kuandikisha Jeshi askari wapya umefafanuliwa kwenye Kanuni ya 5 ya Kanuni ya Majeshi ya Ulinzi Juzuu ya Kwanza (Utawala). Aidha, Serikali imeondoa utaratibu wa kuandikisha ajira kwa vijana wanaohitimu elimu ya darasa la saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ongezeko la idadi ya ajira na mafunzo jeshini kwa vijana wanaohitimu kidato cha nne hutegemea bajeti inayotengwa kwa mwaka husika. Jeshi huandikisha askari wapya baada ya kupewa maelekezo na idadi

ya nafasi kulingana na uwezo wa bajeti. Nafasi hizo hugawanywa kulingana na mahitaji ya kitaaluma na ujuzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kumekuwa hakuna uwiano kati ya wanaoingia kwenye mafunzo na wale wanapata ajira kwenye vyombo vya ulinzi. Je, upi mkakati wa muda mfupi na wa muda mrefu wa Serikali kwa vijana wanaomaliza mafunzo ya JKT katika kuajiriwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wanapokuwa kwenye mafunzo pia kumekuwa na changamoto ya miundombinu; je, upi mkakati wa Serikali kukabiliana na tatizo la miundombinu kwa hawa vijana wetu wanaoingia kwenye mafunzo ya JKT? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwiano kama nilivyojibu kwenye swali la msingi inategemea sana nafasi za ajira zinazotolewa na Serikali. Hivyo, haiwezekani watoto waliojiunga na JKT 1,000 wakalingana na ajira ambayo inaweza ikatolewa kwa sababu tu uwezo wa Serikali ndiyo unaweza uka-*determine* tuchukue watu wangapi kwenda kwenye ajira za kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini miundombinu katika Vyombo hivi vya Ulinzi na Usalama, Serikali imekuwa ikiviangalia kwa jicho la pekee kabisa. Kwa hiyo, hakuna uhakika mkubwa sana juu ya ukosefu wa vitendeakazi na miundombinu ya kimafunzo kwenye maeneo ya makambi ya Jeshi. Namhakikishia tu kwamba Serikali imeweka miundombinu wezeshi kwa vijana wetu ili waweze kupata mafunzo kamilifu yanayoweza kwenda kuwasaidia wanapomaliza mafunzo yao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha, sasa ni muda wa wageni Bungeni.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wageni sita wa Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maliasili na Utalii kutoka Bunge la Namibia, Mheshimiwa Agnes Kafula – Mwenyekiti wa Msafara, Mheshimiwa Mike Venaani – Mjumbe, Mheshimiwa Annakletha Sikerete –Mjumbe, Mheshimiwa Natangue Ithete – Mjumbe, Ndugu Frankhilde Endjala – Katibu wa Kamati. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Spika, Maafisa wa Idara ya Utawala na Usafiri kutoka Bunge la Uganda wakiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala na Usafiri, Dkt. Medard Turyamureba akiongozana na wajumbe wake Bi. Caroline Among Abura, Bwana Peter Kasudha, Bi. Rebecca Katitwa na Bwana Moses Opio. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax - Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambao ni Ndugu Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe – Katibu Mkuu, Jenerali Jacob John Mkunda – Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Luteni Jenerali Salum Haji Othman – Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele – Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Amri Salim Mwami – Mkuu wa Tiba Jeshini, *Rear Admiral* Ameir Ramadhan Hassan – Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Wanamaji, Jeneral Iddi Said Nkambi – Mkuu wa Kamandi ya Vikosi Chini ya Makao Makuu ya Jeshi na Brigedia Jeneral Erick Mlelwa – Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Akiba. *(Makofi)*

Wapo pia Meja Jenerali Fadhili Omary Nondo – Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Meja Jenarali Shaban Baraghashi Mani – Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga, Meja Jenerali Hawa Issa Kodi – Mkuu wa Tawi la Uhandisi la Lojistiki, *Rear Admiral* Michael Mwanandanje Mumanga – Kamishna wa Tafiti na Maendeleo ya Jeshi, Meja Jenerali Marco Gaguti – Mkuu wa Utawala Jeshini na Brigedia Jenerali Geofrey Renatus Nyoni – Mdhibiti Mkuu Jeshini. *(Makofi)*

Wengine ni Kanali Alphonce Haule – Kaimu Mkuu wa Tawi la Mipango na Maendeleo, Brigedia Jenerali Seif Athuman Hamis –

Meneja Mkuu Shirika la Mzinga, Brigedia Jenerali Hassan Mabena – Mkuu wa Utawala JKT na Bwana Obedi Sayore – Kamishna wa Sera na Mipango. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Jenerali Mstaafu Robert Phillemon Mboma – Mkuu wa Majeshi wa Tano, Jenerali Mstaafu Venance Salvatory Mabeyo – Mkuu wa Majeshi wa Nane na Luteni Jenerali Mstaafu Abdulrahman Shimbo – Mnadhimu Mkuu wa Jeshi (2007 - 2017), ahsanteni. *(Makofi)*

Wapo pia Luteni Jenerali Mstaafu Samuel Ndomba – Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Mzinga, Luteni Jenerali Mstaafu Wynjones Kisamba – Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la *TATC* – Nyumbu na Meja Jenerali Mstaafu Farah Mohamedi – Mwenyekiti wa Bodi ya Suma JKT. *(Makofi)*

Wapo pia Mkuu wa Mkoa wa Kigoma - Mheshimiwa Thobias Andengenye na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji Mstaafu na Mheshimiwa Daniel Chongolo – Mkuu wa Mkoa wa Songwe, ahsanteni. *(Makofi)*

Wengine ni Kanali Evance Mtambi – Mkuu wa Mkoa wa Mara na Kanali Patrick Sawala – Mkuu wa Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wegine ni Bwana Philibert Mponzi – Mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu *NMB*, Ndugu Chabu Mishwaro – Mwakilishi wa Mtendaji Mkuu *CRDB* na Kanali Anthanasius Kamuhabwa – Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la *TATC* Nyumbu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni sita wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Waziri wa Madini ambao ni watumishi kutoka Kituo cha Afya cha Nkuhungu cha Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, mpiga kura wake anaishi Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Abubakari Asenga ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Kilombero Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph Kakunda, viongozi wa Shirikisho la Walimu Tanzania. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, waumini wenzake kutoka Kanisa Katoliki Kisasa, Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Aziza Sleyum ambaye mtoto wake kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni wengine nane wa Mheshimiwa Aziza Sleyum ambao ni wajasiriamali wa kuuza asali kutoka Mkoa wa Tabora ambao wapo kwenye Maonesho Ukumbi wa Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 100 na walimu kumi wa Shule ya Msingi Nyamuge kutoka Ilemela Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 71 kutoka Kanisa la Moravian Ushirika wa *Iringa Road* Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wanafunzi 53 kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Mkoa wa Kilimajaro. *(Makofi)*

Wageni wengine waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 50 na walimu wawili kutoka Shule ya Msingi Kaloleni ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo tarehe 20 Mei, kutakuwa na semina kuhusu majukumu ya Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* pamoja na Wakala wa Usajili wa Biashara za Leseni *(BRELA)* itakayotolewa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Semina hii itafanyika mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia sasa kwenye bajeti ya Wizara ya Ulinzi. Mheshimiwa Waziri, karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliyochambua bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Fungu 57 – Wizara, Fungu 38 – Ngome na Fungu 39 – JKT na kupitisha Mpango wa Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana wakati nchi ikiwa katika hali ya amani na usalama, nchi iko imara na iko shwari.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa unyenyekevu namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuniamini na kuniteua kwa mara ya pili kuongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, hii ni heshima kubwa na dhamana

kubwa na ninaahidi kutekeleza majukumu yangu kwa weledi na kwa uaminifu. *(Makofi)*

Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kuamini viongozi wenzangu Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe - Katibu Mkuu, Jenerali Jacob John Mkunda - Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Luteni Jenerali Salum Haji Othman - Mnadhimu Mkuu wa Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa jitihada zake za dhati na kazi kubwa katika kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa na amani, utulivu na mshikamano. Katika miaka mitatu ya uongozi wake tumeshuhudia mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na katika kuimarisha ulinzi na amani, kupitia falsafa yake ya 'R' nne upatanisho, ustahimilivu, maboresho na ujenzi wa Taifa upya, Mheshimiwa Rais ameendeleza kwa vitendo, maono ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyehimiza umoja miongoni mwa wa Tanzania ili kudumisha amani na kujenga Taifa imara lenye misingi imara ya usawa, haki mshikamano na maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao makini na kwa miongozo wanayonipatia katika kutekeleza majumuku ya Wizara ninayoongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na ninawapongeza pia Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson Mwansansu, Mbunge, kwa kuliongoza Bunge hili kwa weledi na kwa viwango vya hali ya juu. *(Makofi)*

Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, Rais wa 31 wa Mabunge ya Duniani *(IPU)* na mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo kutoka Barani Afrika. Aliongoza kampeni hii yeye mwenyewe kwa umahiri mkubwa na hatimaye kuchaguliwa kwa kishindo, hongera sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwapongeze Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa mafanikio. Nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge kwa kuaminiwa na Bunge lako Tukufu na kuteuliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwako na Bunge lako Tukufu na Taifa kwa kuondokewa na viongozi wakuu wa nchi yetu, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne Hayati Edward Ngoyai Lowassa. Pia natoa pole kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Mbarali Marehemu Francis Leonard Mtega na aliyekuwa Mbunge wa Kwahani Marehemu Ahmed Yahya Abdulwakil, napenda kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na viongozi na wapendwa hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Amiri Jeshi Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, familia na ndugu kufuatia vifo vya wanajeshi waliopoteza maisha wakati wakipigania amani na katika shughuli za uokoaji na Mungu azilaze pema peponi roho zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natoa pole kwa waliopata maafa ya maporomoko ya matope Wilayani Hanang, Mkoa wa Manyara na Kata ya Itezi, Mkoani Mbeya yaliyopelekea kuondokewa na wapendwa wao, uharibifu na upotevu wa mali. Pia nitumie fursa hii kutoa pole kwa watanzania wote waliopata maafa ya mafuriko sehemu mbalimbali nchini.

Aidha, nitoe shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuhakikisha kwamba Watanzania hawa wanapata huduma stahiki na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukurani pia timu ya kukabiliana na maafa chini ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu na uratibu wa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi hiki. Namshukuru pia Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Jacob John Mkunda na timu yake kwa kuhakikisha kuwa maeneo haya yanafikiwa kadri ilivyohitajika kwa wakati na kwa uokozi wa shughuli za na kufikisha mahitaji yaliyohitajika kwa haraka. Tunapongeza sana wote walioshiriki na kusimamia shughuli za uokozi ikiwa ni pamoja na maafisa, maaskari, marubani na wasaidizi wao na wale wote walioshiriki katika shughuli hizi mahususi kwa njia mbalimbali, tunawashukuru kwa kufanya kazi bila kuchoka na kwa uzalendo wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa maoni na ushauri wanaoendelea kutupatia ikiwa ni pamoja na katika maandalizi ya bajeti hii. Maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati wakati wakichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na mapendekezo katika mpango wa bajeti wa mwaka 2024/2025 yameisaidia kuboresha mapendekezo ya makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 ninayowasilisha asubuhi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi; katika mwaka wa fedha 2023/2024 hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu yenye urefu wa jumla ya kilometa 5923.41 inayohusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji imeendelea kuwa shwari. Mipaka hiyo kwa upande wa Magharibi Tanzania inapakana na nchi za Burundi, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo na Rwanda; upande wa Mashariki kuna Bahari ya Hindi na tunapakana na nchi za Comoro na Shelisheli; upande wa Kusini tunapakana na Malawi, Msumbiji na Zambia na upande wa Kaskazini tunapakana na nchi ya Kenya na Uganda. Katika kipindi husika hakukuwa na matukio ya kutishia amani baina ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo isipokuwa changamoto kadhaa za kiulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za kiulinzi na usalama zilizojitokeza katika baadhi ya mipaka yetu hususan wa Kusini na Magharibi ni pamoja na uwepo wa vikundi vya kigaidi vyenye silaha katika nchi jirani. Tanzania kwa kushirikiana na nchi jirani imeendelea kukabiliana na changamoto hizo, maelezo ya kina kuhusu hali katika kila mpaka yapo katika aya ya 12 mpaka aya ya 21 ukurasa wa sita mpaka wa 10 wa hotuba ninayoiwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; wakati Wizara ikiwasilisha hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 hapo tarehe 24 Mei, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipitia na kujadili utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha huo na kutoa maoni, ushauri na maelekezo yaliyolenga kuboresha utendaji. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamezingatiwa ikiwa ni pamoja na kujumuishwa katika mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2024/2025 ninayoiwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi; katika kutekeleza mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imeendelea kuzingatia maelekezo yaliyoainishwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi wa mwaka 2020 Sura ya 5 Ibara ya 105 kama inavyoonekana

katika maeneo mbalimbali ya hotuba hii na pia katika mpango wa bajeti wa mwaka 2024/2025. Maelezo ya Ilani ya CCM yaliyoainishwa katika Sura ya 5 Ibara ya 105 yanaonekana katika aya ya 23(a) mpaka (k) ya hotuba ninayoiwasilisha ukurasa wa 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa fedha 2023/2024; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilikadiriwa kukusanya makadirio ya jumla ya shilingi 87,603,000 kutoka katika mafungu yake matatu; Fungu 38 – NGOME shilingi 22,000,000, Fungu 39 – JKT shilingi 64,403,000 na Fungu 57 – Wizara shilingi 1,200,000. Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2024 Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli ya shilingi 79,352,295.48 ikiwa ni sawa na 90.58% ya makadirio. Mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu unaonekana kwenye Jedwali Na. 1 ukurusa wa 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,989,967,122,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika mafungu yake matatu Fungu 38 – NGOME, Fungu 39 – JKT na Fungu 37 – Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi 2,273,738,750,000 ni kwa ajili ya matumizi wa kawaida na shilingi 48,867,636,000 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 38 – NGOME liliidhinishiwa shilingi 2,273,738,750,000 kwa matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo shilingi 48,867,636,000; Fungu 39 – JKT lilihidhinishiwa shilingi 468,397,562,000 kwa matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo shilingi 13,965,535,000 na Fungu 57 – Wizara shilingi 24,997,639,000 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 160,000,000,000 kwa matumizi ya maendeleo. Muhtasari na mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeainishwa katika Jedwali Na. 2 lililopo ukurasa wa 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2024 fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni shilingi 2,389,381,299,149.56 ikiwa ni sawa na 79.9% au 80% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi

2,277,685,836,213.70 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 111,695,462,935.86 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kiasi hicho Fungu 38 – NGOME limepokea shilingi 1,877,499,711,248.87 kwa matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo shilingi 12,345,336,244; Fungu 39 – JKT limepokea shilingi 979,838,502,509.60 kwa matumizi ya kawaida na kwa shughuli za maendeleo ni shilingi 10,643,690,000. Fungu 57 – Wizara limepokea shilingi 20,347,622,455.23 kwa matumizi ya kawaida na kwa shughuli za maendeleo shilingi 88,706,436,691.87. Muhtasari wa mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu yote umeainishwa katika Jedwali Na. 3 lililopo katika ukurasa wa 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara imepokea fedha ya nyongeza zenye jumla ya shilingi 1,648,083,492,153.66 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mahususi ikiwa ni pamoja na kugharamia mikataba mbalimbali, kugharamia vikundi vya maafisa na askari katika *operation* mbalimbali ikiwemo Misheni ya Jumuiya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya Kupambana na Ugaidi nchini Msumbuji na Misheni ya Kuleta Amani Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo *(DRC)* inayojulikana *SAMIDRC* na katika misheni zote hizi Tanzania tunashiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2023/2024 zimetumika kugharamia shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na malipo ya stahiki za maafisa na maaskari, watumishi wa umma, matunzo ya zana na vifaa, mafunzo ya kijeshi na mazoezi, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, mpango mkakati wa kilimo na mifugo, mafunzo ya Jeshi la Akiba, utatuzi wa migogoro ya ardhi, huduma za afya na bima, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi kitaifa, kimataifa na kikanda na baina ya nchi na nchi, ushirikiano na mamlaka ya za kiraia katika shughuli mbalimbali na ushiriki katika michezo ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya kijeshi na mazoezi; katika mwaka wa fedha 2023 Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali na kozi za kijeshi ndani na nje ya nchi na kuwaendeleza wanajeshi

katika taaluma mbalimbali za uongozi. Mafunzo hayo yameongeza weredi katika utendaji na morali. Aidha, katika kipindi husika Jeshi la Ulinzi la Wananchi lilifanya mazoezi mbalimbali ya kijeshi ikiwemo ndani ya nchi, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo na matunzo ya zana na mitambo; Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kufanya matengenezo, maboresho na matunzo ya zana na vifaa mbalimbali. Vilevile ukarabati wa mitambo na mashine umefanyika katika Mashirika ya Mzinga na *Tanzania Automative Technology Center* linalojulikana zaidi kama NYUMBU.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa; Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakavu, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa na stadi za kazi kwa vijana wa kundi la mujibu la sheria na kwa vijana wa kundi la kujitolea. Vijana wa kundi la mujibu wa sheria waliopata mafunzo wameongezeka katika mwaka huu wa fedha kutoka 26,000 mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia 52,119 kwa wa fedha 2023/2024 ikiwa ni ongezeko la 100%. Kati ya hao wavulana ni 31,256 na wasichana 20,863. Aidha, vijana 12,000 wa kujitolea wanaendelea kupatiwa mafunzo katika kambi mbalimbali za JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu pamoja na umma wa Tanzania kwamba dhumuni la mafunzo yanayotolewa kwa vijana ni kuwajengea uzalendo, ukakavu, umoja wa kitaifa na kuwapatia stadi za kazi na stadi za maisha ili wakimaliza haya na kulitumikia Jeshi la Kujenga Taifa waweze kurejea katika jamii wakiwa raia wema na wenye uwezo wa kujitegemea na kulilinda Taifa lao. Nitoe rai kwa vijana wote wanaopata fursa ya kupata mafunzo haya kuwa raia wema na kuzitumia stadi walizozipata kuajiri na kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, yamekuwepo maombi ya kuona jinsi ya kuwasaidia vijana wanaomaliza JKT kujiajiri, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kupitia Bunge hili, kuwa ombi hili linafanyiwa

kazi ikiwa ni pamoja na kuwa ithibati ya mafunzo ya stadi wanazozipata kwa hiyo, wakimaliza watakuwa na vyeti ambavyo vimepata hiyo ithibati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuzungumza na benki, tayari tunazungumza na benki ili kuwe na utaratibu mahususi wa kupata mikopo nafuu na yenye utaratibu mahususi na kuwapatia fursa zilizopo katika sekta mbalimbali kama vile kilimo na uvuvi ambapo sasa hivi wanapatia fursa kupitia programu za *Building Better Tomorrow,* lakini pia kwa ukubwa wa suala hili na maombi mbalimbali tuliyoyapata kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla, Wizara imeunda timu ambayo inaliangalia suala hili kwa mapana yake, ili tuweze kujua tunakwenda nalo namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya Jeshi la Akiba; Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Akiba ambayo hufanyika katika mikoa yote ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 jumla ya wananchi walioandikishwa na kuhitimu mafunzo hayo ni 15,840 ambapo kati ya hao wanaume ni 13,633 na wanawake ni 2,207. Vilevile Ofisi za Washauri wa Jeshi la Akiba katika mikoa na wilaya zimeendelea kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi. Jeshi la Akiba ni muhimu sana katika kudumisha ulinzi, lakini pia katika kuendeleza dhana ya kuwa ulinzi ni jukumu la wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi; imekuwepo migogoro ya ardhi baina ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na wananchi. Kupitia mpango wa miaka mitatu wa kutatua migogoro ya ardhi wa mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 Wizara imeendelea kutatua migogoro hiyo ambapo mpaka sasa migogoro 78 sawa na 89.7% ya migogoro iliyotambuliwa imetatuliwa kwa njia ya mazungumzo na kuhuisha mipaka, kupima, kufanya tathmini na kulipa fidia kwa wananchi wanaostahili. Mpango huu niliourejea unajumuisha pande zote mbili za Muungano. Ipo migogoro baina ya wananchi na Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania kutoka upande wa Tanzania, Zanzibar pia inahusisha migogoro kutoka upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyolipwa na kulipwa fidia tangu mpango huu umeanza ni maeneo 31 kama yanavyoonekana katika Kiambatanisho Namba 2 na maeneo yaliyokwisha kufanyiwa uhakiki na yanasubiri kulipiwa fidia ni 33 kama yanavyoonekana katika Kiambatanisho Namba 1 na maeneo ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi ni maeneo tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia Bunge lako Tukufu kusisitiza kuwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni kwa ajili ya shughuli mahususi kwa maslahi mapana ya Taifa letu hususan ulinzi wa Taifa letu. Hivyo, kupitia Bunge lako Tukufu niwaombe viongozi na wananchi wote kutoa ushirikiano kwa kuyalinda, kutoyavamia na kupelekea migogoro isiyo ya lazima. Aidha, migogoro inapojitokeza itatuliwe kwa mashauriano na kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa na siyo kisiasa. Jeshi siyo sehemu ya siasa ni taasisi mahsusi kwa kazi mahsusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tusishawishike sisi kama viongozi, lakini pia wananchi kuchukua hatua zitakazoleta taharuki, chuki, vurugu kati ya wananchi na Jeshi letu. Migogoro yote ilioletwa Wizarani imefanyiwa kazi kwa weledi, maridhiano na kwa wakati. Waheshimiwa Wabunge wote walioleta migogoro yao katika maeneo yao mbalimbali tumezungumza, tumechukua hatua ikiwa ni pamoja na kutuma timu za wataalamu wa ndani na wakati mwingine mimi mwenyewe nimekwenda katika maeneo husika. Migogoro hiyo imetatuliwa kwa mwafaka, kwa kuzingatia uhalisia, maslahi ya pande zote mbili yaani upande wa Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania na wananchi. Aidha, kuvamia maeneo ya jeshi ni kuhatarisha maisha kwani maeneo hayo hutumiwa kwa shughuli mbalimbali ikiwemo pia mazoezi ambayo hutumia silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano wa kiulinzi, kijeshi na nchi nyingine; Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kushirikiana na nchi rafiki katika masuala ya kiulinzi, usalama katika maeneo mbalimbali ikiwemo mafunzo, misaada ya kitaalamu, zana na vifaa. Vilevile kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Tanzania imeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo

Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mafunzo, ubadilishanaji wataalamu na operesheni mbalimbali, yaliyofanyika katika mwaka wa fedha 2023/2024 na yanayoendelea kufanyika yanaonekana katika aya ya 40 ya hotuba hii ambayo ni ukurasa wa 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushiriki wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika shughuli za ulinzi wa amani; katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Serikali kupitia Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa katika operesheni za ulinzi wa amani ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Lebanon chini ya Misheni za Umoja wa Mataifa. Vilevile Serikali kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linashiriki katika Misheni ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya kupambana na ugaidi wa vikundi vya wahalifu nchini Msumbiji na Misheni ya *SADC* ya kuleta amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kama nilivyokwishaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano na mamlaka za kiraia katika shughuli mbalimbali; Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika shughuli mbalimbali zikiwemo kutoa misaada wakati wa majanga na maafa, kushiriki katika utekelezaji na ulinzi wa miradi ya kimkakati. Maelezo ya kina ni kama yanavyoonekana katika aya ya 44 ukurasa wa 27 na 28 wa hotuba ninayowasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema; "Jambo lililokubwa zaidi ni kwamba wanajeshi wetu sasa ni sehemu ya jamii yetu. Mchango na uaminifu wao umedhihirika mara nyingi toka Jeshi lilipoundwa hapo mwaka 1964."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu niwapongeze wanajeshi wetu kwa uhodari, uzalendo na kazi kubwa wanayoifanya na niwatie moyo waendelee kuwa sehemu ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utunzaji wa mazingira; Wizara kupitia taasisi zake imeendelea na utunzaji wa mazingira

kwa kulinda maeneo yake yenye miti ya asili yasivamiwe kwa shughuli za kijamii, kuendelea kupanda miti mipya. Katika kipindi husika Wizara na taasisi zake imepanda miti ipatayo 989,106. Vilevile Wizara imeendelea na utunzaji wa fukwe katika Mkoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi. Aidha, maeneo yote ya jeshi yana zuio la ukataji miti, kuchoma mkaa na kuchunga mifugo. Napenda nitoe wito kwa wananchi wote kuzingatia zuio la ukataji miti, kuchoma mkaa na kuchunga mifugo katika maeneo ya jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kutimiza azma ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhusu utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi kwa taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100, Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania na makambi yote yamefikia 90% ya matumizi ya nishati safi ya kupikia. Jeshi la Kujenga Taifa limefikia 98%, Shirika la Mzinga limefikia 98%, Shirika la Nyumbu limefikia 95% na lengo ni kufikia 100% kufika mwishoni mwa mwaka huu wa fedha. Maelezo ya kina kuhusu shughuli zote nilizozitaja ambazo zimetumia fedha za matumizi ya kawaida katika aya ya 30 mpaka ya 54 ukurasa wa 18 mpaka 33 wa hotuba ninayowasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya fedha za maendeleo; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imeweza kutumia fedha za maendeleo kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Ununuzi wa zana na vifaa;

(ii) Uhuishaji na uboreshaji wa zana za Kijeshi;

(iii) Kugharamia mikataba na matengenezo na matunzo ya zana;

(iv) Ujenzi wa maghala ya kuhifadhia zana na vifaa katika mikoa mbalimbali;

(v) Ujenzi wa mahanga ya maafisa na askari;

(vi) Ujenzi wa Hospitali Kuu Kanda ya Jeshi Msalato Dodoma kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani;

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga hospitali kubwa sana ambayo tuna imani pia itakuwa mkombozi wa matatizo ya kiafya katika Mkoa wa Dodoma, kwani Hospitali za Jeshi hazitumiwi na wanajeshi tu, hutumiwa pia na raia. *(Makofi)*

(vii) Ujenzi wa miundominu ya majengo katika Hospitali ya Jeshi ya Kanda, Mwanza na vituo vya afya vikosini;

(viii) Ujenzi wa Jengo la Ramani;

(ix) Kulipa fidia kwa wananchi katika vijiji vya Manispaa ya Moshi, Kibaoni, Makole, Lukungwi na Kihangaiko katika Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze;

(x) Ununuzi wa magari kwa ajili ya matumizi ya jeshi;

(xi) Ujenzi wa miundombinu ya *scheme* za umwagiliaji katika Kikosi cha Chita JKT, kilichopo Mkoani Morogoro;

(xii) Ujenzi wa mahanga ya vijana katika Vikosi vya JKT na kufanya tathmini na ufutiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia JKT imefanikiwa pia kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia rasilimali za ndani kama inavyoonekana katika aya ya 59 ya hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mashirika yaliyo chini ya Wizara; nikianza na Shirika la *Tanzania Automotive Technology Center* (NYUMBU) katika mwaka wa fedha wa 2023 shirika limeendelea kutekeleza mpango wa maendeleo wa miaka kumi wa 2021/2022 hadi 2031/2032 wa kuliimarisha Shirika la NYUMBU. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa jengo la karakana kuu ya kukaribu chuma, kuwaendeleza kitaalamu wataalamu katika fani mbalimbali, kuendeleza utafiti wa kuzalisha sampuli kifani wa gari la Deraya na gari la NYUMBU, kufanya ukarabati wa miundombinu ya miliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi husika Shirika la NYUMBU pamoja na majukumu mengine ya msingi limeweza

kutekeleza shughuli nyingine kwa kuitumia rasilimali za ndani kama inavyoonekana katika aya ya 59 ukurasa wa 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Mzinga; katika mwaka wa fedha 2023 Shirika la Mzinga limeendeleza majukumu ya msingi ikiwa ni pamoja na kuendelea kuzalisha mazao ya msingi kwa matumizi ya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania na vyombo vingine vya usalama, kuendelea kufanya ukarabati wa zana na vifaa vya kijeshi, kuendelea kufanya tafiti za kijeshi na kiraia hususan utafiti wa bomu la kufukuza tembo kweye makazi ya watu yaliyokaribu wa hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bomu hili lilizinduliwa tarehe 13 Mei, 2022 na limeanza kutumika. Nitoe shukrani kwa Kamati zote mbili, Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Utalii na Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje pia pamoja na Mheshimiwa *Chief Whip* kwa kuweza kushiriki katika uzinduzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna imani kwamba bomu hili litakuwa mkombozi katika changamoto hii ambayo imekuwepo kwa muda mrefu sana. Bomu hili ni toleo la pili. Lilikuwepo toleo la kwanza ambalo tuliona limeanza kuzoeleka na tembo hawa. Kwa hiyo, toleo hili la pili tuna imani sasa litaweza kuwafukuza tembo hawa na kupunguza madhara yaliyokuwa yakijitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza sana Shirika la Mzinga kwa kufikia hatua hii na pia kwa kushirikiana na *TAWIRI* na kuchangia katika jitihada za Serikali za kukabiliana na tembo ambao wameleta adha kubwa katika maeneo mbalimbali. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza shughuli zake mbalimbali kwa kutumia rasilimali za ndani, namaanisha Shirika la Mzinga kama inavyoonekana katika aya ya 62 ukurasa wa 41.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kutoa umuhimu mzito na mkubwa kwa shughuli za ulinzi ikiwa ni pamoja na kutoa pesa kwa shughuli mahsusi na operesheni maalumu kadiri ilivyojitokeza na kuhitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu amethibitisha kuwa yeye ni mlinzi namba moja wa Taifa letu kwa vitendo na kwa maono mapana na kutowaacha nyuma wafuasi wake. Nafikiri wote tuliaona wakati wa maadhimisho ya miaka 60 alidhihirisha kwamba yeye ni Amiri Jeshi Mkuu. Mvua ilikuwa inanyesha, watu walipata wasiwasi atakagua gwaride, alikwenda kukagua gwaride na kweli alionesha mfano kwa wafuasi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango na mwelekezo wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara inatarjia kukusanya jumla ya maduhuli ya shilingi 87,600,003 kutoka katika mafungu yake matatu; NGOME shilingi 22,000,000, JKT shilingi 67,400,004 na Wizara shilingi 1,200,000. Mchanganuo unaonekana katika Jedwali Namba 4.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo kwa Wizara ikiwa ni jumla ya shilingi 3,326,230,414,000 ambapo katika fedha hizo shilingi 3,008,812,900,007 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 317,417,512,000 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Fungu la 38 - NGOME linatarajiwa kutengewa fedha za matumizi ya kawaida shilingi 2,491,439,934,000 kwa shughuli za maendeleo na shilingi 48, 887,636,000; Fungu 36 - JKT linatarajiwa kutengewa shilingi 490,652,279,000 kwa matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo shilingi 8,549,876,000 na Fungu 57 – Wizara linatarajiwa kutengewa shilingi 26,720,694,000 kwa matumizi ya kawiada na shughuli za maendeleo shilingi 260,000,000,000. Mchanganuo umeainishwa katika Jedwali Namba 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 ni kuendelea kuliimarisha jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa, mafunzo na mazoezi pamoja na rasilimali watu, kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji mzuri wa jeshi, kuimarisha miundombinu mbalimbali katika maeneo ya jeshi, kuimarisha mashirika na taasisi katika sekta ya ulinzi, kuendelea kushiriki katika ujenzi na ulinzi wa miradi wa kimkakati kwa maslahi mapana ya taifa, kuendelea kuimarisha uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa liweze kuchukua

vijana wengi zaidi, kufanya tathmini na kuandaa mpango mkakati kwa lengo la kuweza kuchukua vijana wote wanaostahili kupata mafunzo ya JKT na kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya za Kiakanda na nchi mbalimbali katika nyanja za kijeshi na kiulinzi na hivyo kuimarisha diplomasia ya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shukrani; kabla sijahitimisha hotuba yangu napenda kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wenzangu katika Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia, kazi kubwa wanayoifanya na michango yao madhubuti katika kutekeleza mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na katika kutayarisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe, Katibu Mkuu; Jenerali Jacob John Mkunda, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi; Luteni Jenerali Salum Haji Othman, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi; Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa; Wakuu wa Kamandi zote, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara za Vitengo, Wakuu wa Matawi, Wakuu wa Vyuo, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma wote. Ahsanteni sana kwa ushirikiano mkubwa mnaonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia Bunge lako Tukufu kutoa shukrani kwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Jacob Mkunda; Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Salum Haji Othman, Makamanda, Maafisa na Maaskari wote kwa weledi, uzalendo na kazi kubwa anayoifanya kuhakikishwa kwamba Taifa letu lina amani na ni imara, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuhakikisha kuwa Wizara, Jeshi na taasisi zake zinaweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Wizara itaendelea kutekeleza majukumu ili kutekeleza maono ya Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu ikiwa ni pamoja na kuliimarisha jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa Saba wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Makamanda Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye alikuwa mgeni rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu alisema na naomba kunukuu; "Yapo maendeleo makubwa katika sayansi na teknolojia yanayoendelea na yanayopelekea changamoto mpya za kiulizni na kusalama. Hivyo, hamna budi kuwa tayari kukabiliana na changamoto hizo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo haya yanaonesha dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kuhakikisha kuwa jeshi letu ni imara wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara na taasisi zake zinatekeleza maagizo haya umakini unaotakiwa na kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kutoa shukrani kwa Taasisi za Kimataifa na Kikanda, na Serikali za nchi mbalimbali kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia ikiwa ni pamoja na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, Afrika Kusini, Algeria, Bangladesh, Burundi, Canada, DRC, Ethiopia, Finland, Ghana, Hispania, Indonesia, India, Israel, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Czech, Jordan, Kenya, Malawi, Marekani, Misri, Msumbiji, Morocco, Nigeria, Oman, Pakistan, Rwanda, Serbia, Sweden, Ufaransa, Ujerumani, Uturuki, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi, Uswisi, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukushukuru tena wewe binafsi, Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa ushirikiano na ninapenda pia kuishukuru familia yangu kwa kunitia moyo na upendo wao kwangu unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wao katika ulinzi wa nchi yetu. Ni

matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Taifa letu na ninapenda nitoe rai kwa Watanzania wote waendelee kuwa walinzi wa Taifa lao, kwani jukumu la ulinzi na usalama ni la kila Mtanzania kama alivyohimiza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, wakati akihutubia Taifa kuelekea miaka 50 ya Muungano, *sorry* miaka 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka 60 ya Muungano hapo 25 Aprili, 2024 aliposema kuwa; "Hapa nataka kukumbusha kwamba mlinzi wa kwanza wa usalama wa nchi ni mwananchi mwenyewe. Kila mmoja wetu ana macho na ashirikiane na vyombo vya ulinzi na usalama kubaini, kuzuia na kukabiliana na matishio kwa usalama wa jamii zetu na nchi kwa ujumla." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe kiasi cha shilingi 3,326,230,419,000 katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kati ya fedha hizo shilingi 3,008,812,907,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 317,417,512,000 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Mchanganuo umeainishwa katika aya ya 68 ya Jedwali Na. 5 na kama ambavyo nimekwisha uwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa hoja ninaomba hotuba nzima kama ilivyowasilishwa iweze kuingia katika *Hansard* na hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambayo ni *www.modans.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA BAJETI YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 kwa Fungu 57 - Wizara, Fungu 38 - NGOME, na Fungu 39 - JKT na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana wakati Nchi yetu ikiwa katika hali ya amani na usalama. Aidha, kwa unyenyekevu namshukuru kwa dhati **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuniamini na kuniteua kwa mara ya pili kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hii ni heshima na dhamana kubwa, na ninaahidi kutekeleza majukumu yangu kwa weledi na uaminifu. Aidha, napenda kumshukuru **Mhe**. Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kuwaamini viongozi wenzangu **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe;** Katibu Mkuu; **Jenerali Jacob John Mkunda,** Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi; na **Luteni Jenerali Salum Haji Othman,** Mnadhimu Mkuu wa Jeshi.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, nampongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa jitihada zake za dhati, na kazi kubwa katika kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa na amani, utulivu na mshikamano katika miaka mitatu ya uongozi wake tumeshuhudia mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha ulinzi na amani. Kupitia falsafa yake ya 4R (upatanisho, ustahimilivu, maboresho na ujenzi wa Taifa upya), **Mhe.** Rais ameendeleza kwa vitendo maono ya Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere aliyehimiza umoja miongoni mwa watanzania ili kudumisha amani na kujenga Taifa imara lenye misingi imara ya usawa, haki, mshikamano, na maendeleo**.**

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru **Mhe.**

**Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na **Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.)**, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao makini, na kwa miongozo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ninayoiongoza.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi **Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.)** kwa kuliongoza Bunge kwa weledi na viwango vya hali ya juu. Nakupongeza pia kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), na mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo kutoka Barani Afrika. Uliongoza kampeni wewe mwenyewe, na hatimaye kuchaguliwa kwa kishindo, hongera sana! Vilevile, nampongeza **Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.),** Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa mafanikio. Nimpongeze **Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.)** na **Mhe. Deodatus Philip Mwanyika (Mb.)** kwa kuaminiwa na Bunge lako Tukufu na kuteuliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge.

6. ***Mheshimiwa Spika***, pia nawashukuru Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.)** kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, **Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb.)** kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, **Mhe. Jerry William Silaa (Mb.)** kuteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, **Mhe. Anthony Peter Mavunde (Mb.)** kuteuliwa kuwa Waziri wa Madini, **Mhe. Mhe. Deogratius John Ndejembi (Mb.)** kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), **Mhe. Alexander Pastory Mnyeti (Mb.), Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb.), Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb.), Mhe. Dustan Luka Kitandula (Mb.), Mhe. Zainab Athuman Katimba (Mb.),** na **Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb.)** kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri.

Niwahakikishie kuwa Wizara ninayoiongoza itatoa ushirikiano kwao katika kutekeleza majukumu na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwako, Bunge lako Tukufu na Taifa kwa kuondokewa na Viongozi Wakuu wa Nchi yetu; aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Hayati Ali Hassan Mwinyi**, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne, **Hayati Edward Ngoyai Lowassa.** Pia, natoa pole kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Mbarali **Marehemu Francis Leonard Mtega,** na aliyekuwa Mbunge wa Kwahani **Marehemu Ahmed Yahya Abdulwakil.** Napenda kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na viongozi hawa.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Amiri Jeshi Mkuu na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, familia na ndugu kufuatia vifo vya wanajeshi waliopoteza maisha wakati wakipigania amani, na katika shughuli za uokoaji. Mungu azilaze peponi roho zao.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, natoa pole kwa waliopata maafa ya maporomoko ya matope Wilaya ya Hanang' Mkoa wa Manyara na Kata ya Itezi Mkoa wa Mbeya yaliyopelekea kuondokewa na wapendwa wao, uharibifu na upotevu wa mali. Pia, nitumie fursa hii kutoa pole kwa watanzania wote waliopata maafa ya mafuriko sehemu mbalimbali nchini, ikiwemo Wilaya ya Rufiji Mkoa wa Pwani, Kihonda Wilaya ya Morogoro na Ifakara Wilaya ya Kilombero Mkoa wa Morogoro, Kisongo na Engosengiu Mkoa wa Arusha. Aidha, nitoe shukrani za dhati kwa Mhe. Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuhakikisha Watanzania hawa wanapata huduma stahiki kwa wakati. Aidha, nitoe shukrani pia kwa timu ya kukabiliana na maafa chini ya **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.),** Waziri Mkuu, na uratibu wa **Mhe. Jenista Joakim Mhagama (Mb.)**, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa. Namshukuru pia Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi **Jenerali Jacob John Mkunda** na Timu yake kwa kuhakikisha

maeneo hayo yanafikiwa kadri ilivyohitajika wakati wa uokozi na shughuli za kufikisha mahitaji yaliyohitajika kwa haraka. Tunapongeza sana wote walioshiriki na kusimamia shughuli za uokozi, marubani na wasaidizi wao, na wote walioshiriki katika shughuli hizi mahususi, tunawashukuru kwa kufanyakazi bila kuchoka na kwa uzalendo wa hali ya juu.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia nafasi hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na **Mhe. Vita Rashid Kawawa (Mb.),** akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti **Mhe. Vincent Paul Mbogo (Mb.)**, pamoja na wajumbe wa Kamati kwa maoni na ushauri wanaoendelea kutupatia, ikiwa ni pamoja na maandalizi ya Bajeti hii. Maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati wakati wakichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, na mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, yamesaidia kuboresha mapendekezo ya makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, ninayoiwasilisha leo hapa Bungeni.

## B. HALI YA ULINZI NA USALAMA WA MIPAKA YA NCHI

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, hali ya mipaka ya Nchi yetu yenye urefu wa jumla ya kilomita **5,923.41,** ambayo inahusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji, imeendelea kuwa shwari. Mipaka hiyo ni baina ya Tanzania na Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Uganda na Zambia. Kwa upande wa eneo la maji, hususan Bahari ya Hindi, inapakana na nchi za Komoro na Shelisheli. Katika kipindi husika hapakuwa na matukio ya uhasama yaliyoripotiwa baina yetu na nchi tunazopakana nazo, mbali na kuwepo changamoto kadhaa za ulinzi na usalama.

### Mpaka wa Tanzania na Burundi

12. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu wenye urefu wa kilomita **468.85** ni shwari. Hakuna matukio yoyote yaliyoripotiwa kuhatarisha usalama baina ya

nchi hizi, ingawa eneo hili linakabiliwa na uwepo wa wahamiaji haramu, uvamizi wa wakulima na uingizaji wa mifugo kwa ajili ya kupata malisho. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama imeendelea kukabiliana na hali hii.

**Mpaka wa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo**

13. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu wenye urefu wa kilomita **554** ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama kwa nchi yetu. Hata hivyo, ndani ya Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo yameripotiwa matukio ya waasi kushambulia miji mbalimbali nchini humo. Wizara kupitia JWTZ imeendelea kuwa macho na kujipanga wakati wote. Aidha, ushiriki wa Tanzania kupitia Misheni ya Umoja wa Mataifa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*United Nations Organisation Stabilization Mission in the Democratic Republic of the Congo -MONUSCO*), na Misheni ya Jumuiya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC Mission in Democratic Republic of the Congo - SAMIDRC*) vinachangia Nchi yetu kujiimarisha kiulinzi ipasavyo.

**Mpaka wa Tanzania na Kenya**

14. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu wenye urefu wa kilomita **1,187** ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama dhidi ya Tanzania lililoripotiwa. Hata hivyo, ipo changamoto ya kuharibiwa kwa alama za mpaka. Kazi ya kuimarisha mpaka huu inayotekelezwa na Timu ya wataalam kutoka Tanzania na Kenya inaendelea vizuri. Mpaka sasa, alama za mipaka zimewekwa kuanzia Ziwa Victoria hadi Tarakea Wilaya ya Rombo, Mkoa wa Kilimanjaro.

**Mpaka wa Tanzania na Malawi**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama ya mpaka huu wenye urefu wa kilomita **394**, ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama lililoripotiwa. Ushirikiano uliopo baina ya Jeshi letu na Jeshi la Malawi ni mzuri. Aidha, changamoto ya

mpaka katika Ziwa Nyasa inaendelea kufanyiwa kazi kupitia Tume Maalum ya Usuluhishi (*High Level Mediation Team*) iliyoundwa na Jopo la Viongozi Wastaafu wa Afrika *(African Leadership Forum*). Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inaendelea kutumia njia za kidiplomasia ili kupata ufumbuzi kuhusu suala hilo.

**Mpaka wa Tanzania na Msumbiji**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu wenye urefu wa kilomita **922.76**, haitabiriki kutokana na mashambulizi yanayofanywa na kundi la kigaidi la *Ansar Al Sunna Wal Jamaah (AASWJ)* katika maeneo ya Kaskazini mwa Msumbiji, katika Jimbo la Cabo Delgado linalopakana na mkoa wa Mtwara. Kundi hilo limekuwa likiathiri usalama kwa kuendelea na harakati za kigaidi, ikiwemo kulingania wapiganaji wapya kujiunga na kundi hilo. Hali hii imedhibitiwa kwa kiasi kikubwa, na JWTZ imeendelea kuimarisha ulinzi kwa kufanya operesheni za ndani ya nchi kukabiliana na kundi hilo. Vilevile, JWTZ inashiriki operesheni chini ya Mwamvuli wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika nchini Msumbiji (*SADC Mission in Mozambique - SAMIM*) katika jitihada za kudhibiti ugaidi huo. Operesheni hizi zimeendelea kuimarisha ulinzi katika eneo la mpaka, kudumisha amani na utulivu.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuwa operesheni zimesaidia kupunguza nguvu ya kundi hilo la kigaidi, bado linatekeleza mashambulizi kwa kuhamahama na kubadili mbinu za kimapigano. Vikundi vyetu vinaendelea kupambana kuhakikisha kundi hilo halileti madhara zaidi. Wizara inaishukuru Serikali, hususan **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kulipa kipaumbele suala hili, ikiwa ni pamoja na kutoa fedha kwa ajili ya mahitaji mbalimbali kwa vikundi vyetu kupambana na kundi hilo.

**Mpaka wa Tanzania na Rwanda**

18. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu wenye

urefu wa kilomita **230** ni shwari, ingawa yapo matukio machache ya kihalifu yanayofanywa na wahamiaji haramu na uingizaji wa mifugo kwa ajili ya malisho. Wizara kupitia JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Usalama inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti matukio hayo.

**Mpaka wa Tanzania na Uganda**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika mpaka huu wenye urefu wa kilomita **397.80** ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama wa Nchi yetu. Pamoja na hali hii, ipo changamoto ya uingizaji haramu wa mifugo kwa ajili ya malisho. JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama inaendelea kuchukua tahadhari zote muhimu kuhakikisha kuna usalama katika mpaka huu.

**Mpaka wa Tanzania na Zambia**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika mpaka huu wenye urefu wa kilomita **345**, ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama wa Nchi yetu lililoripotiwa hadi sasa.

**Mpaka wa Tanzania Katika Bahari ya Hindi**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu wenye urefu wa kilomita **1,424**, ni shwari. Katika Mpaka huu tumepakana na Nchi za Komoro na Shelisheli**.** Hakuna tukio lililoripotiwa la kuhatarisha usalama dhidi ya Nchi yetu. Aidha, JWTZ imeendelea kufanya doria za mara kwa mara katika eneo la Bahari ya Hindi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama ili kubaini na kuzuia uharamia, wahamiaji haramu uvuvi haramu, uvuvi wa kutumia mabomu, usafirishaji haramu wa binadamu, usafirishaji wa dawa za kulevya na matishio ya kigaidi.

## C. UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

22. ***Mheshimiwa Spika,*** wakati Wizara ikiwasilisha Hotuba ya bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24 hapo tarehe 24 Mei, 2023. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na

Usalama ilipitia na kujadili utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 na kutoa maoni, ushauri na maelekezo yaliyolenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamezingatiwa na kufanyiwa kazi wakati wa kuandaa na kukamilisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

## D. UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara imeendelea kuzingatia maelekezo yaliyoainishwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya uchaguzi mkuu wa Mwaka 2020 kama inavyoonekana katika maeneo mbalimbali ya hotuba hii. Maelekezo hayo yameainishwa katika Sura ya Tano Ibara ya 105, ya Ilani ifuatavyo:

a. *''Kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na mipaka yake ili kudumisha Muungano, kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, umoja, mshikamano, amani na usalama wa raia na mali zao;*

b. *Kuendeleza jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani;*

c. *Kuwezesha ushirikiano wa vyombo vya ulinzi na usalama kufanya utafiti na ubunifu kwa kushirikiana na taasisi za utafiti;*

d. *Kuhusisha kikamilifu Majeshi ya Ulinzi na Usalama katika kulinda miradi mikubwa ya kimkakati;*

e. *Kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi, uzalendo wa*

f. *kitaifa, usalama na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi ikiwa ni pamoja na Jeshi la Akiba na ulinzi shirikishi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu;*

g. *Kuimarisha uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika kushiriki shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda katika sekta ya*

*ulinzi na maeneo mengine ya kimkakati;*

h. *Kuimarisha viwanda vya NYUMBU na Mzinga ili viweze kutimiza azma ya kuanzishwa kwake;*

i. *Kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ili viwe vyombo vya kuwapatia vijana ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa na pia kuwa vyombo mahiri vya huduma na uzalishaji mali hasa katika ujenzi, kilimo, ufugaji na uvuvi;*

j. *Kupanua na kuongeza idadi ya kambi za JKT na JKU ili kuwezesha vijana wengi zaidi wakiwemo wahitimu wote wa kidato cha sita kupata fursa ya mafunzo ili kujenga uzalendo na moyo wa kujitolea; na*

k. *Kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia makazi bora na kuongezea uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia mafunzo ya kitaaluma na kitaalam, vitendea kazi na zana za kisasa zinazoendana na teknolojia ya kisasa''.*

## E. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

### Tathmini ya Makusanyo ya Maduhuli

24. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu yafuatayo: Fungu 38 - NGOME **Shilingi 22,000,000.00,** Fungu 39 - JKT, **Shilingi 64,403,000.00,** na Fungu 57 - Wizara **Shilingi 1,200,000.00.**

25. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2024, Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 79,352,295.48** sawa na **asilimia 90.58** ya makadirio. Kwa upande wa Fungu 38 - NGOME, yamekusanywa maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 18,969,295.48** sawa na **asilimia 86.22** ya makadirio, ambayo yametokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, na malipo ya kamisheni zinazotokana na makato ya bima kwa wanajeshi kutoka makampuni mbalimbali ya bima. Fungu 39 - JKT lilikusanya **Shilingi 60,383,000.00** sawa na **asilimia 93.80** zilizotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, mauzo ya mazao ya bustani, bidhaa za

mifugo, nafaka, na bidhaa zitokanazo na ufugaji wa nyuki. Fungu 57 - Wizara, haijafanikiwa kukusanya kiasi chochote katika kipindi husika. Mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1**.

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Makusanyo ya Maduhuli Kuanzia Julai 2023 hadi Aprili 2024**

| Fungu | Makadirio ya Mapato 2023/24 (Tshs) | Makusanyo Julai 2023 hadi Aprili 2024 (Tshs) | kusanyo (%) |
|---|---|---|---|
| 38 - NGOME | 22,000,000.00 | 18,969,295.48 | 86.22 |
| 39 - JKT | 64,403,000.00 | 60,383,000.00 | 93.80 |
| 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 0.00 | 0.00 |
| **Jumla** | **87,603,000.00** | **79,352,295.48** | **90.58** |

**Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

**Fedha Zilizoidhinishwa**

26. ***Mheshimiwa Spika***, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,989,967,122,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo katika mafungu yake matatu. Fungu 38 - NGOME, Fungu 39 - JKT na Fungu 57 - Wizara. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,767,133,951,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 222,833,171,000.00** ni kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo. Fungu 38 - NGOME liliidhinishiwa fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 2,273,738,750,000.00**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 48,867,636,000.00**; Fungu 39 - JKT liliidhinishiwa fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 468,397,562,000.00**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 13,965,535,000,00**; Fungu 57 - Wizara liliidhinishiwa fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 24,997,639,000.00**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 160,000,000,000.00**. Muhtasari wa Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeainishwa katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| Fungu | Matumizi ya Kawaida (Tshs) | Shughuli za Maendeleo (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 38 - NGOME | 2,273,738,750,000.00 | 48,867,636,000.00 | 2,322,606,386,000.00 |
| 39 - JKT | 468,397,562,000.00 | 13,965,535,000.00 | 482,363,097,000.00 |
| 57 - Wizara | 24,997,639,000.00 | 160,000,000,000.00 | 184,997,639,000.00 |
| **Jumla** | **2,767,133,951,000.00** | **222,833,171,000.00** | **2,989,967,122,000.00** |

**Fedha Zilizopokelewa Kuanzia Julai 2023 hadi Aprili 2024**

27. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2024 fedha zilizopokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ni **Shilingi 2,389,381,299,149.56** sawa na **asilimia 79.91** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,277,685,836,213.70** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 111,695,462,935.86** ni kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo. Katika kiasi hiki; Fungu 38 - NGOME limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 1,877,499,711,248.87**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 12,345,336,244.00**; Fungu 39 - JKT limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 379,838,502,509.60**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 10,643,690,000.00**; na Fungu 57 - Wizara limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 20,347,622,455.23**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 88,706,436,691.86**. Muhtasari wa mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu yote umeainishwa katika **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa Fedha Zilizopokelewa Kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024**

| Fungu | Aina ya Matumizi | eti kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 (Tshs) | Mapokezi ya Fedha kuanzia Julai 2023 Aprili, 2024 (Tshs) | Asilimi a (%) |
|---|---|---|---|---|
| **38 - NGOME** | Mishahara | 1,819,031,480,000.00 | 1,503,608,229,749.67 | 82.66 |
| | Chakula | 281,802,534,735.00 | 234,835,445,612.50 | 83.33 |
| | Posho ya msamaha wa kodi | 87,888,060,000.00 | 65,916,045,000.00 | 75.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 85,016,675,265.00 | 73,139,990,886.70 | 86.03 |
| | Maendeleo | 48,867,636,000.00 | 12,345,336,244.00 | 25.26 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Jumla ya Fungu** | **2,322,606,386,000.00** | **1,889,845,047,492.87** | **81.37** |
| **39 - JKT** | Mishahara | 316,624,942,000.00 | 263,963,785,343.00 | 83.37 |
| | Chakula | 74,711,214,000.00 | 50,223,545,500.00 | 67.22 |
| | Posho ya msamaha wa kodi | 11,700,000,000.00 | 8,100,000,000.00 | 69.23 |
| | Matumizi Mengineyo | 46,861,406,000.00 | 39,051,171,666.60 | 83.33 |
| | Mafunzo ya Vijana Mujibu wa Sheria | 18,500,000,000.00 | 18,500,000,000.00 | 100.00 |
| | Maendeleo | 13,965,535,000.00 | 10,643,690,000.00 | 76.21 |
| | **Jumla ya Fungu** | **482,363,097,000.00** | **390,482,192,509.60** | **80.95** |
| **57 - WIZARA** | Mishahara | 9,654,200,000.00 | 7,245,761,148.38 | 75.05 |
| | Matumizi Mengineyo | 15,343,439,000.00 | 13,101,861,306.85 | 85.39 |
| | Maendeleo | 160,000,000,000.00 | 88,706,436,691.86 | 55.44 |
| | **Jumla ya Fungu** | **184,997,639,000.00** | **109,054,059,147.09** | **58.95** |
| | **Jumla Kuu** | **2,989,967,122,000.00** | **2,389,381,299,149.56** | **79.91** |

28. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imepokea fedha za nyongeza zenye jumla ya **Shilingi 1,648,083,492,153.66** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mahususi ikiwa ni pamoja na kugharamia mikataba mbalimbali ya zana na vifaa, kulipa madeni ya kimkataba ya zana na vifaa kwa wazabuni wa ndani na nje ya Nchi, kugharamia vikundi vya maafisa na askari katika operesheni mbalimbali ikiwemo Misheni ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya Kupambana na Ugaidi nchini Msumbiji *(SADC Mission in Mozambique - SAMIM*) na Misheni ya Kuleta Amani katika Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo *(SADC Mission in DRC - SAMIDRC*).

**Matumizi ya Fedha za Kawaida**

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2023/24, zimetumika kugharamia: malipo ya stahiki za maafisa, askari na watumishi wa umma; matunzo ya zana na vifaa; mafunzo ya kijeshi na mazoezi; mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa; Mpango Mkakati wa Kilimo na Mifugo; mafunzo ya Jeshi la Akiba; utatuzi wa migogoro ya ardhi; huduma za afya na tiba; ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi kimataifa, kikanda, na baina ya nchi na nchi; ushirikiano na mamlaka za

kiraia katika shughuli mbalimbali; ushiriki katika michezo kitaifa na kimatatifa; mapambano dhidi ya VVU, magonjwa sugu yasiyoambukiza na yanayoambukiza; utawala bora; na utunzaji wa mazingira.

***Mafunzo ya Kijeshi na Mazoezi:***

30. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi katika shule na vyuo vya kijeshi ndani na nje ya nchi kwa wanajeshi. Vilevile, JWTZ imetoa mafunzo ya awali, na kuwaendeleza wanajeshi katika taaluma mbalimbali za uongozi. Pia, imeendelea kupeleka maafisa na askari nje ya nchi kwa ajili ya kupata mafunzo mbalimbali ya kijeshi, ambayo yameongeza weledi katika utendaji. Katika kipindi husika JWTZ ilifanya mazoezi mbalimbali ya kijeshi ikiwemo ya kikanda na kimataifa. Lengo la mafunzo ya kijeshi na mazoezi hayo lilikuwa ni kuimarisha na kuwajengea uwezo maafisa na askari.



Maafisa na askari wakiwa katika zoezi la kujiweka tayari kwa ulinzi wa Taifa lililofanyika Brigedia ya Faru Mkoani Tabora.



Kikundi cha makomando wa JWTZ wakiwa kwenye maonesho ya utayari wa kulilinda Taifa kwenye maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano yaliyofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 26 Aprili, 2024

***Matengenezo na Matunzo ya Zana na Mitambo***

31. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kufanya matengenezo, maboresho na matunzo ya zana na vifaa mbalimbali. Vilevile, ukarabati wa mitambo na mashine umefanyika katika mashirika ya Mzinga na *Tanzania Automotive Technology Centre (TATC),* zaidi ikijulikana kama Shirika la NYUMBU.

***Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa***

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) imeendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa, na stadi za kazi. Katika kipindi husika, mafunzo kwa vijana wa kundi la mujibu wa sheria, na kundi la kujitolea yamefanyika kwenye makambi mbalimbali za Jeshi la Kujenga Taifa kupitia operesheni mbalimbali ambapo idadi ya vijana wa kundi la mujibu wa sheria waliopatiwa mafunzo imeongezeka kutoka 26,000 Mwaka wa

Fedha 2022/23 hadi kufikia 52,119 Mwaka wa Fedha 2023/24. Kati yao wavulana ni 31,256 na wasichana ni 20,863. Aidha, vijana 12,000 wa kujitolea wanaendelea kupatiwa mafunzo katika makambi mbalimbali za JKT.



Vijana wa JKT wakiwa katika mafunzo ya ukakamavu ya Jeshi la Kujenga Taifa.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Kumekuwepo kilio cha muda mrefu cha kuwachukua vijana wote wenye sifa. Napenda kumshukuru **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kukubali kuongeza bajeti katika Mwaka wa Fedha 2023/24 iliyowezesha kuchukua vijana waliomaliza kidato cha sita kwa asilimia 50.8 toka asilimia 29.89 Mwaka wa Fedha 2022/23. Aidha, Wizara inaendelea kufanya tathmini ya mahitaji, na kuandaa mpango utakaowezesha kuchukua vijana wote wenye sifa hatua kwa hatua, kadri bajeti itakavyoruhusu.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu pamoja na umma wa watanzania kwamba, dhumuni la mafunzo yanayotolewa kwa vijana ni kuwajengea uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa, na kuwapatia stadi za

kazi na stadi za maisha, ili wakimaliza mafunzo na kulitumikia Jeshi la Kujenga Taifa waweze kurejea katika jamii wakiwa raia wema wenye uwezo wa kujitegemea na kulilinda Taifa. Nitoe rai kwa vijana wote wanaopata fursa za kupata mafunzo hayo, kuwa raia wema na kuzitumia stadi walizozipata kujiajiri na kujitegemea.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JKT imeendelea pia kutekeleza Mpango Mkakati wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi (2019/2020 – 2024/2025) ambao unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao na kujitosheleza kwa chakula, ili kuipunguzia Serikali gharama za kulisha vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT na kuiwezesha Nchi kuwa na akiba ya chakula. Vilevile, katika kuhakikisha Mkakati huo unafanikiwa, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Mkataba wa Makubaliano katika maeneo ya teknolojia za kilimo, utafiti wa kilimo, uzalishaji wa mazao ya kimkakati na uzalishaji wa mbegu za chikichi, kahawa, mahindi, mpunga na alizeti.

***Mafunzo ya Jeshi la Akiba***

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Akiba ambayo hufanyika katika mikoa yote ya Tanzania. Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 jumla ya wananchi walioandikishwa na kuhitimu mafunzo hayo ni **15,840** ambapo kati yao wanaume ni **13,633** na wanawake ni **2,207**. Vilevile, ofisi za washauri Jeshi la Akiba katika Mikoa na Wilaya, zimeendelea kuelimisha wananchi juu ya masuala ya Ulinzi.

***Huduma za Afya na Tiba***

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi husika, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa huduma za tiba kwa maafisa, askari, watumishi wa umma, na familia zao pamoja na wananchi wanaoishi karibu na Hospitali au vituo vya tiba vya Jeshi. Katika kuboresha huduma za afya, juhudi mbalimbali zimefanyika ikiwemo kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Vilevile, JWTZ imeboresha upatikanaji wa huduma muhimu ikiwemo huduma ya uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo, huduma za usafishaji wa figo, huduma za vipimo vya CT Scan na MRI katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo. Huduma katika hospitali za kanda na vituo vya

tiba vikosini zimeendelea pia kuboreshwa kwa kupatiwa vifaa tiba na kuongezewa madaktari bingwa. Pia, huduma ya Bima ya Afya Jeshini imeboreshwa kwa kuweka utaratibu wa kushirikiana na hospitali zisizo za Jeshi.

***Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi***

*38.* ***Mheshimiwa Spika,*** JWTZ inamiliki maeneo ya kimkakati katika mikoa mbalimbali nchini ambayo yametengwa maalum kwa matumizi ya kijeshi. Imekuwepo migogoro ya Ardhi, na kupitia Mpango wa Kutatua Migogoro ya Ardhi wa Mwaka 2021/22 - 2023/24, Wizara imeendelea kutatua migogoro hiyo ambapo mpaka sasa asilimia 89.7 ya migogoro yote iliyotambuliwa imeweza kutatuliwa kwa kuhuisha mipaka, kupima, na kulipa fidia kwa wananchi wanaostahili. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, fidia ililipwa kwa wananchi katika maeneo ya RTS Kihangaiko, MMTB Kibaoni, Rupungwi, na Makole Mkoa wa Pwani; na Kijiji cha RAU Mkoa wa Kilimanjaro. Aidha, maeneo yaliyokwishafanyiwa uhakiki na yanasubiri kulipwa fidia ni kama inavyonekana katika **Kiambatisho Na. 1.** Hatua iliyofikiwa na maeneo yaliyopimwa na kulipa fidia tangu kuanza kwa mpango huu ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 2.**

*39.* ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kupitia Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa wananchi kutovamia maeneo ya Jeshi kwani kufanya hivyo ni kuhatarisha usalama wa maisha yao, kutokana na shughuli za kijeshi zinazofanyika katika maeneo hayo, ikiwemo mafunzo na mazoezi mbalimbali ambayo yanatumia risasi za moto, milipuko na zana zenye mionzi. Aidha, kufanya uvamizi katika maeneo hayo, ni kuhatarisha usalama wa Taifa, na kukwamisha shughuli muhimu za kuliweka tayari Jeshi letu kukabiliana na matishio yoyote yanayoweza kujitokeza.

***Ushirikiano wa Kiulinzi na Kijeshi na Nchi Nyingine***

40. ***Mheshimiwa Spika,*** JWTZ imeendelea kushirikiana na nchi rafiki katika masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali, ikiwemo mafunzo, misaada ya kitaalamu, zana na vifaa. Vilevile, JWTZ inashirikiana na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

(SADC), na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika mafunzo, ubadilishanaji wataalamu, na operesheni mbalimbali. Aidha, JWTZ inaendelea kushirikiana na nchi rafiki katika kutoa mafunzo kwa maafisa na askari. Nchi hizo ni pamoja na Afrika Kusini, Algeria, Bangladesh, Burundi, Canada, DRC, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Finland, Ghana, Hispania, India, Indonesia, Israel, Jamhuri ya Watu wa China, Jordan, Kenya, Malawi, Marekani, Misri, Morocco, Msumbiji, Nigeria, Oman, Pakistan, Rwanda, Sweden, Ufaransa, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, Uswisi, Zambia na Zimbabwe.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Ulinzi (*National Defence College - Tanzania*) imeendelea kutoa mafunzo ya Usalama na Stratejia kwa maafisa wa vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja, na kwa viongozi katika utumishi wa umma katika ngazi mbalimbali. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 washiriki 53 wanahudhuria kozi ndefu, na washiriki 187 walihudhuria kozi fupi. Mafunzo hayo yanahusisha pia washiriki toka nchi rafiki. Katika kipindi husika, Chuo kimetoa mafunzo kwa washiriki kutoka nchi za Afrika Kusini, Botswana, Burundi, Ethiopia, India, Kenya, Malawi, Misri, Namibia, Nigeria, Rwanda, Sierra Leone, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

***Ushiriki wa JWTZ katika Shughuli za Ulinzi wa Amani***

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka huu wa fedha 2023/24 Serikali kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa. JWTZ imeendelea kuwa na vikosi vya ulinzi wa amani katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Lebanon chini ya Misheni za Umoja wa Mataifa. Vilevile, Serikali kupitia JWTZ inashiriki katika Misheni za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya kupambana na ugaidi na vikundi vya uhalifu nchini Msumbiji (SADC Mission in Mozambique - SAMIM), na Misheni ya SADC ya kuleta amani katika Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (SADC Mission in DRC - SAMIDRC). Pia, Wizara kupitia JWTZ inao maafisa wanadhimu na makamanda kwenye operesheni za ulinzi wa amani nchini Sudan Kusini, Lebanon, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.




Askari wa JWTZ wakiwa katika ulinzi wa Amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya
Kongo (DRC).

43. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wa JWTZ katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa, na Jumuiya za Kikanda, umeiwezesha Nchi yetu kutimiza matakwa ya itifaki ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, na Jumuiya za Kikanda ya kushiriki katika ulinzi wa amani. Ushiriki huu unaendeleza Diplomasia ya Kijeshi, unakuza na kuimarisha uhusiano, na kuliwezesha JWTZ kupanua uwezo kwa kufanya kazi na majeshi ya nchi nyingine, na hii ni utekelezaji wa azma ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kama alivyosema wakati wa hafla ya *Sherry Party* tarehe 07 Februari, 2024, nanukuu "Kwa kuwa Tanzania ni sehemu ya Jumuiya ya kimataifa, itaendeleza nia yake ya dhati ya kudumisha na kuzingatia misingi ya maadili ya Umoja wa Mataifa, tuendelee kuunga mkono juhudi zote za amani na usalama.

***Ushirikianona Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali***

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali zikiwemo, kutoa misaada wakati wa majanga na maafa, kushiriki katika utekelezaji na ulinzi wa miradi ya kimkakati. Hii ni pamoja na katika mabonde na vyanzo vya maji, Reli ya Kiwango cha Kimataifa (*Standard Gauge Railway*), Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP), Mgodi wa *Tanzanite*, ujenzi wa Bomba la Mafuta kati ya Tanzania na Uganda, Daraja la Busisi, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), na maeneo ya viwanja vya ndege. Vilevile, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushiriki katika kuokoa raia na mali zao wakati na baada ya maafa na majanga, yakiwemo maporomoko ya matope yaliyotokea Wilaya ya Hanang' Mkoa wa Manyara na mafuriko sehemu mbalimbali nchini kufuatia mvua za Elnino zilizoungana na mvua za masika na vuli. Aidha, Wizara kupitia JWTZ kwa kulitumia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kupitia SUMAJKT imeendelea na ujenzi wa nyumba 5,000 Msomera Wilaya ya Handeni Mkoa wa Tanga, kwa ajili ya wananchi wanaohama kwa hiari kutoka Hifadhi ya Ngorongoro; na nyumba 73 huko Hanang kwa ajili ya wahanga wa maporomoko ya udongo. Baba wa Taifa Mwl. Julius Kamabarage Nyerere alisema "Jambo lililo kubwa zaidi ni kwamba wanajeshi wetu sasa ni sehemu ya jamii yetu, na uaminifu wao umedhihirika mara nyingi toka jeshi lilipoundwa upya mwaka 1964". Niwatie moyo wanajeshi wetu waendelee kuwa sehemu ya jamii.



Askari wa JWTZ wakiwa katika shughuli za uokoaji wakati wa maafa ya maporomoko ya matope Wilaya ya Hanang' mkoa wa Manyara.

*Ushiriki katika Michezo ya Kitaifa na Kimataifa*

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mwaka wa Fedha 2023/24 imeshiriki michezo mbalimbali ikiwemo SHIMIWI iliyofanyika Mwezi Septemba hadi Oktoba 2023 Mkoa wa Iringa na michezo ya Mei Mosi iliyofanyika kuanzia Mwezi Aprili hadi Mei, 2024 Mkoa wa Arusha. Vilevile, Shirika la Mzinga limeshiriki mashindano ya Shirikisho la michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA), yaliyofanyika Jijini Dodoma Mwezi Novemba 2023. Katika mashindano hayo, Shirika la Mzinga limeweza kushika nafasi ya pili kwa mshindi wa jumla katika michezo mbalimbali. Aidha, Wizara imeshika nafasi ya pili kwa mshindi wa jumla katika mashindano ya michezo ya Mei Mosi yaliyofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 14 Aprili hadi 30 Aprili, 2024.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeshiriki katika michezo mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwemo; mashindano

ya Gofu ya Majeshi ya Dunia (*World Military Golf Championship*) yaliyofanyika San Diego nchini Marekani tarehe 01 - 08 Oktoba 2023, Mashindano ya Dunia ya Michezo ya Majeshi (*World Military Championship Half Marathon*) yaliyofanyika Uswisi tarehe 27 - 30 Oktoba 2023, Mashindano ya Ngumi ya klabu bingwa ya Taifa yaliyofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 15 - 20 Desemba 2023, mashindano ya riadha yaliyofanyika Umoja wa Falme za Kiarabu - UAE (*Ras Al Khaimah Half Marathon*) tarehe 24 Februari 2024, Pambano la Ngumi la *World Boxing Federation in Africa* (WBF) lililofanyika tarehe 01 Machi 2024 jijini Dar es Salaam, mashindano ya riadha yaliyofanyika nchini Brazil (*San Blas Half Marathon*) tarehe 03 Machi, 2024 na mashindano ya riadha ya Shanghai yaliyofanyika nchini China (*Shanghai Marathon*) tarehe 24 Machi, 2024.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Wizara kupitia JKT imeshiriki michezo mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwemo, mashindano ya ubingwa wa mpira wa miguu kwa wanawake ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yaliyofanyika tarehe 12 - 30 Agosti, 2023 nchini Uganda ambapo JKT Queens ilitwaa ubingwa. Pia, timu hiyo ilishiriki Mashindano ya Klabu Bingwa Barani Afrika kwa Wanawake yaliyofanyika nchini Ivory Coast tarehe 05 - 19 Novemba, 2023. Aidha, Timu ya Mashujaa imefanikiwa kuingia hatua ya robo fainali ya kombe la Shirikisho la CRDB.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika michezo hii na mashindano haya, wanamichezo wetu waliweza kupata ushindi na kuliletea Taifa letu medali. Napenda kutumia fursa hii, kuzipongeza timu zetu zote kwa ushindi walioupata ikiwa ni pamoja na JKT Queen kutwaa ubingwa wa CECAFA, Mashujaa kuingia robo fainali ya kombe la Shirikisho la CRDB. Aidha, napenda kuwapongeza, **Sajini Alphonce Felix Simbu,** aliyepata Medali ya Fedha katika Mashindano ya Majeshi ya Dunia ya Mbio za Riadha (*Shanghai Marathon*)**, Koplo Magdalena Crispin Shauri** aliyepata Medali ya Shaba Mashindano ya Dunia ya Michezo ya Majeshi yaliyofanyika nchini Uswisi na **Sajin Taji Jackline Juma Sakilu** alikuwa mshindi wa tatu kwa upande wanawake katika Mashindano ya Riadha yaliyofanyika Umoja wa Falme za Kiarabu - UAE. Vilevile, **Sajini Taji Sakilu** alishika nafasi ya kwanza katika Mashindano ya Riadha ya Shanghai Marathon yaliyofanyika nchini China tarehe 24 Machi,

2024 na **Praiveti Najiat Idrisa Abasi** aliyekuwa Golikipa bora katika Mashindano ya Ubingwa wa Mpira wa Miguu kwa wanawake Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

49. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki huo umewezesha JWTZ kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati yake na nchi rafiki na vyombo vya ulinzi na usalama. Vilevile, nchi yetu imepata fursa ya kuandaa Mkutano Mkuu wa Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (CISM) utakaofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 12 – 19 Mei, 2024.



Timu ya Mpira wa Miguu ya Wanawake JKT Queens ilivyotwaa ushindi katika mashindano ya ligi Kuu ya Wanawake (CAF Women's Champions League).

***Mapambano dhidi ya VVU, magonjwa sugu yasiyoambukiza na yanayoambukiza***

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupambana na Virusi vinavyosababisha Upungufu wa Kinga Mwilini na Magonjwa yasiyoambukiza, katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kupambana na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe kwa watumishi wenye maambukizi ya VVU. Hatua hizi zinachukuliwa kwa kuzingatia mwongozo wa udhibiti VVU na UKIMWI. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya

Afya imetoa elimu na kuhamasisha upimaji wa hiari, na uchangiaji damu.

*Utawala Bora*

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara pamoja na taasisi zake imeendelea na jitihada mbalimbali ili kuimarisha Utawala Bora. Wizara na taasisi zake zimekuwa zikiandaa taarifa za kila Robo Mwaka ambazo huwasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Vilevile, semina mbalimbali kwa watumishi, kuhusu jinsi ya kupambana na kuzuia rushwa mahala pa kazi zimeendelea kutolewa. Wizara imekuwa ikishirikisha watumishi katika kutoa maoni na ushauri kupitia vikao mbalimbali, hususan vikao vya Idara/Vitengo, Baraza la Wafanyakazi, Kamati ya Maadili, Bodi ya Zabuni, na Kamati ya Ajira. Aidha, kuzingatia sheria za matumizi ya fedha za umma na ununuzi, ambapo Wizara na taasisi zake zimeendelea kupata hati safi za ukaguzi. Juhudi hizi zimeimarisha Utawala Bora kwa Wizara na taasisi zake.

*Utunzaji wa Mazingira*

52. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za utunzaji wa mazingira, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara kupitia taasisi zake imeendelea na utunzaji wa mazingira katika maeneo yake yenye miti ya asili, kuyalinda maeneo hayo yasivamiwe kwa shughuli za kijamii na kuendelea kupanda miti mipya. Katika kipindi husika Wizara imepanda miti **983,106** kwa mchanganuo ufuatao: JWTZ miti **37,343**, JKT miti **648,063,** TATC miti **2,500** na Mzinga miti **295,200**. Vilevile, Wizara imeendelea na utunzaji wa fukwe katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi. Aidha, maeneo yote ya Jeshi yana zuio la ukataji miti, kuchoma mkaa na kuchunga mifugo. Napenda nitoe wito kwa wananchi wote kuzingatia zuio la ukataji miti, kuchoma mkaa na kuchunga mifugo katika maeneo ya Jeshi.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutimiza adhma ya Mheshimiwa Rais kuhusu utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa taasisi ambazo zinalisha zaidi ya watu 100, JWTZ na makambi yake imefikia asilimia 90 ya matumizi ya nishati safi ya

kupikia, Jeshi la Kujenga Taifa limefikia asilimia 98, Shirika la Mzinga asilimia 98, na Shirika la TATC asilimia 95.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** mashirika yaliyo chini ya Wizara ambayo ni TATC, Mzinga na SUMAJKT yameendelea na uzalishaji wa bidhaa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na njia za kisasa za kutibu maji yenye kemikali yanayotoka viwandani. Vilevile, viwanda vimeendelea na utaratibu wa kuwapa wafanyakazi wake vifaa kinga vyenye mfumo wa kudhibiti sauti ili kuzuia madhara yatokanayo na kelele.

**Matumizi ya Fedha za Maendeleo**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara imeweza kutumia fedha za maendeleo kutekeleza yafuatayo:

a. Ununuzi wa zana na vifaa;
b. Uhuishaji na uboreshaji wa zana za kijeshi;
c. Kugharamia mikataba ya matengenezo na matunzo ya zana;
d. Ujenzi wa maghala ya kuhifadhi zana na vifaa katika mikoa mbalimbali;
e. Ujenzi wa Hospitali Kuu ya Kanda ya Jeshi huko Msalato Dodoma kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani;
f. Ujenzi wa miundombinu na majengo katika Hospitali ya Jeshi ya Kanda - Mwanza;
g. Ujenzi wa Jengo la Ramani;
h. Kulipa fidia kwa wananchi katika vijiji vya Rau katika Manispaa ya Moshi; Kibaoni, Makole, Rupungwi na Kihangaiko katika Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze;
i. Ununuzi wa magari kwa ajili ya matumizi ya Jeshi;
j. Ujenzi wa Miundombinu ya Skimu ya Umwagiliaji katika Kikosi cha Chita JKT Mkoa wa Morogoro;
k. Ujenzi wa mahanga ya vijana katika vikosi vya JKT;
l. Mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi; na
m. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi katika mikoa mbalimbali.

PICHA ZA MIRADI ILIYOTEKELEZWA KWA FEDHA ZA MAENDELEO MWAKA WA FEDHA 2023/24



Jengo la Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa (MMUT) lililopo katika hatua za mwisho za ujenzi eneo la Kikombo, Jijini Dodoma.



Maghala mapya ya kuhifadhi vifaa vya kijeshi katika Kikosi cha Gongolamboto, Dar- es-Salaam.



Kamati ya kudumu ya Bunge Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ikiongozwa na Mwenyekiti Mhe. Vita Rashid Kawawa (Mb.) ilipotembelea Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makazi kwa washiriki wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi tarehe 16 Machi, 2024. Kunduchi Jijini Dar es Salaam.



Miundombinu ya skimu ya umwagiliaji katika Kikosi cha Chita JKT, Mkoa wa Morogoro



Mahanga ya vijana wa JKT yaliyojengwa katika Kikosi cha Mtabila JKT Mkoa wa Kigoma.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JKT imefanikiwa pia kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia rasilimali za ndani ifuatavyo:

a. Kilimo cha chikichi katika Kikosi cha Bulombora Mkoa wa Kigoma;
b. Kilimo cha mkonge katika vikosi vya Maramba na Mgambo Mkoa wa Tanga;
c. Kilimo cha kahawa katika vikosi vya Itende Mkoa wa Mbeya na Rwamkoma Mkoa wa Mara;
d. Kilimo cha korosho katika vikosi vya Nachingwea Mkoa wa Mtwara, Makutopora Mkoa wa Dodoma, Ruvu na Kibiti Mkoa wa Pwani;
e. Ufugaji wa samaki katika vikosi vya Rwamkoma Mkoa wa Mara, Chita Mkoa wa Morogoro, na Ruvu Mkoa wa Pwani; na
f. Ufugaji wa nyuki katika vikosi vya Msange Mkoa wa Tabora, Kanembwa na Mtabila Mkoa wa Kigoma.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia mashirika yake ya *Tanzania Automotive* Technology Centre - (*TATC)*; Mzinga; na SUMAJKT imeendelea kutekeleza majukumu yake ifuatavyo:

**Tanzania Automotive Technology Centre (TATC) – Nyumbu**

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Shirika liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 15,575,090,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi wa 2021/22 - 2031/32 wa Kuliimarisha Shirika. Hadi kufikia Mwezi Aprili 2024, Shirika limepokea jumla ya **Shilingi 5,033,058,242.00** sawa na **asilimia 32.31** ya kiasi kilichoidhinishwa. Fedha hizi zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

a. Ujenzi wa Jengo la Karakana Kuu ya kukalibu chuma;
b. Kuwaendeleza kitaaluma wataalam katika fani ya utafiti, usubiaji chuma na uunganishaji wa magari;
c. Kuendeleza utafiti na kuzalisha sampuli kifani ya Gari la Deraya na Gari la Nyumbu; na
d. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya milki (majengo, barabara za ndani na mifumo ya umeme na maji).

59. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, TATC pamoja na majukumu yake ya msingi imeweza pia, kutekeleza shughuli zifuatazo kwa kutumia rasilimali za ndani:

a. Kufanya maboresho ya kuongeza vifaa muhimu kwenye magari 182 ya kubeba wagonjwa kutoka Wizara ya Afya;
b. Utengenezaji wa vifaa kwa ajili ya matumizi ya JWTZ;
c. Utengenezaji wa vipuri mbalimbali vya Shirika la Reli; na
d. Ukarabati wa pampu za maji na vipuri vya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

**Shirika la Mzinga**

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Shirika la Mzinga liliidhinishiwa **Shilingi 4,000,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa malighafi, vipuri, zana na mashine kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya msingi. Fedha hizo zinatarajiwa kupokelewa kabla ya Mwezi Juni 2024.

61. ***Mheshimiwa Spika***, Shirika la Mzinga limeendelea kutekeleza majukumu ya msingi ifuatavyo:

a. Kuendelea kuzalisha mazao ya msingi kwa matumizi ya JWTZ na vyombo vingine vya usalama;
b. Kuendelea kufanya ukarabati wa zana na vifaa vya kijeshi; na

c. Kuendelea kufanya tafiti za kijeshi na kiraia hususan utafiti wa bomu baridi la kufukuza Tembo kwenye makazi ya watu yaliyopo karibu na hifadhi ambalo limeanza kutumika.

62. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Shirika limeendelea kutekeleza shughuli zifuatazo kwa kutumia rasilimali za ndani:


a. Kuendelea kufanya maboresho ya miundombinu na ujenzi wa majengo;
b. Kuendelea kutoa huduma za ujenzi kupitia Kampuni tanzu ya Mzinga; na
c. Kuendelea kutoa huduma ya Kumbi za Mikutano na Malazi, huduma za afya na mafunzo ya Ufundi Stadi.

**Shirika la Uzalishaji Mali la JKT**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT), liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,000,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa zana za kilimo. Kiasi hiki cha fedha kimechangia katika kuimarisha uzalishaji wa chakula ili kuipunguzia Serikali gharama za malezi ya vijana wanaojiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na kuiwezesha JKT kujitosheleza kwa chakulakwa vijana wa JKT, na kuchangia pia katika usalama wa chakula na uzalishaji wa mbegu. Aidha, SUMAJKT ni shirika linalojitegemea na linafuata taratibu za Mashirika ya Umma. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2023 hadi Aprili 2024, SUMAJKT limeendelea kutekeleza shughuli za uzalishaji mali kupitia kampuni tanzu na viwanda vyake. Shughuli hizo zinatekelezwa kupitia sekta ya ujenzi, viwanda, biashara na huduma, kilimo, mifugo na uvuvi. Taarifa za utendaji hutolewa kwa kuzingatia sheria na taratibu za Mashirika ya Umma.



Nyumba zilizojengwa na SUMAJKT Construction Company Msomera Mkoani Tanga kwa ajili ya wananchi wanaohama kwa hiari kutoka Hifadhi ya Ngorongoro.



Mashine ya kumwagilia maji katika shamba la Mpunga lililopo Mngeta Ifakara Mkoa  wa Morogoro.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kutoa umuhimu na uzito mkubwa katika shughuli za ulinzi, ikiwa ni pamoja na kutoa fedha kwa shughuli mahususi, na operesheni maalum kadri inavyojitokeza na kuhitajika.

## F. MPANGO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/25, Mpango na Bajeti kwa kuzingatia Dira na Dhima ya Wizara, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs), Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba uniruhusu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 ifuatavyo:

### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

67. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2024/25, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu, ambapo Fungu 38 - NGOME linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 22,000,000.00,** Fungu 39 - JKT linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 64,403,000.00,** na Fungu 57 - Wizara linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 1,200,000.00** kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.**

**Jedwali Na 4: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/25**

| Na. | Fungu | (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | 38 - NGOME | 22,000,000.00 |
| 2 | 39 - JKT | 64,403,000.00 |
| 3 | 57 - Wizara | 1,200,000.00 |
| | **Jumla** | **87,603,000.00** |

**Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

68. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2024/25, Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shughuli za Maendeleo ikiwa na jumla ya **Shilingi 3,326,230,419,000.00** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,008,812,907,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 317,417,512,000.00** ni kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo. Fungu 38 - NGOME linatarajia kutengewa kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 2,491,439,934,000.00,** na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 48,867,636,000.00.** Fungu 39 - JKT linatarajia kutengewa kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 490,652,279,000.00** na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 8,549,876,000.00**; na Fungu 57 - Wizara linatarajiwa kutengewa kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 26,720,694,000.00,** na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 260,000,000,000.00**. Mchanganuo umeainishwa katika **Jedwali Na. 5.**

**Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25**

| Na | Fungu | Matumizi ya Kawaida (Tshs) | Matumizi ya Maendeleo (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 38 - NGOME | 2,491,439,934,000.00 | 48,867,636,000.00 | 2,540,307,570,000.00 |
| 2 | 39 - JKT | 490,652,279,000.00 | 8,549,876,000.00 | 499,202,155,000.00 |
| 3 | 57 - Wizara | 26,720,694,000.00 | 260,000,000,000.00 | 286,720,694,000.00 |
| | **Jumla Kuu** | **3,008,812,907,000.00** | **317,417,512,000.00** | **3,326,230,419,000.00** |

69. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2024/25 zitazingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo:

a. Kuendelea kuliimarisha Jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa, mafunzo na mazoezi, pamoja na rasilimali watu;
b. Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi wa Jeshi ikiwemo maslahi, huduma bora za afya na makazi;
c. Kuimarisha miundombinu mbalimbali katika maeneoya Jeshi;
d. Kuimarisha mashirika na taasisi katika Sekta ya Ulinzi;

e. Kuendelea kushiriki katika ujenzi na ulinzi wa miradi ya kimkakati kwa maslahi mapana ya Taifa;
f. Kuendelea kuimarisha uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuboresha miundombinu ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi watakaopata mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa, na stadi za kazi kwa vijana wa kundi la lazima na wakujitolea;
g. Kufanya tathmini ya hali ilivyo ya mafunzo ya JKT na kuandaa Mpango Mkakati utakaoainisha mahitaji, bajeti na muda wa utekelezaji, kwa lengo la kuweza kuchukua vijana wote wanaostahili kupata mafunzo ya JKT kwa kundi la lazima;
h. Kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya za Kikanda, na nchi mbalimbali katika nyanja za kijeshi na kiulinzi na hivyo kuimarisha Diplomasia ya Ulinzi; na
i. Kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura inapohitajika.

**G. SHUKRANI**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijahitimisha Hotuba yangu, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Viongozi na watendaji wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipatia, kazi kubwa wanayoifanya, na michango yao madhubuti katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24, na kutayarisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ninayoiongoza kwa Mwaka wa Fedha 2024/25. Napenda kumshukuru **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe,** Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, **Jenerali Jacob John Mkunda,** Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, **Luteni Jenerali Salum Haji Othman,** Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, **Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele,** Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Wakuu wa Kamandi zote, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Matawi Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** pia napenda kupitia Bunge lako Tukufu kutoa shukrani kwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi **Jenerali Jacob John Mkunda,** Mnadhimu Mkuu wa Jeshi **Luteni Jenerali Salum Haji Othman,** Maafisa na Askari wote kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha Taifa letu lina amani na ni imara. Asanteni sana.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee namshukuru **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuhakikisha kuwa Wizara, Jeshi na Taasisi zake zinaweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Wizara itaendelea kutekeleza majukumu ili kutekeleza maono ya **Mhe.** Rais na Amiri Jeshi Mkuu ikiwa ni pamoja na kuliimarisha Jeshi letu. Katika mkutano wa saba wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na makamanda, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu alisema "*yapo maendeleo makubwa katika Sayansi na Tecknolojia yanayoendelea na yanayopelekea changamoto mpya za kiulinzi na usalama. Hivyo hamna budi kuwa tayari kukabiliana na changamoto hizo*". Maelekezo haya yanaonesha dhamira ya Mhe. Rais na Amiri Jeshi Mkuu kuhakikisha kuwa Jeshi letu ni imara wakati wote. Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara na Taasisi zake zinatekeleza maagizo haya kwa vitendo.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii, kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani kwa Taasisi za Kimataifa na Kikanda, na serikali za nchi mbalimbali, kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia ikiwa ni pamoja na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, Afrika Kusini, Algeria, Bangladesh, Burundi, Canada, DRC, Ethiopia, Finland, Ghana, Hispania, Indonesia, India, Israel, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Czech, Jordan, Kenya, Malawi, Marekani, Misri, Msumbiji, Morocco, Nigeria, Oman, Pakistan, Rwanda, Serbia, Sweden, Ufaransa, Ujerumani, Uturuki, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi, Uswisi, Zambia na Zimbabwe.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Wizara ya Ulinzi na JKT, na taasisi zake katika ulinzi wa nchi yetu. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Taifa letu.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuishukuru familia yangu kwa kunitia moyo na upendo wao kwangu unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru wewe binafsi, Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii, inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo ni ***www.modans.go.tz***

77. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kumalizia, napenda kutoa rai kwa watanzania kuwa jukumu la ulinzi na usalama ni lakila mtanzania. Aidha, wito huu umetiliwa mkazo na kuhimizwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wakati akihutubia Taifa kuelekea Miaka 60 ya Muungano hapo tarehe 25 Aprili, 2024 aliposema kuwa, "Hapa nataka kukumbusha kwamba, Mlinzi wa kwanza wa usalama wa nchi ni mwananchi mwenyewe. Kila mmoja wetu awe macho na ashirikiane na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kubaini, kuzuia na kukabiliana na matishio kwa usalama wa jamii zetu na nchi kwa ujumla".

78. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe kiasi cha **Shillingi 3,326,230,419,000.00** katika Mwaka wa Fedha 2024/25 kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kati ya fedha hizo, **Shillingi 3,008,812,907,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shillingi 317,417,512,000.00** ni kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa Hoja.

**KIAMBATISHO NA. 1**

**MAENEO YALIYOKWISHAFANYIWA UTHAMINI BADO KULIPWA FIDIA KATIKA KIPINDI CHA MKAKATI ULIOANZIA 2020/21 HADI 2022/23 (MAOMBI YAMEWASILISHWA HAZINA)**

| Na. | Eneo | Mkoa | Fidia (Tshs) | Kitabu kilipo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 191 Regt Bomani Kibasila Kisarawe | Pwani | 2,520,249,865.00 | HAZINA |
| 2 | SKM Rufiji | Pwani | 230,958,981.00 | HAZINA |
| 3 | Minara 4 | Pwani | 8,838,170.00 | HAZINA |
| 4 | Senje Msalato | Dodoma | 3,167,352,000.00 | HAZINA |
| 5 | Chimlata | Dodoma | 459,725,310.00 | HAZINA |
| 6 | Mnara moreti Kongwa | Dodoma | 7,958,100.00 | HAZINA |
| 7 | Mnara Ibiwha Bahi | Dodoma | 10,883,460.00 | HAZINA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8 | AFS/601KJ Kiseke Ilemela | Mwanza | 354,795,000.00 | HAZINA |
| 9 | 977/Regt Olumitu Losirway | Arusha | 3,016,902,317.28 | HAZINA |
| 10 | Mnara Arumueru | Arusha | 13,345,262.50 | HAZINA |
| 11 | Mnara Usariva | Arusha | 13,584,913.00 | HAZINA |
| 12 | 977 Regt Losirway Moshono | Arusha | 2,278,836,961.06 | HAZINA |
| 13 | Mtabila JKT 825KJ | Kigoma | 1,312,755,175.49 | HAZINA |
| 14 | Mnara Dakawa Mvomero | Morogoro | 1,644,804.00 | HAZINA |
| 15 | Mnara Fulwe/Mikese | Morogoro | 757,613.50 | HAZINA |
| 16 | SMH Pangawe Vol 1 (152acres) | Morogoro | 84,416,152.00 | HAZINA |
| 17 | SMH Pangawe Vol 2 (152acres) | Morogoro | 335,868,372.25 | HAZINA |
| 18 | SMH Pangawe Ngong'olo | Morogoro | 2,975,154,589.99 | HAZINA |
| 19 | 601KJ Ngerengere | Morogoro | 147,342,403.45 | HAZINA |
| 20 | Mabama Uyui DC | Tabora | 363,003,000.00 | HAZINA |
| 21 | 122 Regt Rest House Ipazi (PAPS 20) | Tabora | 83,767,220.00 | HAZINA |
| 22 | 122 Regt Nhobola Nzega | Tabora | 2,112,593,174.00 | HAZINA |
| 23 | Itaka Sasenga Village | Songwe | 3,491,271,800.00 | HAZINA |
| 24 | Itaka Mboji Village | Songwe | 74,358,600.00 | HAZINA |
| 25 | Itaka Itewe Village | Songwe | 2,150,311,800.00 | HAZINA |
| 26 | Mnara Hedaru Same | Kilimanjaro | 7,628,000.00 | HAZINA |
| 27 | Mnara Kiverenge, Mwanga | Kilimanjaro | 7,246,010.00 | HAZINA |
| 28 | Mnara Kitifu, Korogwe | Tanga | 7,628,600.00 | HAZINA |
| 29 | Minara 2, Kabuku & Kitumbi | Tanga | 19,211,200.00 | HAZINA |
| 30 | Minara 2, Mazinde & Buiko | Tanga | 14,738,100.00 | HAZINA |
| 31 | Mnara Michungwani, Muheza | Tanga | 19,883,800.00 | HAZINA |
| 32 | Minara 4 ya DSM | DSM | 85,759,635.00 | HAZINA |
| 33 | Mnara wa Mseko, Iramba | Singida | 10,970,130.00 | HAZINA |
| | **JUMLA** | | **25,389,740,519.52** | |

**KIAMBATISHO NA. 2**

## MAENEO YALIYOPIMWA NA KULIPWA FIDIA

| Mwaka Wa Fedha | Na. | Eneo | Mkoa | Malipo Ya Fidia (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| **2021/22** | 1. | Mitwelo | Lindi | 181,919,027.44 |
| | 2. | Ras Mishindo | Lindi | 624,236,405.00 |
| | 3. | Bugasha | Kagera | 3,772,349,754.00 |
| | 4. | Mayondwe | Kagera | |
| | 5. | Nyamigaju | Kagera | |
| | 6. | Kibonangoma | Kagera | |
| | 7. | Itoju | Kagera | |
| | 8. | Nyamisangura | Mara | 2,288,466,639.05 |
| | 9. | Nyabange | Mara | 203,649,661.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 10. | Kigongo Ferry | Mwanza | 676,522,440.00 |
| | 11. | Lukobe na Buduku | Mwanza | 6,148,022,486.58 |
| | 12. | Nyagungulu | Mwanza | 160,035,200.00 |
| | 13. | Chato | Geita | 972,218,036.00 |
| | 14. | Kikombo phase II | Dodoma | 2,261,604,837.45 |
| | | **Jumla** | | **17,289,024,486.52** |
| **2022/23** | 1. | Gurungu | Singida | 254,679,723.59 |
| | 2. | Mtipa | Singida | 229,052,639.00 |
| | 3. | Mkwese | Singida | 25,575,512.52 |
| | 4. | Mkiwa | Singida | 184,248,479.89 |
| | 5. | Choda | Singida | 56,474,828.04 |
| | 6. | Kisakasaka | Zanzibar | 5,530,069,975.00 |
| | 7. | Chukwani | Zanzibar | 1,247,603,905.15 |
| | 8. | Itaga na Usule | Tabora | 194,029,643.00 |
| | 9. | Ras Nondwa | Kigoma | 2,488,033,681.27 |
| | 10. | Kibiti | Pwani | 721,761,651.79 |
| | 11. | Funta | Pwani | 330,788,467.00 |
| | 12. | Machenje | Dodoma | 388,126,941.00 |
| | 13. | Bulifani | Kagera | 492,962,708.00 |
| | 14. | Tondoroni | Pwani | 46,712,720.00 |
| | | **Jumla** | | **12,190,120,875.25** |
| **2023/24** | 1. | RTS Kihangaiko | Pwani | 7,407,109,340.40 |
| | 2. | MMTB (Kibaoni, Rupungwi na Makole) | Pwani | 1,737,440,082.10 |
| | 3. | Kijiji cha RAU | Kilimanjaro | 28,873,130.28 |
| | | **Jumla** | | **9,173,422,552.78** |

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, hoja imeungwa mkono. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha

2023/2024, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa uchambuzi wa Kamati; msingi wa Kamati kuchambua makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na masharti ya kifungu cha 6(3) kikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa masharti haya yamezingatiwa na kwamba ninaliomba Bunge hili lijadili hoja ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawanda ya taarifa; taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi yaliyochambuliwa inagusa Mafungu matatu ya Kibajeti ambayo ni Fungu 38 - NGOME, Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutambulisha mawanda ya taarifa, ninaomba kuisoma taarifa hii kwa muhtasari ili kuendana na muda pasipo kuathiri mtiririko wa maudhui. Hata hivyo, kwa umuhimu wa kumbukumbu kamili, ninaomba taarifa yote kama ilivyowasilishwa mezani mapema leo hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi ya washiriki wa kozi za Chuo cha Taifa cha Ulinzi *(NDC)* Kunduchi, Dar es Salaam. Mradi huo ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

Taarifa kuhusu ukaguzi wa miradi hii ni kama inavyoonekana katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024; uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulilenga kulinganisha makusanyo ya mapato na lengo la makusanyo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za matumizi mengineyo na upatikanaji wa fedha za maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa mafungu yote matatu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo; moja, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati; wakati wa kuchambua mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Kamati ilishauri masuala mbalimbali yanayopaswa kufanyiwa kazi na Wizara hii. Naomba kuliarifu Bunge lako kuwa taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba Serikali imezingatia sehemu ya ushauri kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 1 cha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uzingatiaji wa ushauri, upo ushauri ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali, mathalani ushauri kuhusu Serikali kufanya mapitio ya Sheria za Kodi zinazotoza kodi za vifaa vya Jeshi pamoja na mashine mbalimbali ili kuweka utaratibu mzuri wa kutoa msamaha wa kodi kwa vifaa vyote vinavyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, uchambuzi wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2023/2024; Kamati ilipitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024, kwa kuchambua hali ya ukusanyaji wa mapato pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi milioni 87.6 kwa Mafungu yote matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia mwezi Februari, 2024 kiasi cha fedha za maduhuli kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa shilingi milioni 57.6 sawa na 66% ya lengo la mwaka lililopangwa. Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa ni pungufu kwa shilingi milioni 7.1 sawa na 11% ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambayo yalikuwa ni shilingi milioni 64.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa, makusanyo hayo yamechangiwa na Mafungu ya Wizara ambapo Fungu 38 - Ngome limekusanya 20.5% na Fungu 39 - JKT limekusanya 79.5% ya kiasi kilichokusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Fungu 57 – Wizara; hadi kufikia mwezi Machi, 2024 halikuwa limekusanya kiasi chochote cha fedha sawa na mwaka wa fedha wa 2022/2023 ambapo hadi kufikia Februari, 2023 Wizara haikuwa imekusanya kiasi chochote cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01 na Grafu Na. 01.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa makusanyo yaliyopatikana kwa kila Fungu kufikia mwezi Februari, 2024 na makusanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/2023 kama inavyoonekana katika Grafu Na. 02.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa: -

(i) Makusanyo katika Fungu 38 - Ngome yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa 25% lakini katika

utekelezaji Fungu hilo limechangia kwa 20.5% ya kiasi kilichokusanywa;

(ii) Makusanyo ya Fungu 39 - JKT yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa 74% lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya JKT yamechangia kwa 79.5% ya kiasi kilichokusanywa; na

(iii) Makusanyo ya Fungu 57 - Wizara yalikusudiwa kuchangia kwa 1.3% kwenye mapato yote ya Wizara lakini hali halisi imeonesha Wizara haijakusanya mapato yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo ni mzuri kwa Fungu 39 pekee ambapo kufikia mwezi Februari, 2024 lilikuwa limekusanya 79.5%. Aidha, mwenendo wa Fungu 38 na 57 siyo mzuri, kwani Fungu 38 halijafanikiwa kufikia lengo kwani kufikia Februari, 2024 lilikuwa limekusanya 20.5% ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 57 - Wizara halikuweza kukusanya kiasi chochote hadi kufikia mwezi Februari, 2024. Fungu hili pia halikuweza kukusanya kiasi chochote katika mwaka wa fedha 2022/2023. Kushindwa kukusanya kiasi chochote kwa muda wa miaka miwili mfululizo ni wazi kuwa makisio yanayowekwa hayana uhakika na hayaakisi uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; baada ya kupokea taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2023/2024, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha fedha kilichotolewa hadi kufikia Februari, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha

Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ililinganisha uwiano wa bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekana katika Jedwali Na. 2 na Na. 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia uchambuzi huo Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu imepokea shilingi trilioni 1.9 sawa na 64% ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi trilioni 1.8 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naam.

**NAIBU SPIKA:** Twende kwenye uchambuzi wa mpango wa bajeti. *(Makofi)*

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mpango wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; ili kujiridhisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kamati ilipitia majukumu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na dira na dhima ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025; kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi milioni 87.6. Kiasi hiki ni sawa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024. Mchanganuo wa lengo hilo la makusanyo na sura ya mchanganuo wake

inaonekana katika Jedwali Na. 04. na Chati Na. 01 katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara hii ni sawa na lengo la Makusanyo liliowekwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 na mwaka huu wa fedha unaoishia yaani 2023/2024;

(ii) Fungu 38 - Ngome linategemewa katika makusanyo kwa kiasi cha 25%;

(iii) Fungu 39 - JKT linategemewa katika makusanyo kwa kiasi cha 74%; na

(iv) Fungu 57 - Wizara linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha 1.3%.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa miaka miwili mfululizo Wizara imeshindwa kukusanya maduhuli ya kiasi chochote. Hata hivyo, fungu hili pamoja na kushindwa kukusanya kwa kipindi tajwa hapo juu, bado kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeweka lengo la kukusanya shilingi milioni 1.2. Kamati haioni umuhimu wa kuweka makadirio haya wakati uhalisia lengo hili haliwezi kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa makusanyo kwa Fungu 39 ni mzuri, kwani katika mwaka wa fedha 2022/2023 fungu hili liliweza kufikia lengo la makusanyo. Tathmini inaonesha kuwa hata kwa mwaka wa fedha 2023/2024 fungu hili litafikia malengo ya makusanyo. Hata hivyo, Kamati inaona ipo haja ya kuongeza lengo la makusanyo kwa fungu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo Kamati inaamini kuwa Wizara kwa Fungu 38 na 39 imeweka lengo linalofikika, lakini Fungu 57 haliwezi kufikia lengo lililowekwa kwa fungu hilo, kwani fungu hilo halina chanzo cha maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi; maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa, katika mwaka wa fedha 2024/2025 bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliyoombwa kwa mafungu yote matatu ni shilingi trilioni 3.326. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 3.008 sawa na 90.4% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 317.4 sawa na 9.5% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi mantiki ya masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia kasma na mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa shilingi 336.2 ikilinganishwa na bajeti ya fedha 2023/2024. Tofauti hiyo ni ongezeko la 11.22%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kimeongezeka kwa shilingi 94.58 ambayo ni sawa na ongezeko la 42.4% ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Fedha hizo zimeongezeka katika Fungu 57 - Wizara kwa 62%. Aidha, fedha za maendeoleo kwa Fungu 38 - Ngome zimebaki kiasi sawa na kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 na Fungu 39 - JKT fedha za maendeleo zimepungua kwa 38%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya shilingi bilioni 317.4 zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo, 15.4% ni kwa ajili ya Fungu 38 - Ngome, asilimia 3 ni kwa ajili ya Fungu 39 - JKT na 81.1% ni kwa ajili ya Fungu 57 - Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo halitakuwa na mantiki iwapo Wizara ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye maoni na ushuri wa Kamati.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati; kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri utakaotolewa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati; moja, utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika Wizara hii kwa mtiririko uliopangwa ni jambo linapaswa kupewa kipaumbele stahiki ili kuendana na malengo yaliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, madeni ya takribani shilingi bilioni 1.9 ambayo Kampuni Tanzu ya Shirika la Mzinga linadai kwa Taasisi za Umma ikiwemo Halmashauri za Masasi, Bagamoyo, Mkalama na Chalinze, yanaathiri mtaji na uendeshaji wa Shirika hilo, imefikia wakati Wizara kuchukua hatua ili wadaiwa walipe madeni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa na mashine kwa ajili ya matumizi ya Jeshi vimekuwa vikitozwa kodi mbalimbali kwa mujibu wa sheria. Hali hiyo husababisha Jeshi kutumia fedha nyingi kulipa kodi wakati vifaa hivyo ni kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuondoa kodi katika vifaa vya jeshi itakuwa ni utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo inaondoa kodi katika vifaa vya jeshi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha utaratibu wa mchakato wa kutoza kodi unatoa fursa wa watu wasiohusika kukagua na kuona vifaa vya jeshi jambo ambalo tathimini ya kiusalama inaonesha siyo la afya katika medani za ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati kuhusu Sera ya Ulinzi wa Taifa; kwa zaidi ya miaka minne mfululizo sasa umefikia hatua ya kuhitaji kuwekwa katika utekelezaji. Hivyo ukamilishaji wa Sera ya Ulinzi wa Taifa ni jambo linalopaswa kupewa kipaumbele katika mwaka wa fedha wa 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka ya nchi yetu inavipenyo visivyo rasmi zaidi ya 1,000 ambayo inaweza kutumika vibaya na watu wasiyo na nia njema kwa nchi yetu ikiwemo kupitisha bidhaa haramu na za magendo. Kuimarisha mipaka yetu ili kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi ni suala linalopaswa kuendelea kupewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyumbu na Mzinga ni mashirika ya kimkakati, suala la kuyaboresha mashirika haya kwa mtaji, miundombinu, teknolojia na rasilimali watu linapaswa kupewa kipaumbele kimkakati. Hivyo fedha zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo kwa mashirika haya zitolewe kwa kuzingatia mipango iliyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ugunduzi wa bomu baridi la kufukuza tembo wanaovamia makazi ya watu uliyofanywa na Shirika la Mzinga ni jambo la kujivunia kwa nchi. Ni matumaini ya Kamati kuwa shirika hilo litaendelea kufanya tafiti za kimkakati kwenye nyanja za kijeshi pamoja na tafiti zinazolenga kutatua changamoto mbalimbali kwenye jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati; kutokana na maoni hayo kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili wa kibajeti wa miradi ya Wizara ili kupata tija iliyokusudiwa kwa masilahi mapana ya wananchi na Taifa kwa ujumla;

(ii) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 38 - Ngome kwa mtiririko uliyopangwa. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 57 - Wizara na Fungu 39 - JKT ili kutoathiri utekelezaji wa

shughuli zilizopangwa ikiwemo za Mashirika ya Nyumbu na Mzinga; na

(iii) Serikali ifanye mapitio ya sheria za kodi zinazotoza vifaa vya jeshi pamoja na mashine mbalimbali ili kuweka utaratibu wa kutoa msamaha wa kodi kwa vifaa vyote vinavyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya jeshi. Ushauri huu sasa umefikia hatua ya kutekelezwa kikamilifu na Serikali kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 Serikali ikamilishe upatikanaji wa Sera ya Taifa ya Ulinzi, pia Serikali iendelee kuchukua hatua za kimakakati na madhubuti kuimarisha miundombinu ya kiulinzi na kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi katiaka mipaka yetu. Kufanya hivyo kutawezesha kudhibiti vitendo visivyo na afya kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali itoe fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Mashirika ya Mzinga na Nyumbu ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa, kufanya hivyo itakuwa ni sehemu ya kuimarisha utendaji kazi wa mashirika hayo. Wizara iweke mikakati ya kusaidia kampuni tanzu ya Shirika la Mzinga kulipwa madeni yake ambayo inadai kwa taasisi za umma. Kulipwa kwa madeni hayo kutasaidia kuongeza mtaji na ufanisi wa kampuni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iendelee kutekeleza maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususani katika bajeti za miaka mitatu iliyopita ya mwaka 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii, naomba majina yao kama yalivyo katika taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na JKT Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax - Mbunge kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha namshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha niishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na likubali kuhidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FUNGU 38, 39, 59) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na

Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT, kujadailiwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika tarehe 25 Machi, 2024 baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117 (1) hadi 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda ya Taarifa hii, nitangulie kulikumbusha Bunge hili kuwa Wizara ya Ulinzi na JKT inajumuisha Mafungu Matatu (3) ya Kibajeti yafuatayo:-

a) Fungu 38 - Ngome;
b) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa; na
c) Fungu 57 – Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu sita (6) zifuatazo: -

Sehemu ya kwanza; ikiwa ni sehemu ya utangulizi; Sehemu hiyo inatoa maelezo ya jumla kuhusu msingi na muundo wa Taarifa. Sehemu ya Pili inafafanua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge. Na sehemu ya tatu hadi ya nne zinafanya

uchambuzi wa Utekelezaji wa mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na kuchanganua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya tano inaonesha Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na matokeo ya Uchambuzi. Aidha, sehemu ya sita na ya mwisho inakamilisha taarifa kwa kutoa shukurani na kulishauri Bunge kuhusu Hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## SURA YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Nyumba kwa ajili ya Makazi ya Washiriki wa Kozi za Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) Kunduchi-Dar es Salaam. Mradi huo ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili yafuatayo: -

a) Muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024; na
b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa Fedha ilizo ziidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

### 2.1 Muhtasari wa Maelezo kuhusu Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu mradi uliokaguliwa ni kama ifuatavyo: -

### 2.1.1 Mradi wa ujenzi wa Nyumba za Makazi kwa Washiriki wa Kozi za Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC)- Kunduchi-DSM

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ulinzi na JKT ilitengewa kiasi cha **Shilingi 10,809,103,955.82** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa majengo manne yenye Gorofa tatu kila moja kwa ajili ya Makazi Washiriki wa Kozi za Chuo cha NDC. Majengo hayo yanatambulika kama Jengo A, B, C na D. Kila Jengo linagharimu **Shilingi 2,702,275,988.95** Mradi huu unasimamiwa na SUMAJKT.

### 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makazi ya Wanafunzi NDC ulianza kujengwa tarehe 17 Aprili, 2023. Wakati wa ukaguzi Kamati ilielezwa kuwa Jengo A limefikia asilimia 99 na litakamilika tarehe 25 Machi, 2024 na Jengo B lilikuwa limefika Asilimia 58. Aidha, utekelezaji wa Jengo D na C bado haujaanza. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2024 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 4,677,459,012.00/=**; ambapo kiasi hicho kimetumika katika ujenzi wa Jengo A na B. Kamati iliridhishwa na hatua mradi ulipofikia pamoja na utekelezaji wake.

### 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni kuwa, Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ya Wizara hii kutokana na umuhimu wake.

## SURA YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ulilenga kulinganisha Makusanyo ya Mapato na lengo la Makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za Matumizi Mengineyo na upatikanaji wa fedha za Maendeleo ikilinganishwa na bajeti

iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kwa mafungu yote Matatu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Januari na Machi, 2024 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo: -

**3.1 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yanayopaswa kufanyiwa kazi na Wizara hii. Naomba kuliarifu Bunge lako kuwa, taarifa ya Mtoa Hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu ya ushauri kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii.

Mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupima, na Kupata Hati za maeneo yote ambayo hayajapimwa. Kamati imeridhishwa na namna Serikali ilivyozingatia na kutekeleza ushauri huu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uzingatiaji mzuri wa ushauri, upo ushauri ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kufanya mapitio ya Sheria za Kodi zinazotoza kodi vifaa vya Jeshi pamoja na Mashine mbalimbali ili kuweka utaratibu mzuri wa kutoa msamaha wa kodi kwa vifaa vyote vinavyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 3.2 Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara katika Kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024 kwa kuchambua hali ya ukusanyaji wa mapato pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

### 3.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kwa Mafungu yote matatu (3).

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 kiasi cha fedha za maduhuli kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa Shilingi **57,635,020.00** sawa na **asilimia 66** ya lengo la mwaka lililopangwa**.** Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa ni pungufu kwa **Shilingi 7,146,131.48** sawa na **asilimia 11** ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambayo yalikuwa **Shilingi 64,781,151.48**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa makusanyo hayo yamechangiwa na Mafungu mawili ya Wizara ambapo; Fungu 38 (Ngome) limekusanya **asilimia 20.5** na Fungu 39 (JKT) limekusanya **asilimia 79.5** ya kiasi kilichokusanywa.

Aidha, Fungu 57 (Wizara) hadi kufikia Mwezi Machi, 2024 halikuwa limekusanya kiasi chochote cha Fedha. Hali hii pia ni sawa na Mwaka wa fedha, 2022/2023 ambapo hadi kufikia Februari, 2023 Wizara haikuwa imekusanya kiasi chochote cha fedha.


**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 01** na **Grafu Na. 01** hapa chini.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Mapato**

| FUNGU | MAKADIRIO | MAKUSANYO | % YA JUMLA YA LENGO | % YA JUMLA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|
| 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 11,842,020.00 | 25 | 20.5 |
| 39 - JKT | 64,403,000.00 | 45,793,000.00 | 74 | 79.5 |
| 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 0.00 | 1.3 | 0.00 |

Chanzo: Randama ya Wizara 2024/2025


**Grafu Na. 1: Ulinganisho wa lengo na Makusanyo halisi ya Mapato**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2024/2025***

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa Makusanyo yaliyopatikana kwa kila Fungu kufikia Mwezi Februari, 2024 na Makusanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho katika Mwaka 2022/2023 kama inavyoonekana katika **Grafu na 2** hapa chini: -

**Grafu Na. 2: Ulinganisho wa Makusanyo 2022/2023 na 2023/2024**




| | 38-Ngome | 39-JKT | 57-WIZARA |
|---|---|---|---|
| 2022/2023 | 17,281,151.48 | 47,500,000.00 | - |
| 2023/2024 | 11,842,020.00 | 45,793,000.00 | - |

***Chanzo: Randama za Wizara 2022/2023 na 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kufanya Uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa: -

i) **Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 25** lakini katika utekelezaji Fungu hilo limechangia kwa **asilimia 20.5** ya kiasi kilichokusanywa.

ii) **Makusanyo ya Fungu 39 –JKT** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 74,** lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya JKT yamechangia kwa **asilimia 79.5** ya kiasi kilichokusanywa.

iii) **Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara**, yalikusudiwa kuchangia kwa **asilimia 1.3** kwenye mapato yote ya Wizara, lakini hali halisi imeonesha Wizara haijakusanya mapato yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa, umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo ni mzuri kwa fungu 39 pekee ambapo kufikia Mwezi Februari, 2024 lilikuwa limekusanya **asilimia 79.5**. Aidha, mwenendo wa Fungu 38 na 57 si mzuri. Kwani, Fungu 38 halijafanikiwa kufikia lengo kwani kufikia Februari, 2024 lilikuwa limekusanya **asilimia 20.5** ya Lengo.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 57 (Wizara) halikuweza kukusanya kiasi chochote hadi kufikia Mwezi Februari, 2024. Fungu hili pia halikuweza kukusanya kiasi chochote katika mwaka wa Fedha 2022/2023. kushindwa kukusanya kiasi chochote kwa muda wa miaka miwili mfululizo ni wazi kuwa makisio yanayowekwa hayana uhakika na hayakiisi uhalisia.

**3.2.2 Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2023/2024, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha Fedha kilichotolewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ililinganisha uwiano wa Bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekana katika **Jedwali Na. 02** na **03** hapa chini.

**Jedwali Na. 2: Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa kwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka 2023/2024 | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa | Fedha zilizopokelewa kufikia Februari, 2024 | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa |
|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 2,322,606,386,000 | 77.6 | 1,495,648,219,557.92 | 64 | 78 |
| 39 | 482,363,097,000 | 16.1 | 311,396,067,948.28 | 64 | 16.4 |
| 57 | 184,997,639,000 | 6 | 100,037,213,023.59 | 54 | 5.2 |
| **2,989,967,122,000** | | **100** | **1,907,081,500,529.79** | | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2024/2025***

**Jedwali Na. 3: Ulinganisho wa fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa na zilizopokelewa kwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka 2023/2024 | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa kiuwiano | Fedha zilizopokelewa kufikia Februari, 2024 | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa kiuwiano |
|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 48,867,636,000.00 | 22 | 9,345,336,244.00 | 19 | 10 |
| 39 | 13,965,535,000.00 | 6 | 5,321,845,000.00 | 38 | 5 |
| 57 | 160,000,000,000.00 | 72 | 83,212,378,401.66 | 52 | 85 |
| | **222,833,171,000.00** | **100** | **97,879,559,645.66** | 44 | **100** |

**Chanzo: Randama ya Wizara 2024/2025**

Kupitia uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

i) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu imepokea **Shilingi 1,907,081,500,529.79** sawa na **asilimia 64** ya fedha zilizoidhinishwa.

ii) Kati ya fedha zilizopokelewa **Shilingi 1,809,201,940,884.13** sawa na asilimia **95** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 97,879,559,645.79** sawa na **asilimia 5** ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

iii) Kati ya fedha zilizopokelewa; Fungu 38 (Ngome) limepokea **asilimia 78,** Fungu 39 (JKT) limepokea **asilimia 16.4** na Fungu 57 (Wizara) limepokea **asilimia 5.2.**

iv) Kiasi cha fedha kilichopokelewa na Wizara hii kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kimeongezeka kwa **Shilingi 4,882,845,216.75** sawa na **asilimia 5** ikilinganishwa na **Shilingi**

**92,996,714,428.91** zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2022/2023.

v) Kati ya **Shilingi 97,879,559,645.79 zilizopokelewa** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, **asilimia 10** ni kwa ajili ya Fungu 38 (Ngome), **asilimia 5** ni kwa ajili ya Fungu 39 (JKT) na **asilimia 85** ni kwa ajili ya Fungu 57 (Wizara).

vi) Katika Fedha zilizoidhinishwa kwa kila Fungu kwa ajili ya miradi ya maendeleo, Fungu 38 (Ngome) limepokea **Shilingi 9,345,336,244.00** sawa na **asilimia 19** ya **Shilingi 48,867,636,000.00** zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Fungu hilo.

vii) Fungu 39 (JKT) lilipokea **Shilingi 5,321,845,000.00** sawa na **asilimia 38** ya **Shilingi 13,965,535,000** zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Fungu hilo;

viii) Fungu 57 (Wizara) limepokea **Shilingi 83,212,378,401.66** sawa na **asilimia 52** ya **Shilingi 160,000,000,000** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Fungu hilo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo unaonesha kuwa Serikali ilizingatia uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii. Mathalani, Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 (Ngome) ikiwa ni **asilimia 77.6** ya Bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo ni **asilimia 78** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia Mwezi Februari, 2024;

Fungu 39 liliidhinishiwa **asilimia 16.1** ya bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo hadi kufikia Februari, 2024 ni **asilimia 16.4** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara; na

Fungu 57 ilitengewa **asilimia 6** ya bajeti yote ya Wizara, hadi kufikia Februari 2024 ilikuwa imepokea **asilimia 5.4** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mtiririko huo mzuri wa upatikanaji wa fedha, Kamati haijaridhishwa na mtiririko wa fedha za maendeleo kwa Mafungu yote ya Wizara hii ambapo hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 Fungu 38 (Ngome) lilikuwa limepokea **asilimia 19** ya fedha zilizoidhinishwa**,** Fungu 39 (JKT) lilikuwa limepokea **asilimia 38** ya fedha zilizoidhinishwa na Fungu 57 (Wizara) lilikuwa limepokea **asilimia 52** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa ujumla kati ya **Shilingi 222,833,171,000** zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Wizara hii; hadi Mwezi Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 44** sawa na **Shilingi 97,879,559,645.66**

**Mheshimiwa Spika,** kutokutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati katika Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kiasi kikubwa kunaathiri mipango ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara ikiwemo miradi ya Mashirika ya Kimkakati ya MZINGA na NYUMBU.

## SURA YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA BAJETI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na Kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na Dira na Dhima ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu Sita likiwemo kuliongezea uwezo wa kimedani Jeshi la ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia vifaa vya kisasa na zana bora; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma, Kuwapa Viijana wa kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa

kitaifa na uwezo wa kujitegemea, kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya Kijeshi na kiraia, kuendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Akiba na kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine katika Nyanja za kijeshi na kiulinzi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, majukumu yaliyopangwa yatawezesha kufikiwa kwa malengo sita (6) ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia mpango kazi uliowekwa.

### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu (38, 39 na 57) inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 87,603,000.** Kiasi hiki ni sawa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 na
2023/2024.


Mchanganuo wa lengo hilo la Makusanyo na Sura ya mchanganuo wake inaonekana katika **Jedwali Na. 04.** na **Chati Na. 01** hapa chini: -

**Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka 2024/2025**

| Fungu | Makadirio | Asilimia ya lengo la Wizara |
|---|---:|---:|
| Fungu 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 25 |
| Fungu 39 - JKT | 64,403,000.00 | 74 |
| Fungu 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 1.3 |
| **JUMLA** | **87,603,000.00** | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2024/2025***

**Chati Na. 1: Mchanganuo wa asilimia ya Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka 2024/2025**




Chanzo: Randama ya Wizara 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara hii ni sawa na lengo la Makusanyo liliowekwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 na mwaka huu wa fedha unaoishia yaani 2023/2024;

ii) Fungu 38 (Ngome) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 25;**

iii) Fungu 39 (JKT) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 74;** na

iv) Fungu 57 (Wizara) linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 1.3.**

v) Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa miaka miwili mfululizo Wizara (Fungu 57) limeshindwa kukusanya maduhuli ya kiasi chochote. Hata hivyo Fungu hili pamoja na kushindwa kukusanya kwa kipindi tajwa hapo juu bado kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imewekewa lengo la kukusanya **Shilingi 1,200,000/=.** Kamati haioni umuhimu wa kuweka makadirio haya wakati kiuhalisia lengo hili haliwezi kufikiwa.

vi) Mwenendo wa makusanyo kwa Fungu 39 ni mzuri kwani katika mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu hili liliweza kufikia lengo la makusanyo. Tathmini inaonesha kuwa hata kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu hili litafikia malengo ya makusanyo. Hivyo Kamati inaona ipo haja ya kuongeza lengo la makusanyo kwa Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, Kamati inaamini kuwa Wizara kwa Fungu 38 na 39 imeweka lengo linalofikika. Lakini Fungu 57 haliwezi kufikia lengo lililowekwa kwa kuwa Fungu hilo halina chanzo cha maduhuli.

**4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote matatu ni **Shilingi 3,326,230,418,800.00/=.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,008,812,906,800** sawa na **asilimia 90.4** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 317,417,512,000.00** sawa na **asilimia 9.5** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mantiki ya Masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma *(Items)*, Vifungu *(Subvotes)* na Mafungu *(Votes)* yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

i) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **Shilingi 336,263,296,800** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Tofauti hiyo ni ongezeko la **asilimia 11.2**;

ii) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kimeongezeka kwa **Shilingi 94,584,341,000** ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 42.4** ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Fedha hizo zimeongezeka katika Fungu 57 (Wizara) kwa **asilimia 62**. Aidha, fedha za maendeoleo kwa Fungu 38 (Ngome) zimebaki kiasi sawa na kilichotengwa

katika mwaka wa fedha 2023/2024, na Fungu 39 (JKT) fedha za maendeleo zimepungua kwa **asilimia 38;**

iii) Kati ya Shilingi **317,417,512,000.00** zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, **asilimia 15.4** ni kwa ajili ya Fungu 38 - Ngome, **asilimia 3** ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT na **asilimia 81.1** ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara;

iv) Ongezeko la fedha za miradi ya maenedeleo halitakuwa na mantiki iwapo Wizara haitahakikisha kuwa Mafungu yote yanakamilisha taratibu za awali za kuomba fedha kwa wakati na kwamba HAZINA itatoa fedha zinazohusika kama inavyostahili;

v) Makadirio ya matumizi ya aina zote katika Wizara hii yamezingatia umuhimu wa kufanikisha uimarishaji wa hali ya ulinzi na usalama ikiwemo mipaka ya nchi;

vi) Makadirio ya matumizi yaliyowasilishwa yasipopitishwa na Bunge kwa kiasi hicho au kwa nyongeza zaidi, majukumu ya Wizara hii yatakuwa mashakani na shughuli za umma kwa ujumla nchini zitaingia matatani.

## SURA YA TANO

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri utakaotolewa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

### 5.1 Maoni ya Kamati

i) Utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika Wizara hii kwa mtiririko uliopangwa ni jambo linapaswa kupewa kipaumbele stahili ili kuendana na malengo yaliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha kwa ajili hiyo.

ii) Madeni ya takribani Shilingi Bilioni 1.9 ambayo Kampuni Tanzu ya Shirika la Mzinga linadai kwa taasisi za umma ikiwemo Halmashauri za Masasi, Bagamoyo Mkalama na Chalinze

yanaathiri mtaji na uendeshaji wa Shirika hilo. Imefikia wakati Wizara kuchukua hatua ili wadaiwa walipe madeni hayo.

iii) Vifaa na mashine kwa ajili ya matumizi ya Jeshi vimekuwa vikitozwa Kodi mbalimbali kwa mujibu wa Sheria. Hali hiyo husababisha Jeshi kutumia fedha nyingi kulipa kodi wakati vifaa hivyo ni kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi na kwa matumizi ya Jeshi katika kutekeleza majukumu yake ya muhimu ya ulinzi wa Taifa. Kuondoa kodi katika Vifaa vya Jeshi itakuwa ni utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Customs Management Act No. 147 R.E 2019*) ambayo inaondoa kodi katika vifaa vya Jeshi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

iv) Aidha, utaratibu na mchakato wa kutoza kodi unatoa fursa wa watu wasio husika kukagua na kuona vifaa vya Jeshi jambo ambalo tathmini ya kiusalama inaonesha si la afya katika medani za ulinzi na usalama.

v) Ushauri wa Kamati kuhusu Sera ya Ulinzi wa Taifa kwa zaidi ya miaka 4 mfululizo sasa umefikia hatua ya kuhitaji kuwekwa katika utekelezaji. Hivyo, Ukamilishaji wa Sera ya Ulinzi wa Taifa ni jambo linalopaswa kupewa kipaumbele katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

vi) Mipaka ya nchi yetu ina vipenyo visivyo rasmi zaidi ya 1000 ambayo inaweza kutumika vibaya na watu wasio na nia njema kwa nchi yetu ikiwemo kupitisha bidhaa haramu na za magendo. Kuimarisha Mipaka yetu ili kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi ni suala linalopaswa kuendelea kupewa kipaumbele.

vii) NYUMBU na MZINGA ni mashirika ya kimkakati. Suala la kuyaboresha mashirika haya kwa mtaji, miundombinu, teknolojia na rasilimali watu linapaswa kupewa kipaumbele kimkakati. Hivyo, fedha zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo kwa mashirika haya ni muhimu zikatolewa kwa kuzingatia mipango iliyowekwa.

viii) Ugunduzi wa Bomu baridi la Kufukuza Tembo wanaovamia makazi ya watu uliofanywa na Shirika la MZINGA ni jambo lakujivunia kwa nchi. Ni matuamaini ya Kamati kuwa Shirika hilo litaendele kufanya tafiti za kimkakati kwenye Nyanja za kijeshi pamoja na tafiti zinazolenga kutatua changamoto mbalimbali kwenye jamiii.

### 5.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na maoni hayo, Kamati inashauri yafuatayo: -

i) Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili wa kibajeti miradi ya Wizara ili kupata tija iliyokusudiwa kwa maslahi mapana ya wananchi na na Taifa kwa ujumla.

ii) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 38 - Ngome kwa mtiririko uliopangwa. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 57 - Wizara na Fungu 39 (JKT) ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ikiwemo za Mashirika ya NYUMBU na MZINGA.

iii) Serikali ifanye mapitio ya Sheria za Kodi zinazotoza kodi vifaa vya Jeshi pamoja na Mashine mbalimbali ili kuweka utaratibu mzuri wa kutoa msamaha wa kodi kwa vifaa vyote vinavyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi. Ushauri huu sasa umefikia hatua ya kutekelezwa kikamilifu na Serikali kwa maslahi mapana ya Taifa.

iv) Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali ikamilishe upatikanaji wa Sera ya Taifa ya Ulinzi (*The National Defence Policy*).

v) Serikali iendelee kuchukua hatua za kimkakati na madhubuti kuimarisha miundombinu ya kiulinzi na kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi katika mipaka yetu. Kufanya hivyo kutawezesha kudhibiti vitendo visivyo na afya kwa Taifa.

vi) MZINGA na NYUMBU ni mashirika ya kimkakati katika sekta ya ulinzi na usalama. Uimarishaji na uboreshaji wa Masharika haya ni suala la kupewa kipaumbele stahili. Hivyo basi, Serikali itoe fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendelo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa mashirika haya ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa. Kufanya hivyo itakuwa ni sehemu ya kutaimarisha utendaji kazi wa Mashirika hayo.

vii) Wizara iweke mikakati ya kuisadia Kampuni Tanzu ya Shirika la MZINGA kulipwa madeni yake ambayo inadai kwa taasisi za umma. Kulipwa kwa madeni hayo kutasaidia kuongeza mtaji na ufanisi wa Kampuni hiyo.

viii) Wizara iendelee kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024.

## SURA YA SITA

### 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard): -

1. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Cosato David Chumi, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Dr. Alfred James Kimea, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb - Mjumbe

11. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Minza Simon Mjika, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Maimuna Salum Mtanda, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Stagomena Lawrence Tax (Mb) kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, niishukuru Sekretariat ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono Hoja na naomba kuwasilisha.

**Vita Rashid Kawawa, Mb**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

20 Mei, 2024

*Kiambatisho Na. 1*

**UTELEKEZAJI WA MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA (NUU) KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2023/2024**

| NA. | USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili wa kibajeti miradi ya Wizara ili kupata tija inayokusudiwa kwa maslahi mapana ya wananchi na taifa kwa ujumla. | Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Ulinzi na JKT. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Fungu 57 – Wizara liliidhinishiwa **Shilingi bilioni 140**, Fungu 38 – NGOME liliidhinishiwa **Shilingi bilioni 32.6** na Fungu 39 – JKT liliidhinishiwa **Shilingi bilioni 4** kwa ajili ya shughuli za maendeleo.<br>Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023,<br>Fungu 57 – Wizara iliidhinishiwa **Shilingi bilioni 160** ambayo ni ongezeko la **asilimia 14.28**, Fungu 38 – NGOME liliidhinishiwa **Shilingi bilioni 56.6** ambayo ni ongezeko la **asilimia 73.62** na Fungu 39 – JKT liliidhinishiwa **Shilingi bilioni 13.7** ambayo ni ongezeko la **asilimia 242.5.** |
| 2. | Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 38 – NGOME kwa mtiririko uliopangwa. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 57 – Wizara na Fungu 39 – JKT ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli | Serikali imeendelea kutoa fedha za maendeleo katika mafungu yake yote matatu katika Wizara ya Ulinzi na JKT kugharamia miradi ya maendeleo. Katika Mwaka wa fedha 2022/23 Wizara ilitenga **Shilingi 230,333,171,000.00** na kiasi kilichopokelewa ni **Shilingi 125,279,918,014.21** sawa na |

| | | |
|---|---|---|
| | zilizopangwa. | **asilimia 54.39** . Kati ya fedha hizo, 57 – Wizara limepokea **Shilingi 83,415,939,641.95** sawa na **asilimia 52.13**, Fungu 38 – NGOME limepokea **Shilingi 31,363,978,372.26** sawa na **asilimia 55.64**, na Fungu 39 JKT limepokea **Shilingi 10,500,000,000.00** sawa na **asilimia 75.19**.<br>Aidha, Katika Mwaka wa fedha 2023/24 Wizara ilitenga **Shilingi 222,833,171,000.00** na kiasi kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Februari 2024 ni **Shilingi 97,879,559,645.66** sawa na **silimia 43.93**. Kati ya fedha hizo, Fungu 57 – Wizara limepokea **Shilingi 83,212,378,401.66** sawa na **asilimia 52.01**, Fungu 38 – NGOME limepokea **Shilingi 9,345,336,244.00** sawa na **asilimia 19.12**, na Fungu 39 JKT limepokea **Shilingi 5,321,845,000.00** sawa na **asilimia 38.11**<br><br>Wizara inaendelea kuwasiliana kwa karibu na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa fedha zinazoidhinishwa zinapatikana kwa mtiririko mzuri kama ilivyopangwa. |
| 3. | Mamlaka ya Mapato (TRA) pamoja na mamlaka nyingine zinazohusika ziidhinishe maombi ya Jeshi kutumia *Bonded Warehouse* zake. Kufanya hivyo kutasaidia Jeshi kupunguza muda wa mizigo yake kukaa | Mchakato wa Jeshi kuwa na *Bonded Warehouse* ulianza, lakini TRA na Mamlaka husika zilitoa vigezo ambavyo Jeshi halikuweza kuvifikia. Vigezo hivyo ni pamoja na mashine za kupakua/kupakia mizigo, eneo kuwa na uzio, |

| | | |
|---|---|---|
| | kuepuka gharama kubwa inazotumia kuhifadhi mizigo bandarini (Demurrage charges na storage charges) | uwepo wa vyumba vya ofisi, na malipo ya Bima kwa mizigo. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia NGOME imeanza upya mchakato wa kuwa na '***Bonded Warehouse***' kwa kutafuta fedha ili kufanikisha ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vitendea kazi husika. |
| 4. | Serikali ifanye mapitio ya sheria za kodi zinazotoza vifaa vya Jeshi ili kuweka utaratibu mzuri wa kutoa msamaha kwa vifaa vyote vinavyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi kuliko utaratibu uliopo sasa. | Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na JKT imeanza kuchukua hatua ya kuhakikisha kunakuwa na utaratibu mzuri wa kutoa msamaha kwa vifaa vyote vinavyoingizwa nchini kwa matumizi ya Jeshi. Hatua hizo ni pamoja na kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kufanya mapitio ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani na Sheria ya Fedha. Hatua hii itaendana pia na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Customs Management Act No. 147 R.E 2019*) inayoelekeza kuwa vifaa vyote vinavyoingizwa nchini kwa matumizi ya Jeshi visitozwe kodi. Aidha, Wizara iliwasilisha mapendekezo ya kurekebisha Sheria za Kodi katika Tume ya Kurekebisha Sheria, ili kutoa msamaha kwa vifaa vyote vinavyoingizwa nchini kwa matumizi ya Jeshi. |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali ikamilishe upatikanaji wa Sera ya Taifa ya Ulinzi (The National Defence Policy) kwa umuhimu wake kwa Taifa kama ambavyo imekuwa ikishauriwa vipindi tofauti tangu Bunge la Tisa. | Kazi ya kuandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ulinzi inaendelea vizuri. Kwa sasa, Wizara inafanya Tathmini ya Hali ya Ulinzi, ambayo ni muhimu katika kuandaa Sera ya Taifa ya Ulinzi. Tathmini hii inatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. |
| 6. | Serikali iendelee kuchukua hatua madhubuti kuimarisha miundombinu ya kiulinzi na kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi katika mipaka yetu. Kufanya hivyo kutawezesha kudhibiti vitendo visivyo na afya kwa Taifa. | Wizara ya Ulinzi na JKT imeendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhakikisha kuwa barabara na alama za mipaka zinaendelea kuimarishwa. Vilevile, JWTZ imeendelea kuimarisha viteule vilivyopo mipakani na kuviwezesha kufanya doria za mara kwa mara. Aidha, Wizara kupitia JWTZ imefanya tathmini ya kusimika mifumo ya ulinzi wa mipaka katika Mpaka wa Kusini ili kudhibiti mianya isiyo rasmi na vitendo visivyo na afya kwa Taifa. |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Wizara iongeze kasi ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupima, na Kupata Hati za maeneo yote ambayo hayajapimwa. Kufanya hivyo, kutawezesha maeneo ya Wizara kutambulika rasmi na hivyo kuepuka migogoro isiyo na lazima na wananchi. | Wizara inatekeleza Mpango wa kuhakikisha maeneo yote ya Jeshi yanapimwa na kupatiwa hati miliki ili kuondoa migogoro iliyopo. Hadi sasa, Mpango huo umetekelezwa kwa **asilimia 71.5** kwa kuhakiki, kupima na kufanya uthamini wa maeneo mbalimbali ya Jeshi nchini na jumla ya **Shilingi bilioni 29.624** zimetumika kulipa fidia kwa wananchi. Mkakati umejumuisha maeneo ya Jeshi yaliyopo Tanzania Bara na Zanzibar. |
| 8. | Uimarishaji wa Mashirika ya Mzinga na Nyumbu uende sambamba na kuongeza rasilimaliwatu kwa kuzingatia mahitaji ya mashirika hayo. Kufanya hivyo, kutaimarisha utendaji kazi wa Mashirika hayo na hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa. | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kufanya mawasiliano na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu kujazwa kwa nafasi zilizo wazi katika Mashirika. Aidha, katika kipindi ambacho Wizara inasubiri kupatiwa watumishi hao, imeendelea kutumia watumishi waliopo pamoja na Maafisa na Askari wa JWTZ. Vilevile, Wizara imeendelea kuongeza juhudi kuhakikisha mashirika yanaimarika kiutendaji. |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Wizara iendelee kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023. | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa, hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023. |

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliyopo Bungeni asubuhi hii, wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax, Waziri wa Ulinzi, ambao ni viongozi na watendaji wa Wizara ya Ulinzi Makao Makuu ya Jeshi, Makao Makuu ya JKT na Mashirika yaliyopo chini ya Wizara. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi nane kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro wakiongozwa na Abdulijalil Amri Kishama, karibuni. *(Makofi)*

Viongozi wa *TUGHE* Tawi la Ulinzi wakiongozwa na Bwana Markus K. Nyanda. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Venant Daud, Katibu wa CCM Wilaya ya Singida Mjini, Mkoani Singida. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni wanafunzi 50 na walimu kumi wa shule ya awali ya msingi ya *St. Marks*. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaanza mjadala tunaanza na Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, ajiandae Mheshimiwa Bupe, ajiandae Mheshimiwa Vincent.

**MHE. MAULID SALEH ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia uhai na afya njema ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendeleza vyema vyombo vyetu hivi vya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Vilevile nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Stergomena Lawrence Tax, kwa kazi nzuri anayofanya akishirikiana na Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika lakini vilevile nimpongeze sana Mkuu wa Majeshi - Jenerali John Mkunda na nimpongeze msaidizi wake, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi - Luteni Jenerali Othman. Vilevile niwapongeze Makamanda, Wakuu wa Kamandi wote, maafisa wakubwa na maafisa wadogo wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia na nitachangia mambo mawili; jambo la kwanza, kuhusu upatikanaji wa fedha za maendeleo katika jeshi letu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika jeshi letu linafanya kazi kubwa na nzuri sana ya kulinda mipaka yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha za maendeleo ya jeshi letu hili lililopo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kiukweli fedha walizopokea ni kidogo sana...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge masuala ya pesa zote mwisho wa bajeti ya Serikali ni mwezi wa sita na hoja zote za mapato na maingizo ya pesa kwenye Wizara zipo kwenye Kamati ya Bajeti, naomba uchangie maeneo mengine, masuala yote ya pesa zitalipwa na zipo kwenye Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

**MHE. MAULID SALEH ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, saw ana nikushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe Serikali ipeleke fedha kwa wakati ili watekeleze majukumu yao kwa muda waliyojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kuna madeni, niiombe Serikali iweke mpango mkakati wa kuyafuatilia madeni haya ili iweze kuyalipa kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilipongeze Shirika la Mzinga kwa uvumbuzi wa bomu hili baridi la kufukuza tembo. Tembo hawa wamekuwa wakiathiri sana uchumi wa maendeleo katika nchi yetu, lakini niipongeze tena Serikali hususani shirika hili kwa ubunifu wao na umahiri wao wa kuweza kuleta teknolojia hii ambayo nchi yetu itanufaika kwa maendeleo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali hasa Wizara ya Fedha kuwa na mpango mzuri wa kupeleka fedha kwa wakati ili mashirika yetu haya yaweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana watendaji wote wa Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Ulinzi la Kujenga Taifa na nimpongeze sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa umahiri wake na umakini wake wa kuweza kuwa nchi yetu ipo salama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bupe, ajiandae Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja yetu iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima lakini nichukue nafasi hii kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu, Rais wetu, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuviendeleza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kuiongoza vizuri Wizara hii nyeti ya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Katibu Mkuu Kaka yangu Mnyeti kwa kazi nzuri, lakini pia niendelee kuvipongeza vyombo vyetu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa tamka jina vizuri la Katibu Mkuu.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kaka yangu Mnyepe, Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kupongeza vyombo vyetu vya Ulinzi kwa ujumla Jeshi letu la ulinzi linafanya kazi nzuri sana, mipaka yetu yote ipo imara, Watanzania wote tunaamani na bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, tumeweza kutembelea nchi za wenzetu ambazo wana migogoro kwa kweli wanashinda, sisi Watanzania tunaamani kwa sababu Jeshi letu la Ulinzi lipo imara na linafanyakazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu muda wote wanawake ni kubeba mizigo, hekaheka, lakini sisi Watanzania tunalala usingizi, tunafanya mambo yetu kwa uhuru na amani kwa sababu vyombo vyetu vya ulinzi vipo imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze *CDF* - Mkuu wa Majeshi, nimpongeze Mnadhimu Mkuu kaka yangu Othman, niwapongeze maofisa wote na wakuu wote wa Kamandi wanafanya kazi nzuri sana katika nchi yetu hii, nchi yetu tunaamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie sasa kwenye suala la JKT; nimpongeze sana pia kaka yangu Meja Jenerali Rajabu Mabele, anafanya kazi nzuri sana, vijana wetu wote sasa hivi kimbilio lao wanatamani sana waingie JKT. JKT inafanya kazi nzuri sana tukiimarisha sana JKT itafanya vizuri kwa sababu vijana wetu

wengi watapunguza mambo ya ushoga, wakienda kujiunga na JKT watakuwa imara na nchi yetu itakuwa na vijana imara wanaoweza kujitegemea hata pasipo kuajiriwa. Kwa hiyo nipongeze sana jeshi letu la JKT linafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kupongeza Shirika letu la Mzinga na nimpongeze pia Brigedia Hamis, amefanya kazi nzuri sana ya ugudunzi wa bomu baridi la kufukuza tembo, lakini pia kufukizia wanyama wakali. Wote hapa Wabunge tulikuwa na kilio cha tembo, tembo walikuwa wanaleta maafa mazito katika nchi yetu, lakini shirika hili wameweza kugundua silaha baridi ya kuweza kuwafukuza tembo hawa bila kuwaua, hongera sana Mzinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa natamani sana Mzinga hao wanafanya shughuli zao za kujipatia kipato katika shirika lao, lakini hawalipwi, naomba taasisi zile za umma ambazo zimefanya kazi na Shirika la Mzinga, wanaodaiwa waweze kuwalipa Shirika la Mzinga. Nimeona kuna deni hapa takribani shilingi bilioni 1.9 ambazo hawajalipwa watu wa Mzinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hizi taasisi ziweze kuwalipa haraka sana, hawa watu wanafanya kazi nzuri hawalali kwa ajili yetu kwa nini tuwacheleweshee pesa zao. Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapo...

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwongezea taarifa mzungumzaji anayezungumza kwa sasa kwamba Shirika la Mzinga kwa kweli ni shirika ambalo linafanya kazi nzuri sana, kwa kugundua bomu hilo la machozi baridi tunaomba lisambazwe nchi nzima, halmashauri zote zinunue ambazo zinasumburiwa na tembo ili mambo yaweze kwenda vizuri. Tunawashukuru sana kwa uvumbuzi wao, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bupe muda wako umekwisha.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo jiandae, Mheshimiwa Ahmed Ally.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naipokea taarifa na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo, ajiandae Mheshimiwa Ahmed Ally.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi na timu yote ya Wizara ya Ulinzi kwa bajeti nzuri waliyoileta ndani ya Bunge na naomba Wabunge wote tuipitishe ili jeshi liweze kufanya kazi kwa bidii. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa sababu tunaona anaendelea kuviboresha vyombo vya ulinzi na usalama hasa jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa mipakani na hasa katika maziwa, mfano Ziwa Tanganyika, upande wa Ziwa Tanganyika ndiyo kuna lango kuu kubwa sana la uhalifu kwa sababu lipo mipakani na nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Rukwa hasa wavuvi mikoa hii mitatu Kigoma, Katavi na Rukwa wana changamoto kubwa sana ya wahalifu wanaotoka nchi jirani, wanapoenda kufanya shughuli zao za uvuvi, wanavamiwa wananyang'anywa nyavu zao na zana za uvuvi na pengine kuvuka kabisa kuja upande wetu na kunyang'anywa mali zao na fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Wizara ya Ulinzi pamoja na Mheshimiwa Waziri na timu yote. Mimi kama Mbunge

na mwakilishi wao natokea ukanda wa Ziwa Tanganyika niliandika barua ya maombi kuwaomba ili waweze kuja kujenga Kambi ya Jeshi ukanda wa Ziwa Tanganyika. Hatua hii imechukuliwa kwa haraka, wameshatuma timu ya wataalamu, wamekuja kuainisha eneo la Tarafa ya Wampembe, Kata ya Kizumbi, tayari eneo limeshapatikana. Kwa hiyo, niombe Wizara ipewe fedha ili kambi hii ikishajengwa wavuvi na wananchi wa ukanda wa Ziwa Tanganyika wamepokea kwa raha sana na wanampongeza Mheshimiwa Rais, kwa sababu hawana hofu tena ya uvamizi *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kambi hii ikijengwa wavuvi wanaofanya shughuli za kiuchumi watafanya kazi bila hofu na maendeleo yatakuwepo, kwa sababu kutakuwa ulinzi ndani ya Ziwa Tanganyika. Kambi ikijengwa itakuwa inafanya kazi ya *intelligence gathering* ndani ya ziwa na kutoa elimu katika ukanda wa Ziwa Tanganyika hasa kwa wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi za JKT; sasa hivi tunaona kuna mwamko na mwitikio mkubwa sana wa vijana wetu kujiunga na Kambi za JKT. Kambi za JKT zilizopo ni chache. Tunaomba Wizara ipewe fedha ili vijana wetu waende wakapewe elimu ya uzalendo ili wawe na mapenzi na nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamechangia kuhusu bomu la kufukuza tembo, niiombe Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa iweke ushirikiano na Jeshi letu lililovumbua bomu la tembo, ili pale mara inapotokea changamoto ya tembo kuvamia makazi ya watu, Jeshi la Ulinzi pamoja na Wizara ya Maliasili kwa pamoja waende kwa haraka ili kuweza kutatua changamoto hiyo kwa haraka ili wananchi waendelee kufanya kazi zao kwa amani na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ya jeshi wamesema tunaona kuna changamoto; niiombe Wizara ipewe fedha maeneo yote ili yapate hati kamili ili maeneo ya jeshi yasivamiwe, yawe na hati kamili ili kuondoa migogoro kati ya wananchi na wanajeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, ajiandae Mheshimiwa Nahodha.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kwanza kabisa ninaunga mkono hoja bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Amiri Jeshi Mkuu kwa namna anavyofanya kazi kubwa hasa kulinda na kulishughulikia jeshi letu na kuhakikisha kabisa kwamba, nchi yetu inakuwa na amani muda wote saa 24, siku saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Waziri Mheshimiwa Dkt. Stergomena kwa kazi nzuri anayoifanya, nimpongeze pia Katibu Mkuu ndugu yangu Dkt. Faraji, niwapongeze wote wakiongozwa na *CDF* Jenerali Mkunda, Mnadhimu Mkuu Luteni Jenerali Salum Othman, *Major Generals* wote pamoja na ma-*CDF* wastaafu, nimemwona pale ndugu yangu Jenerali Mstaafu Mabeyo, wote kwa pamoja wanafanya kazi. Jenerali Mabeyo alifanya kazi kubwa sana wakati ule ameliweka jeshi vizuri sana. Vilevile nimpongeze na niendelee kumpa moyo *CDF* Mkunda, kwa kazi kubwa anayoifanya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza muda wake pale ameongelea masuala mazima ya mpakani. Nchi yetu ina historia kubwa sana kutoka wakati wa Awamu ya Kwanza ya Mheshimiwa Rais wetu Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere. Kwa wakati ule nchi yetu ilikuwa katika ile hali ya kukomboa nchi nyingi za Afrika ikiwemo Msumbiji, Zimbabwe na kazi yote hiyo ilifanywa na jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya vijana wa jeshi *by then* tulikwenda *physically* kabisa kuwasaidia nchi hizo kupata uhuru, lakini hali ile imekwenda na sasa hivi nchi zote zimepata

uhuru tulizozikusudia zipate uhuru kwa wakati ule Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini *operation* zinaendelea mpaka sasa hivi? Kwanza kabisa tumshukuru Mungu kwa neema hii ya amani ambayo tunayo sasa hivi. Tunamshukuru sana hii ni zawadi tu kwa Mungu kwamba nchi ya Tanzania iwe ya amani. Nchi za jirani zinapokuwa hazina amani inakuwa ni kimbilio kuja kwetu kwa maana kutaka amani ama kwa mazungumzo au hata kutuma vijana wetu wa jeshi kwenda kulinda amani kama ambavyo inafanya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi vijana wetu wapo kwenye mpaka hapo Mtwara na Msumbiji, vijana wapo Congo, vijana wapo Afrika ya Kati, vijana wapo wanafanya kazi kubwa mno, hii yote ni kwamba, tulinde amani kule tuwasaidie ili chochoko zile zisije zikaleta tashwishi katika nchi yetu hii nzuri ambayo Mungu ametusaidia mpaka hivi sasa kuwa nchi ya amani katika Afrika namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hizi *operation* zinazofanywa ni kazi kubwa, vijana wanafanya kazi kubwa sana. Mimi nishauri tu kwamba katika bajeti waliyopanga Mheshimiwa Waziri ahakikishe kabisa fedha hizi kwa ajili ya *operation* zinapatikana kwa wakati muda wowote na kwa uharaka ule ule unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana ya kwamba inaweza ikatokea jambo sasa hivi tu la haraka na la za dharura sasa fedha zinapochelewa ili kwenda kuwahudumia hawa kwa maana ya kununua mitambo, kuwapa maslahi yao waweze kwenda kwa haraka inakuwa siyo jambo zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhakikishe kabisa kwamba fedha zinakuwa kwa wakati wote, muda wote na nimesoma bajeti yake Mheshimiwa Waziri, kuna asilimia *almost 21* fedha hazijakamilika kwa maana kuanzia mwezi Aprili, lakini toka mwezi Aprili mpaka tunapoenda kumaliza bajeti hii mwezi Aprili, ahakikishe basi hii 21% ya bajeti tuliyopitisha mwaka jana wanaipata jeshi hili ili waendelee kufanya majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi majeshi yote duniani yanakwenda kidigitali, tutoke huku tulipo sasa hivi. Mimi naamini kabisa sina mashaka na wanajeshi, sina mashaka na *CDF* na sina mashaka kabisa na wanajeshi, wapo wataalamu wazuri sana na waliobobea na ni wazalendo kwa muda wowote. Ukiwatuma wakati wowote wanakwenda kufanya kazi nzuri kabisa ya kulinda nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zana ambazo tunazo kama itampendeza na ninafikiri wakikaa kama kikao, tutoke kwenye zana hizi twende kwenye zana za kisasa. Zana za kisasa ni pamoja na zana ambazo sasa hivi utaona wanajeshi wanatumia zana chache tu wanakaa hivi, vitu vinakwenda kule kulinda nchi yetu. Kuliko kutumia zana za zamani ambazo zinakuwa na gharama kubwa au kazi kubwa kabisa ya kufanya *mobilization* na mitambo ile au zana zile kwenda kwenye eneo ambalo tumekusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona jeshi upande mwingine inapotokea janga lolote au dharura tunakwenda kuomba wanajeshi ili watusaidie. Tumeona pale Manyara, tumeona pale Kusini barabara imekatika na tumeona maeneo mengi tu, lakini kitengo hiki ni muhimu sana kwa maslahi ya Taifa letu. Hiki kitengo tunakisaidiaje? Kwa maana kwamba, tuna fedha gani ya kuwasaidia hawa. Wanahitaji mitambo ya kisasa, wanahitaji zana za kisasa, wanahitaji kufanyiwa *training* na wanahitaji magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, mnakumbuka wiki mbili tatu mvua iliyonyesha wakati ule imenyesha zaidi ya siku tatu, nne, tano tu au wiki mbili, tatu mafuriko ya nchi nzima. Waliokwenda kutusaidia wale ni akina nani? Ni wanajeshi wenyewe. Ukiona Wanajeshi wanavyokwenda kusaidia pale wanakwenda kizalendo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotakiwa hapa ni kuwasaidia kuwapa zana ili kazi ya kwenda kusaidia kama ni kujenga barabara, kama ni kujenga daraja na kama ni kusaidia wananchi wawe na zana. Kazi ya siku mbili, tatu wanakwenda wiki nzima, *why?* Hapana. Tuone namna ya kuwasaidia hiki Kitengo cha Uokoaji katika Jeshi letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyumbu ni eneo kubwa sana na bado ninaliongelea sana. Hivi tukikaa kabisa tukasema tunatenga bajeti hii hapa tunataka Nyumbu sasa izalishe vifaru. Tunataka Nyumbu sasa izalishe magari ya kijeshi, tunashindwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Wachina wanaanza miaka 30 iliyopita walikuwa wana-*copy* na ku-*paste*. Wanachukua magari ya Ulaya, wanachukua magari ya Marekani wanayafumua wanayatengeneza kama hivyo wanaweka jina lao pale. Jeshini kuna watu wapo vizuri mno wamesoma. Mimi ninaamini hivyo na wana uwezo na ni wazalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala tu la kukaa kuona sasa hii Nyumbu tunaiwekea fedha gani shilingi bilioni 200, shilingi bilioni 500, kwa namna ambavyo watakavyofanya *visibility study* au *business plan.* Wataona namna ya kuihuisha hii Nyumbu ili iweze sasa kuzalisha magari, kuzalisha vitu pale ambavyo vitakwenda kulisaidia jeshi letu huko mbele ya safari na inawezekana tukauza hata nchi ya jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kuna nchi ndogo ndogo hapa Vietnam wanaanza kutengeneza vifaa, sijui Bulgaria. Bulgaria miaka 30 iliyopita walikuwa sawa na sisi tu. Wanafyatua risasi, wanatengeneza silaha, wanatengeneza kila kitu. Sisi tunashindwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Nyumbu pale ndio unaona kabisa hili jengo Watanzania waliopo hapa, uzalendo uliopo hapa, wanajeshi waliopo hapa, kilichobaki ni kidogo tu. Kupanga mikakati, kutenga bajeti kusukuma ili mambo yaende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya wanajeshi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ahmed, muda wako umekwisha.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa, tunamwita Mheshimiwa Nahodha, ajiandae Mheshimiwa Mama Kikwete, ajiandae Mheshimiwa Neema Kichiki.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninapenda kukushukuru na nitoe mchango wangu kwenye maeneo matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, jeshi letu kwa muda mrefu limekuwa likitoa msaada mkubwa sana wa ulinzi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndani ya Bara la Afrika na nje ya Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zama za sasa mbinu na medani za kivita zimebadilika sana na kwa maana hiyo basi, tunao wajibu kama Taifa tuliandae vizuri jeshi letu ili likabiliane na changamoto za karne ya 21. Katika karne hii vita vingi vya kimkakati havitapiganwa kwa kutumia mizinga mikubwa bali kama mwenzangu alivyosema hapa vitapigwana kwa kutumia roboti, mifumo ya *cyber* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo basi, ninalotaka kulisema hapa ni kwamba tunao wajibu kama Taifa tuangalie changamoto hizo ili tuweze kuwasaidia wanajeshi wetu. Nitataja maeneo matano ambayo Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania lina changamoto:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, mtakubaliana nami katika karne hii maadui wa nchi wanaweza kutumia mifumo ya *cyber* kuharibu benki, mashirika ya umeme, hospitali, vituo vya hifadhia *data* na kadhalika, kwa kutumia mifumo ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili, maadui wanaweza kuharibu hewa, maji na kwa kitaalamu tunaita *biologically and chemically warfare.*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya tatu, kadiri nchi yetu inavyoendelea ndivyo mahitaji ya wahandisi mahiri wanavyohitajika hasa katika miundombinu ya bandari, reli za kisasa, viwanja vya ndege na anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya nne, ninayotaka kuielezea hapa ni siasa za dunia katika karne hii zitahamia katika Bahari ya Hindi kwa sababu katika Bahari ya Hindi, kuna rasilimali kubwa sana kama mafuta, gesi asilia, madini, samaki na usafiri wa mizigo. Kwa maana hiyo basi mataifa yenye nguvu yatamimika sana katika eneo hilo. Ninapendekeza hapa Majeshi ya Maji katika nchi wanachama wa maeneo hayo wafanye mafunzo ya mara kwa mara ili waweze kukabiliana na changamoto ya Bahari ya Hindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya tano, Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania limekuwa likishiriki katika misheni mbalimbali za Kimataifa na kusema kweli jeshi letu limefanya kazi nzuri sana, kwa maana hiyo basi pamoja na umasikini wetu kuna haja sisi kama Taifa tuwaandalie vijana wetu malipo mazuri ya fidia kwa wanajeshi ambao kwa bahati mbaya watapata ulemavu wa kudumu na wale watakaopata vifo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ninaiomba Wizara ya Ulinzi ishirikiane na Chuo Kikuu cha Taifa Muhimbili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma ili kuandaa vijana wenye taaluma katika kozi nitakazozieleza; kozi za *Cyber Security, Space Technology, Military Medicine, Maritime Security* pamoja na *Mechatronic Engineering* ili tupate vijana wenye weledi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakubalina nami kwamba nchi yetu sasa inatekeleza miradi mikuu ya kimkakati Bwawa la Mwalimu Nyerere na reli ya Taifa. Miradi hii inahitaji ulinzi wa hali ya juu sana pamoja na mahitaji ya matengenezo ya kiufundi hasa miradi hii itapokamilika. Kwa maana hiyo basi kuna haja ya kuandaa vijana wetu wa jeshi wenye taaluma kwenye maeneo hayo ili miradi hii ikikamilika na yatakapotokea mahitaji ya matengenezo. Tusikimbilie nje kutafuta wahandisi wa nje, bali jeshi letu litoe msaada wa kiufundi na kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mama Kikwete, ajiandae Mheshimiwa Neema.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya wote nimshukuru Mwenyezi Mungu na hatimaye nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye yeye ndio Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yetu ya Ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampa pongezi Mheshimiwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu za msingi na sababu hizo si nyingine isipokuwa Mheshimiwa Mama na Amri Jeshi Mkuu, ameendelea kufanya kazi kuisimamia nchi yetu, hata pale nchi ilipopata misukosuko yeye aliweza kusimama imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa misukosuko mikubwa iliyojitokeza hivi karibuni ni pamoja na nchi kupata mvua zisizokuwa za kawaida. Mama amesimama imara na akawaambia Watanzania msiwe na wasiwasi na hata ile hotuba yake katika sherehe za kutimiza miaka 60 ya Muungano aliwaambia Watanzania kaeni, kuweni na subira, kuweni makini, yupo tayari kuhakikisha kwamba, miundombinu yote iliyoharibika tutairejesha na itakuwa salama, wananchi msiwe na wasiwasi. Huyu si mwingine bali ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyoona na kutambua kwamba Amiri Jeshi Mkuu ndio namba moja, hatimaye, yanafuatia majeshi mengine, yeye akisimama imara hata haya Majeshi yatasimama imara. Tunalipongeza Jeshi kwa kazi kubwa na nzuri inayoifanya na hapo kuna viongozi ambapo wanaongeza majeshi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jenerali Jacob John Mkunda, tunampongeza sana kwa kazi nzuri, Luteni Jenerali Salim Haji Othman, tunampongeza sana, Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele, tunawapongezeni sana kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax kwa kusimamia vizuri Wizara yake. Sambamba na hilo leo hotuba yake ameitoa vizuri sana tena sana, hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ulinzi na usalama; hali ya ulinzi na usalama wa nchi yetu ambayo taarifa imetolewa hapa ya mwaka 2023/2024 mipaka ya nchi yetu ipo shwari kabisa. Urefu wa mipaka ya nchi yetu ni zaidi ya kilometa 5,923.41, tunaambiwa mipaka ipo shwari kabisa. Usivione vinaelea hivi vimeundwa na waundaji si wengine bali ni pamoja na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa mipaka ya nchi kavu na mipaka ya maji yote ipo shwari, lakini pamoja na ushwari huo ambao unapatikana bado tuna changamoto kadhaa. Nitazitaja changamoto chache tu ambazo zinakabili mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa NaibU Spika, kama tunavyofahamu bila kuwa na usalama wa nchi, bila mipaka kulindwa vizuri hata haya mafanikio makubwa tuliyoyapata yanaweza yakaharibika. Kwa hiyo, tuna wajibu mkubwa wa kuendelea kulinda mipaka hii ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano Tanzania na Kenya kuna uharibifu wa alama za mipakani, lakini pamoja na uharibifu huo kazi inaendelea na kila kitu kinaendelea vizuri. Mipaka inapoanza kuwa na uharibifu hii ni hatari.

Sasa tukienda Tanzania na Malawi na kule kuna changamoto katika Ziwa letu Nyasa, lakini kazi nayo inaendelea

kuhakikisha hali inakuwa shwari. Kuna Tume maalumu ya usuluhishi na hili ni jopo la viongozi wastaafu. Tunawatakia kila la heri na mafanikio ili matatizo haya au changamoto hizi zimalizike haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna Tanzania na Msumbiji. Upande wa kule Kusini Mtwara na Lindi. Msumbiji kule kuna kadhia ambayo kadhia hii inaletwa kutokana na kundi la kigaidi linaloitwa *Ansar Al Sunna Wal Jamaah* hawa wapo katika eneo la Kaskazini mwa Msumbiji na katika Jimbo la Cabo Delgado. Hili Jimbo ndilo linalopakana na Mkoa wa Mtwara na Lindi yake kwa ujumla. *(Makofi)*

Sasa tutambue kwamba Mtwara na Lindi kuna miradi ya kimkakati. Kuna gesi asilia ipo Mtwara na Lindi, lakini kuna zao la korosho na zao hili ndilo linalotuingizia…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Kikwete hoja hizo zinazungumzwa kwenye Kamati.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na hayo nataka niwapongeze vilevile hawa Wana-Nyumbu. Nyumbu hawa wametengeneza bomu; na bomu hili ni bomu baridi la kuwafukuza tembo. Tunashukuru sana kwa sababu tembo walikuwa ni shida katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tunaomba hii bajeti ambayo mwaka huu imekuja ya shilingi trilioni 3.3 imekuja wakati muafaka na imeongezwa vizuri ukilinganisha na mwaka uliopita. Ahsante sana kwa kuongeza hii bajeti, tunawapongeza sana, tena sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika kutokana na suala la bomu, elimu itolewe yasije yale mabomu yakalia wakafikiria ndiyo wale watu wametoka huko sasa hivi wametuingilia kwenye maeneo yetu kumbe ni suala la bomu lile kuwafukuza hawa wanyama tembo au jina lingine wanaitwaje vile? Wanyama ndovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa 100%. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema, ajiandae Mheshimiwa Hawa.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Ulinzi pamoja na JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya na jitihada zake za dhati kabisa kuimarisha amani na utulivu katika Taifa letu na sote Watanzania tunajivunia kuwa katika Taifa letu na tunajivunia kuwa katika hali hiyo. Hali kadhalika nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha utulivu, mshikamano na demokrasia kwenye Taifa letu kupitia falsafa za *4R*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia ya hivi sasa inajielekeza kwenye kujiimarisha kwenye eneo zima la ulinzi dhidi ya vita ama dhidi ya matukio ama dhidi ya changamoto zozote zinazoletwa kutokana na matumizi hasi ya kidigitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishachangia mwaka jana hapa ndani ya Bunge kwamba Serikali ijielekeze katika kuwekeza zaidi katika kuwezesha jeshi kuweza kukabiliana na changamoto hizi za matumizi hasi ya kidijitali, lakini hata mwaka huu mwezi Februari niliishauri pia Serikali ione namna ambavyo italiongezea jeshi fedha ili waweze kuwa na mikakati, kujielimisha pamoja na kuwa na vifaa vya kuweza kupambana na kudhibiti *electronic warfare* (vita ya kidigitali). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumeona Taifa letu pamoja na mataifa mengine tulikuwa katika hali ya kutokuwa na *access*, kutokuwa na mtandao kwa takribani siku tatu mpaka siku tano. Kitendo hicho kimeleta athari mbalimbali, fedha zimepotea za kiuchumi kutokana na watu kushindwa kufanya kazi zao lakini hata imeongeza athari ya kiusalama katika kipindi hicho kwa sababu moja, hata mawasiliano ya ndege yalikuwa yanashindikana kwa hiyo zipo ndege ambazo zilichelewa kutoka, *bording pass* ilibidi zitoke bila kuwa *printed*. Zipo Balozi ambazo zililazimika kuandika *visa* kwa karatasi na kuwapa wale wasafiri

barua, lakini zipo Balozi ambazo zilifunga kabisa Balozi zao na kusitisha kutoa huduma ya *visa* kwa hofu ya athari ya kutokuwa na mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hilo ni dhahiri kabisa yapo matendo kama hayo yanayoweza kutokea kwa bahati mbaya, lakini pia yapo matendo ya namna hiyo yanayoweza yakatokea kwa makusudi kabisa ambapo wahalifu wakaamua kutumia mwanya huo kuingilia mifumo yetu ya fedha, kuingilia mifumo yetu ya kiusalama, kuingilia mifumo yetu ya kimawasiliano na kuliweka Taifa letu katika hatari kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi kwa unyenyekevu mkubwa sana naiomba sana Serikali ichukulie jambo hili kwa dharura, ione namna ambavyo itaipa fedha Wizara hii ya Ulinzi na kulipa fedha jeshi letu ili waweze kuwa na idara madhubuti ya masuala ya *cyber*, wanajeshi wetu waweze kupata elimu madhubuti ya namna ya kukabiliana na matukio haya, lakini pia na jeshi letu liweze kuwa na vifaa thabiti vya kuweza kudhibiti na kupambana na *electronic warfare* (vita ya kidijitali). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili, nilishasema mwaka jana na narudia tena kusema, kuna msemo ambao tunasema adui yako muombee njaa. Dunia imeshatambua kwamba kuna uhusiano wa karibu sana baina ya uhakika wa chakula na ulinzi na usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo inasema moja ya dira yake ni kulisha Tanzania na kulisha dunia. Hatuwezi kufikia hapo ikiwa bado tunategemea zaidi ya 60% ya mbegu zetu za chakula kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa, jeshi letu liweze kuwezeshwa, liweze kuingia katika kuzalisha mbegu. Ni kupitia kuzalisha mbegu ndipo tutajihakikishia usalama wa Taifa letu, usalama wa chakula tunachokula pamoja na changamoto mbalimbali ambazo wakulima wetu wanazipitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Taifa likitaka kukuangamiza, vita ya chakula ndiyo vita nyepesi kuliko zote na

ina athari kubwa sana. Tunaweza kununua mbegu kutoka nje, tukakuta mbegu zile wakulima wanapanda, chakula hakitoki. Tunaweza kununua mbegu tukakuta mbegu hizi zikifika kiwango fulani mazao yale yanashambuliwa na wadudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mbegu ni suala nyeti sana. Ikiwa sasa hivi dunia inahakikisha na inaweka jitihada, suala la mbegu ni la ulinzi na usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka jitihada kubwa sana kuimarisha sekta ya kilimo. Mimi niiombe sana Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ikiwa jeshi letu limewekeza kwenye ujenzi, ikiwa limewekeza mpaka kwenye *petrol station* ni kwa nini jeshi letu lisiwezeshwe liweze kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Taasisi za *ASA*, *TARI, TOSCI* ili jeshi letu liweze kuzalisha mbegu, ili tuwe na uhakika wa mbegu tunazitumia, mbegu ambazo tunatumia kwa ajili ya mazao ya chakula chetu ni mbegu ambazo hazina athari zozote kwa kizazi cha leo na kizazi cha kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kwa unyenyekevu mkubwa Serikali iweke jitihada za makusudi kabisa kuwezesha jeshi letu katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu na Mama yangu mpendwa Dkt. Stergomena Tax kwa kazi kubwa anayoifanya na kuendelea kuing'arisha Tanzania kwa kuwa moja ya nchi ambazo zinaongea kwa vitendo jitihada ya kuhakikisha tunaongeza ushiriki wa wanawake katika eneo hili la mahusiano ya Kimataifa katika ulinzi na usalama wa mataifa mbalimbali duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nalipongeza jeshi na viongozi wote wakiongozwa na *CDF,* lakini narejea tena naomba sana Serikali itafute fedha za dharura kuwezesha jeshi letu kuweza kujiandaa kudhibiti na kukabiliana na *electronic warfare* (vita za kidijitali), lakini pia wakati umefika jeshi liwezeshwe ili liingie katika kuzalisha mbegu ili kulinda ulinzi na usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja na niwaombe Wabunge wenzangu wote tuunge mkono hoja ya Wizara yetu hii muhimu kwa usalama wa nchi yetu, sote tunalala na tunaishi kwa amani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilisimama hapa Mheshimiwa Waziri, nikamwambia hivi Kikosi Namba 191 cha kule Kazimzumbwi, Kisarawe walifika katika Ofisi ya Serikali ya Kijiji kwa ajili ya kuomba eneo lenye mita 202 na kwa sababu tunafahamu jeshi na tunafahamu kwamba ardhi ni mali ya umma ambaye msimamizi wake mkuu ni Rais, sisi tukasema sawa kabisa walete barua ama maombi ya eneo hilo la mita 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwakubalia na kuwaletea barua wakati wanakuja kupima hizo mita 202, wakaenda zaidi wakachukua zaidi ya mita 202 na hapo ndipo sintomfahamu ilipoanza kati ya Wananchi wa Kazimzumbwi pamoja na Jeshi Kikosi Namba 191 kule Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamwambia Mheshimiwa Waziri kwamba baada ya ile mivutano ikafika mahali tukakubaliana mtatulipa fidia, lakini tangu mwaka 2011 na leo tunazungumza mwaka 2024 fidia hiyo takribani miaka 13 bado hamjatulipa. Mheshimiwa Waziri nitaomba utakapokuwa unakuja kujibu hapa katika shilingi bilioni 11 ulizozisema katika hotuba yako, Kisarawe Kazimzumbwi na kule Tondoroni tupo mahali gani au tuna kiasi gani za kulipiwa fidia ya maeneo yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya sisi kuridhia kabisa mchukue hili eneo kwa sababu tunafahamu umuhimu wa jeshi, tunafahamu kazi ya jeshi, kilichofuata ni kwamba kuna *ambush*, mnatukataza tusiendeleze, kujenga, kulima mnatukataza na mmeweka pale mabango kwamba hili ni eneo la jeshi huruhusiwi kufanya kitu chochote. Kama hivyo ndivyo, tunaomba mtuambie

fidia yetu mnatupatia na mtatupatia lini? Mheshimiwa Waziri mimi nitakuomba kama nimetangulia kusema tunaunga mkono bajeti yako na Wabunge wote wa Bunge hili tunaomba tuunge mkono kwa uzito wa Wizara hii, lakini nikuomba sana mara baada ya Bunge hili, tunakuomba uje Kisarawe, uzungumze na wananchi wa Tondoroni pamoja na wananchi wa Kazimzumbwi. Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho kabisa Mheshimiwa Waziri mimi nitakuomba ukija kujibu uje utuambie kwa sababu watu wa kutoka Wizarani kwako walivyofika wao wakasema wanafanya utambuzi, sisi hatuelewi utambuzi ni kitu gani, sisi tunaelewa tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufidiwa maeneo yetu tunachokijua sisi tunatakiwa kufanyiwa tathmini na sio utambuzi kwa sababu hatujapigwa picha na wala wale wananchi hawajajaza fomu wale wananchi. Sasa utakapokuja kutoa majibu hapa utuelezee kwamba huo utambuzi ndiyo tathmini na tutaenda kulipwa kwa minajili ipi ili hali fomu hatujajaza na wala picha hatujapigwa, tunaenda kulipwaje lipwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, atakapokuja kujibu Mheshimiwa Waziri anaomba atuambie shilingi bilioni 11 ni kiasi gani inaenda kwa wananchi wa Kisarawe, Kata ya Kazimzumbwi, Kijiji cha Kazimzubwi pamoja na Kijiji cha Tondoroni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nipende sana kumpongeza sana tena sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini pia nakupongeza wewe Mheshimiwa Waziri ninyi ni wanawake na nusu. Mnafanya kazi kubwa sana wamama ninyi, Taifa letu lipo limetulia kabisa, nchi yetu ipo imetulia kabisa chini ya wanawake mahiri na madhubuti. Kwa hiyo mimi nipende kuwapongeza sana kwani ulinzi wa nchi yetu upo imara. Kwa hiyo, nitaomba sana utakapokuja hapa utupatie majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja na ahsnate sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, ajiandae Waziri.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Wizara yetu ya Ulinzi na JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini napenda kumpongeza Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na Katibu Mkuu, lakini kipekee niwapongeze Mkuu wa Majeshi Jenerali wetu Jacob Mkunda, lakini nimpongeze Mnadhimu Mkuu, Jenerali Salumu Othman kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Kwa kweli nchi yetu ipo katika mikono salama, tumekaa kwa amani kwa sababu ya watu hawa pamoja na Wakuu wa Kamandi wote, Maofisa na Maaskari, tunatambua mchango wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nianze kwa kulipongeza jeshi letu kwa kazi kubwa wanayofanya, tumekwenda tumeona miradi ya Chuo cha *NDC* wamejenga majengo mazuri sana kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kujifunza mambo yote ya kiuongozi lakini pamoja na usalama. Ni kazi nzuri na ningependa hata halmashauri zetu zingeenda zikaone jinsi ambavyo jesho letu linatumia vizuri fedha na linafanya kazi kwa weledi na umakini mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo ningependa jeshi letu liweze kufanya tafiti mbalimbali, wanafanya tafiti lakini wapewe fedha kwa ajili ya kuendelea kufanya tafiti nyingine mbalimbali za masuala ya magonjwa mbalimbali. Nchi nyingine magonjwa haya mbalimbali wanapewa jeshi/kitengo cha jeshi kufanya tafiti na kuja na *outcome* yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningependa kushauri jeshi letu liweze kupewa hiyo nafasi na kuona namna ambavyo wanaweza wakafanya kazi hii nzuri kwa weledi mkubwa ili kutoa matunda yanayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jeshi letu huko mbele nafikiria waweze kupewa kitengo cha utafiti wa vyakula vinavyoingia

nchini lakini pia na mbegu na mazao ambayo tutazalisha nchini. Ninasema hivi kwa sababu tunaona athari ya vitu mbalimbali ambavyo vinakuja. Kwa hiyo, jeshi letu likipewa fedha kwa ajili na kufanyia kazi tafiti hizi wananchi tutakuwa salama kiafya na kila kitu na jeshi letu litafanya kazi kubwa. Tunaona JKT wamekuwa wakifanya kazi ya kilimo vizuri na kwa weledi mkubwa. Tunaomba wapewe fedha ili wafanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya Misri, jeshi linafanya kazi kubwa ya kilimo na linachangia zaidi ya 50% ya bajeti ya Serikali yao. Kwa hiyo, na sisi tukiiga mfano huo jeshi letu linaweza likafanya kazi kubwa sana ya kuzalisha na kulisha wananchi, pia kuchangia katika bajeti yetu kama watawezeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninawapongeza kwa kazi wanayofanya, lakini waongezewe bajeti ili waweze kufanya kazi kubwa zaidi na tunaweza tukauza hadi mazao nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni uwepo wa madeni. Majeshi yetu yamekuwa yanadai, taasisi mbalimbali za umma, halmashauri zetu hawalipi na wamekuwa wanafanya kwa kidogo wanachokipata wanafanya kwa weledi mkubwa sana. Ningependa Wizara msaidiane na taasisi zetu na mashirika yetu. Kwa mfano Kampuni Tanzu ya Mzinga inadai zaidi shilingi bilioni 1.9 kwa halmashauri zetu. Kuna halmashauri karibu nne ambazo zinadaiwa ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze lakini na Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba wawapelekee hawa wanajeshi wafanye kazi kubwa. Tunaongea hapa wametengeneza mabomu kwa ajili ya wanyama tembo lakini wanafanya kwa weledi mkubwa wangeweza kusaidia kama na fedha hizo zinaweza zikapatikana kwa wakati wakafanyia kazi. Kwa hiyo, hawa wanajeshi wanafanya kazi kubwa, Shirika la Nyumbu linafanya kazi kubwa ya kutengeneza vifaa vingi vya kiteknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba Serikali muwapelekee fedha ili waweze kuandaa vifaa, magari na vitu vyote ambavyo ni mazao ya kazi za jeshi ili waweze kufanya kwa weredi mkubwa kwa sababu kwa kweli ukienda pale unaona jinsi ambavyo wanajituma kwa moyo na wanafanya kazi. Ukiangalia thamani ya kitu wanachokitoa na fedha iliyotumika, unakuta kabisa ni tofauti ya ambavyo tunaona nje. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iyawezeshe haya majeshi yetu yaweze kufanya kazi yake kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna vifaa vinaagizwa kutoka nje; Jeshi linaagiza vifaa kutoka nje vinafika hapa, lakini vinatozwa kodi na vifaa hivi ni mazao ya Jeshi. Sasa kama ni mazao ya Jeshi, yanakaa pale bandarini, tunaomba wawatolee kodi au wawawekee kwenye *bonded warehouse* yakae pale. Kikubwa ni watoe hizi kodi kwa sababu hivi ni vifaa vyetu na mazao yetu ya kijeshi. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iweze kuangalia na kuwasaidia, Jeshi letu liweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mbona haujaunga mkono hoja? *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo, nalipongeza sana Jeshi letu imara kwa namna linavyofanya kazi zake kwa weledi. Pamoja na mambo hayo mazuri binafsi naona wanayo fursa ya kuongeza kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa wananchi ni matokeo ya usalama binafsi kwa wanajeshi wenyewe, asipo kuwa salama itapunguza motisha ya kuangalia usalama wa watu wengine. Tunaomba usalama wa wanajeshi wetu hasa huko Congo uimarishwe, inatuuma sisi tunajitolea kuwalinda majirani zetu, halafu wenzetu hawa sijui kama wanajali usalama wa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu huduma za afya ya akili Jeshini ni muhimu zikaimarishwa, pamoja na kwamba hawa ni wanajeshi, bado ni binadamu, hali ya kwamba hawaruhusiwi kugoma wala kuandamana ni sawa kijeshi, lakini kibinadamu ndiyo wanahitaji zaidi huduma za afya ya akili kwa ujumla kuliko watu wengine waliopewa fursa ya kuongea au kuandamana au kubisha. Hivyo, Kituo cha Afya ya Akili kama ilivyobadilishwa Mirembe sasa ni muhimu sana. Wanajeshi wanahitaji kupata huduma hizo za kisasa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Jeshi letu katika maono yake ni kuwa Jeshi lenye weledi mkubwa. Hivyo basi, elimu ni muhimu sana kwa wanajeshi wetu. Kuhakikisha wanapata elimu bora, lakini na wale wenye elimu watumike vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, tunaomba Jeshi letu litumike sana hata kutoa mafunzo kwa baadhi ya taasisi zetu au baadhi ya viongozi wetu ili kuongeza uzalendo kwa watu muhimu hasa viongozi wetu wasimamizi wa taasisi kama Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi, Waheshimiwa Wabunge na kadhalika. Hii itasaidia sana kuimarisha uhodari, uzalendo na kuondoa uvivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, tunashukuru kwa Jeshi kuchukua hatua kwa vijana wote wanaomaliza *form six,* hiyo ifanyike na kwa wale ambao wanaenda vyuo vya kati bila kusahau Jeshi la Mgambo litoe mafunzo kwa vijana wote walioko mitaani ambao hawajapitia jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake mbalimbali katika Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi wanavyoliongoza

Taifa letu na kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi yam waka 2020 hadi 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax - Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna Waandamizi, watendaji wote vikosini kwa kuendelea kuilinda nchi yetu wakati wote, hongereni sana na Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha nampongeza sana Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Wajumbe wake wote kwa jinsi walivyotimiza wajibu wao, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana ya ulinzi na usalama iliyowasilishwa hivi punde na pande zote mbili kwa maana ya Wizara na Maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba sana Serikali yetu ijitahidi kupeleka fedha zote zinazoombwa kwenye bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa ajili ya kufanikisha mpango wake wa mwaka 2024/2025 ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali iangalie utaratibu wa kuwapatia nafasi za ajira vijana wote wanaohitimu mafunzo kutoka JKT nchini kwa kuangalia utaratibu wa ulinzi katika sekta binafsi hususan maeneo ya biashara na huduma ili kuleta msawazo wa idadi, viwango vya mishahara kwa kuangalia sera ya walinzi kwenye maeneo kama hayo kwa kuwa kwa sasa wanaolinda wengi wao ni wazee sana na wengine hawana ujuzi, lakini pia mlinzi mmoja hulinda eneo kubwa zaidi ya uwezo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kufungua ofisi za Suma-JKT katika makao makuu ya mikoa na wilaya zote nchini ili kuongeza nafasi za ajira kwa vijana wote waliohitimu mafunzo yao hali itakayopunguza idadi kubwa ya vijana wetu hao mtaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali iangalie upya utaratibu wa kuwapatia vyeti vya uhitimu vijana wote wanaohitimu mafunzo yao ya mgambo katika wilaya zetu ili kutoa hamasa kwa vijana na endapo mhitimu ana sababu za kutokupewa cheti wahitimu waambiwe wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isimamie suala la kudumu kwa kutatua changamoto mbalimbali katika maeneo yanayopakana na makambi ya majeshi yetu na wananchi kote nchini ili kudumisha mahusiano mazuri kati yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa umuhimu naendelea kutambua mchango wa vyombo vyetu vyote vya ulinzi na usalama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja 100% na naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tena kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuongoza katika mjadala huu wa uwasilisha wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Aidha, napenda niendelee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa maono na miongozo yake katika kuiendeleza sekta hii ya ulinzi kama ambavyo wengi mmesema na kama ambavyo wengi mmempongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi ya leo katika Bunge lako Tukufu, niliwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na napenda kukushukuru sana kwa namna ambavyo umesimamia na kuongoza kwa umakini mkubwa sana mjadala huu wa bajeti ya Wizara ninayoiongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa. Najua leo ana majukumu mengine na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini na Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni na ushauri mliotupatia. Nawahakikishia kwamba ushauri huu tumeupokea kwa mikono miwili, tutaufanyia kazi na kuuzingatia kama ambavyo tumekuwa tukifanya siku zote, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza. Nilikuwa nafuatilia, lakini sijaambiwa kama tunao waliochangia kwa maandishi, lakini sijaona michango ya kimaandishi. Pia napenda kuwahakikishia kwamba tumezipokea hoja hizo na tuna imani kabisa zitaenda kuchangia katika kuimarisha utendaji na ufanishi wa Wizara. Maoni yenu tumeyachukua, tutayafanyia kazi katika kuboresha utendani na changamoto ambazo mmeziainisha pia tutazifanyia kazi. Wizara inatambua na kuthamini sana michango iliyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea hapa jumla ya Waheshimiwa Wabunge wanane wamechangia kwa mdomo, kwa hiyo, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitajiribu kujibu baadhi ya hoja zilizowasilishwa katika michango hii ikiwa ni pamoja na hoja au ushauri ulioletwa kupitia katika Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwepo hoja ya Bajeti, napenda kuwahakikishia, kuwathibitishia na kuwatoa hofu kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, imetoa uzito mkubwa sana kwenye sekta ya ulinzi ikiwa ni pamoja na katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwathibitishia hili tu Waheshimiwa Wabunge, katika kipindi cha miaka mitatu tu tangu

aingie madarakani, bajeti ya Wizara na taasisi zake imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutoka shilingi 2,358,694,986,000 katika mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia shilingi 2,713,787,405,450 katika mwaka wa fedha 2022/2023 na hili lilikuwa ni ongezeko la 13%; na kufikia shilingi 2,989,967,122,000 katika mwaka wa fedha 2023/2024 ambao ni mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la 9.24%. Katika mwaka wa fedha huu ambao nimewasilisha bajeti ambayo nilikwishaitaja ya shilingi trilioni 3.3. Hili ni ongezeko la 9.4%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza hizi zimeiwezesha Wizara na taasisi zake kutekeleza majukumu yake ipasavyo, lakini kama nilivyoeleza katika hotuba yangu, pia panapohitajika mahitaji mahususi fedha hizo zimeweza kutolewa na Serikali na kuiwezesha Wizara na taasisi zake ikiwa ni pamoja na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kutekeleza majukumu yake bila kutetereka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mtiririko wa bajeti, mpaka sasa hivi tumekwisha pokea kiasi cha 80%. Kwa hiyo, hii inadhihirisha, na hizi *figure* au takwimu hii ni ya mpaka kufikia mwezi wa nne, bado kuna miezi miwili. Kwa hiyo, tuna imani kabisa mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha huu, fedha zote zitakuwa zimekwishatolewa kama ulivyokwishasema Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuwe na imani, Serikali iko makini, inatambua umuhimu wa Wizara na taasisi zake na tumeendelea kupata kinachotakiwa na kilichopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililojitokeza katika mjadala na kwa uzito sana kupitia Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni kuhusu vifaa na mashine kwa ajili ya matumizi ya Jeshi kutozwa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili tumeendelea kulifanyia kazi kwa karibu sana kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha. Tumekwisha kuwa na mazungumzo ambayo yanapelekea kwamba tunaenda kulihitimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizo ni pamoja na kuwasiliana na Wizara ya Fedha kama nilivyosema na kufanya mapitio ya kodi la ongezeko la thamani na Sheria ya Fedha. Hatua hii itaendeana na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *The East African Community Customer and Management Act* inayoelekeza kuwa vifaa vyote vinavyoingizwa nchini kwa matumizi ya jeshi visitozwe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huu, Wizara imewasilisha mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Kodi katika Tume ya Kurekebisha Sheria ili kutoa msamaha kwa vifaa vyote vinavyoingizwa nchini kwa matumizi ya jeshi. Ni imani yangu, nilidhani Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo hapa, ni imani yangu kabisa kwamba kwa hatua tuliyofikia suala hili linaenda kuhitimishwa mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limesemwa kwa hisia sana na Kamati ya Bunge, lakini pia na Mheshimiwa Tendega, ni suala la uwepo wa madeni ya takribani shilingi bilioni 1.9 hususan kwa Taasisi ya Mzinga. Napenda kuwahakikishia kwamba suala hili pia tumelifanyia kazi kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya kampuni hii Tanzu ya *Mzinga Holding* ya shilingi bilioni 1.9 yanatokana na miradi mbalimbali ya ujenzi iliyotekelezwa kama mnavyofahamu. Aidha, hadi sasa madeni haya kwa ujumla mmeonesha kwenye taasisi za Serikali, lakini kiujumla ukichanganya na yaliyopo katika taasisi za sekta binafsi ni shilingi 1,998,000,000 kwa maana ya shilingi bilioni 1.9 ni Serikalini na milioni 98 ni katika taasisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyofahamu hususan Waheshimiwa wa Kamati ya NUU, lakini sasa kwa kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge wote na Bunge lako Tukufu, madeni haya yalikuwa zaidi ya hapa. Tulikuwa na deni la shilingi 4,095,000,000. Kwa hiyo, kwa hatua tulizozichukua deni hili limeweza kupungua na kubakia deni hili la bilioni 1.998. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua tunazozichua ni imani yetu kabisa kwa sababu tumeshafanya mazungumzo na tumeshachukua hata hatua za kisheria, wale wanaohitajika kupelekwa mahakamani tumewapeleka. Kwa hiyo, kwa hatua hizi tunazoendelea nazo, tuna imani kabisa kwamba tutaweza kukamilisha haya madeni mengine ambayo hayajalipwa. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa msisitizo na kwa kuona kwamba hii ni changamoto na tunawahakikishia kwamba tunalitambua na tunaendelea kulifanyika kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imezungumzwa na Kamati na Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge wa Lindi ameisisitiza, ni kuimarisha mipaka ili kudhibiti mianya na njia zisizo rasmi. Kamati imezungumza kwa njia mbalimbali, lakini pia Mama Kikwete ameongezea. Napenda tu kusema kwamba Wizara imeendelea kuimarisha ulinzi katika mipaka ya nchi yetu na nimesema katika hotuba yangu pia na kama nilivyoeleza hali ya mipaka yetu ni salama kabisa na ni shwari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto haziwezi kukosa, changamoto zitakuwepo hizi pia zinafanyiwa kazi inavyotakiwa kila zinapojitokeza. Aidha, Wizara imeendelea kuliwezesha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa zana na vifaa ili kutekeleza majukumu hayo ipasavyo. Naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara inaendelea kuwekeza kwenye mifumo ya kisasa ili kuhakikisha kuwa inadhibiti mipaka yetu kikamilifu ikiwa ni pamoja na njia zisizorasmi mipakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamesisitiza umuhimu wa teknolojia, wamesisitiza umuhimu wa kuwa na vifaa vinavyoendana na wakati na hiki ndiyo kinachofanyika, tunashukuru mmetukumbusha lakini niwahakikishie kwamba hili ndiyo tunaendelea kulifanya, ni suala endelevu linafanyika wakati wote kuhakikisha kwamba jeshi letu linavyo vifaa vya kisasa na katika ulinzi wa mipaka tunaweza kufanya kazi hiyo inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili kwa niaba ya Bunge lako Tukufu naomba sana kutoa shukurani zetu za dhati

kwa Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa uzito mkubwa anaoutoa kwa Jeshi letu katika kuhakikisha kwamba linawezeshwa kwa zana na vifaa vya kisasa katika kutekeleza jukumu lake la msingi la ulinzi wa mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyoeleza kuhusu ongezeko la bajeti, hiyo ni uthibitisho mmojawapo kwamba kweli Mheshimiwa Rais anatoa uzito unaotakiwa ili kuhakikisha kwamba Jeshi letu linaweza kuimarika, lakini yako mambo mengi makubwa yanayofanyika ambayo pia ni ya kukakikisha kwamba Jeshi letu linaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kushirikiana na Wizara, liliongelewa suala la mipaka na Waheshimiwa Wabunge kadhaa na ulitolewa mfano, nafikiri alikuwa Mheshimiwa Mama Kikwete sasa nakumbuka kwamba kuna kati ya mpaka wetu na Kenya na Mpaka wetu na Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tu kusema kwamba tunaendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kuhakikisha kuwa barabara na alama za mipaka zinaendelea kuimarishwa. Hii ni kazi inafanyika, tumefanya kwa kiasi fulani katika mwaka huu wa fedha unaoendelea na tutaendelea kuifanya ili tuweze kuikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mpaka wa Malawi, hilo linasimamiwa chini ya Wizara ya Mambo ya Nje lakini tunashirikiana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kuimarisha viteule vilivyopo mipakani na kuviwezesha kufanya doria za mara kwa mara. Pia tunaendelea na kusimika mifumo ya ulinzi mipakani. Kwa hiyo, haya yote yanafanyika ili kuhakikisha kwamba kweli mipaka yetu iko imara na inaendelea kuwa imara kwa sababu ni imara, lakini tunaishi katika dunia ambayo ina matishio mbalimbali na wakati wote sisi tunatakiwa tuwe tumejipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia liliongelewa suala la umuhimu wa kuendeleza na kuboresha mashirika yetu ya Nyumbu na Mzinga na liliongelewa na Kamati na Mheshimiwa Tendega amelisisitiza sana. Napenda tu kusema kwamba Wizara inatambua umuhimu wa mashirika haya kwa maslahi mapana ya Taifa letu na jeshi na ulinzi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu huu, Wizara imeendelea kutekeleza mpango wa miaka kumi wa kuimarisha Shirika la Mzinga. Nilieleza katika hotuba yangu kwamba tunao Mpango wa miaka kumi0 wa Kuliimarisha Shirika la Mzinga. Kwa hiyo, mpango huu utekelezaji wake unaendelea. Hela imeshatengwa, inaendelea kutolewa mwaka hadi mwaka na hatua za utekelezaji za kufanya masuala mbalimbali zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Shirika la Mzinga, Wizara ipo katika hatua ya awali ya kuanzisha *Mzinga Two*. Tunataka tuanzishe kiwanda kingine ambacho kitakuwa kinaongezea nguvu na kinaenda na mahitaji ya wakati wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu rasilimali watu, Wizara kupitia jeshi na taasisi zake tumeendelea kuwawezesha na vilevile Ofisi ya Utumishi imeendelea kutupatia watumishi awamu kwa awamu. Hivyo, nawaahidi Waheshimiwa Wabunge kuwa tunaendelea kuyaimarisha mashirika yetu haya ili kutimiza azma ya kuanzishwa kwake. Hivyo nawaomba mtupitishie bajeti ambayo naileta hapa, imejumuisha bajeti ya mashirika haya ili yaweze kuendelea kufanya kazi zake na yaendelee kujiimarisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liliongelewa suala la Sera ya ulinzi; hoja ya kukamilisha Sera ya Ulinzi, maandalizi ya sera yameendelea, yamefika mbali. Tumeshafanya tathmini ya hali ya ulinzi na usalama kwa sababu hiyo ndiyo inawezesha kuandaa hiyo sera. Tumeshafanya mazungumzo na upande wa pili na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na tumeshapata maoni yao, lakini suala hili limesimama kidogo kwa sababu kuu mbili; sababu ya kwanza, tuko katika mchakato wa kuandaa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 mpaka 2050 na wakati huo

huo tunaendelea na maandalizi ya Sera ya Mambo ya Nje kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya yote yatakuwa yana uhusiano wa karibu na Sera ya Ulinzi. Kwa hiyo, tukienda haraka kukamilisha Sera ya Ulinzi sasa hivi, tunaweza tukajikuta tumeacha mambo ya msingi ambayo yanatokana na Dira ya Taifa na Sera ya Mambo ya Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge, Sera ya Ulinzi ya Mambo ya Nje ya sasa ilivyo imejumuisha eneo ambalo linahusiana na mambo ya ulinzi na usalama. Kwa hiyo, baada ya hii michakato miwili kukamilika, nawahakikishia kwamba tutaweza kukamilisha sera hii kama itakavyokuwa imekubalika katika mijadala inayoendelea kwa sababu sasa hivi haya masuala yote mawili yanajumuisha wadau wote kitaifa ili kila eneo liweze kutoa mawazo yao. Pengine mnaweza mkaja mkasema hatuhitaji tena Sera ya Ulinzi. Sijui, kwamba kila kitu kimejumuishwa katika Sera ya Mambo ya Nje, sijui. Kwa hiyo, ndiyo maana tunajipa muda ili tuweze kuja na kitu ambacho kitakuwa ni sahihi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo pia maeneo mengine ambayo yaliongelewa sana ambayo niyajumuishe kwa ujumla wake; Mheshimiwa Nahodha, Mheshimiwa Ahmed Salum, Mheshimiwa Lugangira na hata Mheshimiwa Tendega, wameongea kwa njia tofauti, lakini hoja kubwa iliyokuwa inajitokeza ni kuhusu kuliimarisha jeshi letu kivifaa, kiteknolojia, kimafunzo na kiutaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda tu kusema kwamba jeshi letu liko vizuri sana lakini hatusemi kwamba kwa sababu tuko vizuri sana hatuna sababu ya kujifunza na kwenda na wakati. Ni kweli tuko katika karne ya 21, mahitaji yanabadilika na sisi wakati wote tunajitahidi kwenda na mahitaji ya wakati. Kwa hiyo, haya yote mliyoyasema tutayazingatia wakati wote, wakati wa utekelezaji na kwa kadiri tunavyoendelea kuliimarisha jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuko katika karne mpya, *cyber security, technological warfare* na *food security* inayoendana na usalama kwa ujumla wake ni lazima tuizingatie. Kwa hiyo, yote haya tumeyapokea, tutaendelea kuyafanyia kazi na hata katika kuliboresha jeshi letu kitaaluma na kiteknolojia, yote haya tunayazingatia. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umetolewa ushauri kuhusu kufanya ushirikiano na vyuo. Tunapokea na tunafanya hivyo na siyo vyuo tu, tunafanya ushirikiano na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyosikiliza huu mjadala kwa mapana yake, nimeona ni mjadala ambao hauihusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa peke yake, ni mjadala unaoihusu Serikali kwa ujumla wake. Kwa hiyo, hapa sisi tutayachukua na tutaenda kukaa chini kama Serikali na tuone kwamba tunaweza kushirikiana kwa namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ukisema Jeshi lisimamie uzalishaji wa mbegu bora, tunafanya lakini lazima tushirikiane na Wizara ya Kilimo. Tukisema twende kwenye masuala ya *cyber security*, tunafanya lakini lazima tushirikiane na Wizara ya Habari na Teknolojia na Wizara ya Mambo ya Ndani. Haya yote ni mengi ambayo mmeyasema, kwa hiyo, niwahakikishie tu kwamba tutaendelea kushirikiana kama Serikali na tunajua kabisa umuhimu na msisitizo mlioutoa, kwa hiyo, tutalifanyia kazi inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo yote haya ni mengi ambayo mmeyasema kwa hiyo niwahakikishie tu kwamba tutaendelea kushirikiana kama Serikali na tunajua kabisa umuhimu na msisitizo mlioutoa kwa hiyo tutalifanyia kazi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ambayo napenda kusemea ni ya Mheshimiwa Hawa ambayo yeye ameelezea kuhusu maeneo yaliyotwaliwa kwamba yanatakiwa kulipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijajibu hoja hii ya *specific* nipende tu kutoa shukrani sana kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mnaotupatia kwa sababu jeshi bila kupata maeneo utekelezaji wa baadhi ya majukumu utakuwa mgumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata katika utatuzi wa migogoro hii tumefanya pamoja nawashukuru sana. Tulikaa chini tulipohitaji maeneo ya ziada tumekaa pamoja mmeweza kutuelewa na tuendelee kufanya kazi pamoja katika eneo hili na ni kweli tumetoa maeneo mbalimbali kwenye hili hapa ambalo ukiangalia katika kitabu hiki maana yake amesema anataka kauli ulisema kweli Mheshimiwa mwaka jana na nilikuhaidi nitafanyia kazi na tumefanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika kitabu cha hotuba jedwali la pili na jedwali la kwanza, jedwali la pili linaonesha maeneo ambayo yalipimwa na kulipiwa fidia na hapo ukiangalia kwa mwaka 2022/2023 namba 14 tuna Tondorani, Pwani ambapo fidia ya shilingi 46,712,720 ililipwa Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Katika kitabu hiki hiki ukiangalia jedwali na kiambatanisho namba moja hicho nilichokuwa nimekirejea ni kiambatanisho namba mbili kuna maeneo ambayo hayajalipiwa fidia lakini tumeshayafanyia tathimini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo namba moja katika jedwali hilo ni hiyo KJ191 ambayo umeirejea ambayo pia hii katika uthamini tunatarajia kuwalipa shilingi 2,520,249,865 kwa hiyo hii hapa uthamini umeshakamilika kilichosalia sasa hivi ni kwenda kulipa hiyo fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nihitimishe kwa kuanza na kwa niaba ya watumishi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa au Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Taasisi zake kupokea shukrani na pongezi za dhati ambazo mmetupatia kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika ya kulinda mipaka yetu na kudumisha amani na aidha, napenda kuwahakikishia kuwa Wizara ya Ulinzi na taasisi zake ikiwemo Jeshi

la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania tutaendelea kutekeleza majukumu yetu kwa weledi, umahiri na uzalendo na hii ndiyo misingi ya utendaji wetu wa kazi na tutaiendeleza daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya hivi tukitambua kwamba Amiri Jeshi Mkuu yupo nyuma yetu akitusimamia, akituangalia na akitaka kuhakikisha kwamba kweli tunafanya maukumu yetu kama inavyotakiwa na hatutakuwa tayari hata dakika moja kumuangusha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi ambazo mmezitoa kwa Wizara naomba nichukue kwamba ni pongezi ambazo zinatolewa kwetu, lakini zinatolewa kwa Amiri Jeshi Mkuu ambaye ndiyo msimamizi namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufafanuzi huo na kabla sijahitimisha hoja yangu naomba niwashukuru tena kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii na hata waliosikiliza na waliofuatilia hotuba hii na mjadala, naamini tutaendelea kushirikiana katika kudumisha ulinzi na amani na kuwaletea Watanzania maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upekee napenda niwapongeze watendaji wote wa Wizara na taasisi zote wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe kwa upande wa Wizara na Jenerali Jacob John Mkunda, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi kwa upande wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kufanya kazi kwa weredi na kujituma na kuwezesha kufikia hatua hii ambapo tunaelekea kuhitimisha mjadala wa bajeti ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada kubwa zinazofanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais na Amiri Jeshi Mkuu katika kudumisha amani na kuwaletea wananchi maendeleo zinapaswa kuungwa mkono na sisi sote. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inamshukuru kwa dhati kwa namna ambayo amekuwa akisimamia ulinzi na usalama na kuwa mstari wa mbele katika kutatua changamoto zinazoikabiri Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zake tangu aingie

madarakani, lakini changamoto zinazolikabili Taifa letu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa pia mstari wa mbele kuimarisha diplomasia ya ulinzi na ameendelea kuiletea heshima nchi yetu, tuendelee kuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu mpendwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kuwa chini ya uongozi wa Amiri Jeshi Mkuu Wizara ya Ulinzi na taasisi zake ipo imara ili kuhakikisha kuwa nchi yetu ina amani, ipo shwari, ni imara wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha naomba nitoe wito kwenu wote Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kuwa ulinzi wa Taifa letu ni jukumu la kila Mtanzania na kila mmoja wetu analo jukumu la kutekeleza wajibu huo. Wananjeshi wetu na watendaji wote wanafanya kazi kubwa sana usiku na mchana kwa weledi, uhodari na uzalendo wa hali ya juu. Nawapongeza sana kwa moyo huo wa kujituma na kwa kazi kubwa wanayoifanya niwaombe sote tuwaunge mkono na kutoa ushirikiano na tusiwakatishe tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha; naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe kiasi cha shilingi 3,326,230,419,000 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kati fedha hizo shilingi 3,008,812,907,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 317,417,512,000 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante hoja hiyo imetolewa na hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*......................Sh. 22,004,407,400

**MWENYEKITI:** Rudia tena.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*......................Sh. 22,004,407,400

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaingia kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri, nina mjumbe mmoja Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwenye Wilaya ya Mbozi kuna kambi ya jeshi 845KJ ya Itaka na kwa muda mrefu kulikuwa na mgogoro kati ya wananchi na kambi ya jeshi. Niishukuru Serikali kwamba mgogoro ule umeisha ila kilichobaki ni kwamba wale wananchi wamechukuliwa mashamba yao, nyumba zao, kahawa zao na walitegemea kwamba fidia ambayo ingelipwa ingewawezesha

wao kwenda kununua mashamba mapya na kujenga nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni miaka miwili uhakiki wa fedha umeshafanyika, wale wananchi wanaishi kwenye mazingira ya shida sana.

Sasa nataka Mheshimiwa Waziri anihakikishie ni lini wananchi wa Kijiji cha Sasenga, Kijiji cha Mboji na Kijiji cha Itewe kwenye Kata ya Itaka watalipwa fedha zao ili waendelee na maisha yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George hili swali la kisekta siyo la kisera.

Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye *guillotine*. *(Makofi)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*......................Sh. 22,004,407,400
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…….........Sh. 313,110,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*…….........Sh. 845,822,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……..........................Sh. 323,697,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…......Sh. 268,000,000
Kifungu 1006 – *Legal Service Division*………..................Sh. 313,757,200
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*.......Sh. 93,760,200
Kifungu 1009 – *Information and Communication Technology Unit*……………...........……….Sh. 402,200,000
Kifungu 2001– *Industries, Construction and Agriculture Division*…………………………….....….....Sh. 354,432,000
Kifungu 2002 – *Military Research and Development Division*..................................................Sh. 970,021,400
Kifungu 2004 – *Estate Management and Building Consulting Division*…………….....….....Sh. 571,776,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 38 - Ngome**

Kifungu 1001 – *National Defence Headquarter (NDHQ)*......................................Sh. 2,474,140,235,000
Kifungu 1006 – *Defence Forces Headquarter Command (DFHQC)*……..…………Sh. 2,855,375,000
Kifungu 1007 – *Land Forces Command (LFC)*…......Sh. 4,144,693,000
Kifungu 1008 – *Air Forces Command (AFC)*….........Sh. 3,886,107,000
Kifungu 1009 – *Navy Command (NC)*……….....….Sh. 2,395,233,000
Kifungu 1010 – *Military Hospitals (MH)*…...................Sh. 3,318,291,000
Kifungu 1011 – *Reserve Force Command (RFC)*.........Sh. 700,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 – *The National Service Force*...........Sh. 490,652,279,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*….............Sh. 400,000,000
Kifungu 1009 – *Information and Communication Technology Unit*………………………Sh. 2,500,000,000
Kifungu 2001– *Industries, Construction and Agriculture Division*…………………......…..…Sh. 62,329,501,566
Kifungu 2002 – *Military Research and Development Division*...........................................Sh.174,106,718,122
Kifungu 2004 – *Estate Management and Building Consulting Division*……….....….…Sh. 20,663,780,312

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 38 - Ngome**

Kifungu 1001 – *National Defence Headquarter (NDHQ)*..............................................Sh. 48,867,636,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39- Jeshi La Kujenga Taifa (JKT)**

Kifungu 1001 – *The National Service Force*...............Sh. 8,549,876,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa Taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake, hivyo naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa sasa nitawahoji kwamba Bunge likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki, kwa hiyo hii sasa ni rasmi Bajeti ya Waziri yako Mheshimiwa Waziri imepita hongera sana wewe na Vyombo vyako kwa kweli mnafanya kazi nzuri sana. Changamoto haziwezi kukosekana popote, lakini kwa kweli mnalitendea haki Taifa letu.

Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuongeza bajeti kwenye Wizara hii yote kwa kuona umuhimu wa Wizara hii na chombo hiki ambacho muhimu sana kwa Taifa letu.

Kwa hiyo, mimi navipongeza vyombo vyetu *CDF*, *Chief of Staff* na wataalamu wote ambao mpo. Tunapongeza na ma-*CDF* wa zamani ambao na wao wametufikisha hapa katika amani ya Taifa letu na wote waliochangia amani kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.54 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 21 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*